29 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 29 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tuko kwenye Kikao cha Thelathini na Tisa, leo tarehe 29 Mei, 2026.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2025.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Ahsante.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Ninamwita sasa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, aulize swali lake.

Na. 458

Kukamilisha Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Songea

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Songea ambayo inategemewa na wananchi wengi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif**.**

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni moja ya hospitali 25 zilizoanza ujenzi katika awamu ya tatu, mwaka wa fedha 2021/2022. Mpaka sasa hospitali hiyo imepokea jumla ya shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Kuhudumia Wagonjwa Nje *(OPD),* Jengo la Maabara, Jengo la Mionzi, Jengo la Utawala, Jengo la Wazazi, Jengo la Kufulia na Jengo la Kuhifadhia Dawa. Aidha, Hospitali ya Manispaa ya Songea imeanza kutoa huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* na vipimo mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya watoto, wodi ya magonjwa ya ndani wanaume na wanawake, pamoja na *store* ya chanjo katika Hospitali ya Manispaa ya Songea. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafar kwa majibu haya mazuri yenye kuleta matumaini kwa Wana-Songea. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa kuwa Mji wa Songea ni mmoja ambao unakuwa kwa kasi, hasa ongezeko la idadi ya watu. Nini mpango wa Serikali kupanua huduma hususan huduma za madaktari bingwa katika hospitali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba kwa kuwa Mji wa Songea unazidi kupanuka, idadi ya watu inavuka 500,000 kwa hivi sasa na katika hospitali hiyo kuna *ambulance* moja tu. Nini mpango wa Serikali wa kuongeza idadi ya *ambulance* katika hospitali hiyo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti,

ninaomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya kwenye huduma za kibingwa, kwanza tuko katika *level* za hospitali zote za mikoa, *Regional Referral Hospitals* na katika hospitali za wilaya baadhi ambazo tunaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kufanya mawasiliano na wenzetu wa Wizara ya Afya ili kuona ni namna gani tunaanza huduma za kibingwa katika hospitali yetu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika halmashauri yetu hii, angalau kwa awamu ya kwanza waliweza kupata *ambulance* mbili, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa maana amewaombea wananchi hawa na idadi ni kubwa na anakidhi vigezo, kwa maana ya kwamba halmashauri zile za pembezoni zitaangalia ni namna gani *ambulance* zile ambazo tunazipokea kutoka Wizara ya Afya tuweze kumuongezea na wananchi waweze kupata huduma hii bora kabisa ya kuhudumia mama na ndugu zetu katika maeneo hayo. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Daktari, Mheshimiwa Johannes Lukumay.

MHE. JOHANNES L. LUKUMAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali na ninachukua nafasi hii kumshukuru kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa shilingi bilioni 5.5 iliyosababisha kujengwa na kumalizika kwa vituo vitano vya afya katika Jimbo la Arumeru Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivyo vituo vitano, vinne vinatoa huduma ya upasuaji, hususan upasuaji wa mama wajawazito, lakini vituo vitatu havina nyumba za watumishi kabisa, inayosababisha watumishi wale wakae mbali zaidi na vituo vya afya.

Swali, je, lini Serikali itajenga nyumba za watumishi katika Kituo cha Afya cha Oldonyosambu, Mbuyuni, Oloirien na Nduruma ili

wananchi hawa waende kupata huduma iliyokusudiwa? Ninashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Lukumay, Mbunge na pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imeeleza Bunge lako Tukufu ni namna gani *approach* ya kwanza ya kujenga nyumba za watumishi. Lengo hasa ni kuhakikisha zile halmashauri za pembezoni zenye uhitaji mkubwa tunaanza ujenzi wa nyumba za watumishi katika maeneo hayo ili waweze kutoa huduma bora na wapate utulivu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mji wa Tarime inahudumia wananchi wa Mji wa Tarime, Wilaya ya Tarime, wengine wanatoka Rorya na hata nchi jirani ya Kenya. Naishukuru Serikali kwa kutujengea jengo jipya kabisa la mama na mtoto, lakini bado kuna mahitaji ya huduma ya watoto wachanga au njiti, *(Radiant Warmer, UT Warmer Baby Coat Five)*, pamoja na *phototherapy machines.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hiyo ni ya zamani, imechakaa, *OPD* ni mbovu kabisa na haifai, pamoja na jengo la utawala. Nataka kujua sasa ni lini Serikali itapeleka fedha, ili kuweza kujenga Jengo la *OPD* na la utawala kuweza kuendana na ukarabati wote ambao imeufanya wa *EMD,* hiyo *maternity complex* na vingine? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla pongezi ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa na zile ambazo Mheshimiwa Lukumay ametoa, hakika zinakwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ameweka fedha, ameweka nguvu yake yote katika kuhakikisha huduma za afya zinakuwa bora na tumeweza kupata heshima kimataifa kwamba Tanzania tunazidi kupambana kuzidi kupunguza tatizo la mama na mtoto. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Matiko kwamba tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha tunajenga hizo wodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kurekebisha zaidi ya hospitali 49 zile kongwe, kuhakikisha tunaweka miundombinu sawa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Esther kwa mwaka huu wa fedha ambao tumeendelea kutenga, zaidi ya hospitali 105 zitapata fedha kati ya shilingi milioni 600, shilingi milioni 700 na shilingi milioni 800, kuhakikisha tunakamilisha miundombinu hii. Kwa hiyo, wananchi wale wataendelea kupata huduma na tutakamilisha *OPD* ambayo Mheshimiwa Esther ameiomba hapa. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakati Makamu wa Rais anapita kutafuta kura katika uchaguzi wa mwaka 2025 alitoa ahadi kwamba Serikali imeona ukubwa wa Wilaya ya Same kwa hiyo, imeamua kujenga Hospitali ya Wilaya upande wa Jimbo la Same Mashariki. Je, Serikali itaanza lini kuijenga hospitali hii kwa sababu sasa wananchi wanauliza mara kwa mara? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti,

ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba anafuatilia na kuona namna gani Serikali itaendelea kutimiza ahadi ambayo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliitoa. Ofisi ya Waziri Mkuu, tumesema katika Bunge lako Tukufu kwamba ahadi zote za viongozi wetu wakuu wa nchi tutahakikisha tunazitimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri alete andiko, waanze kutenga eneo na tuanze ujenzi katika eneo hilo hata angalau kwa kutenga eneo ili tuweze kutenga bajeti ya kujenga angalau kwa awamu. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakuona Mheshimiwa Boniphace Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Serikali imetujengea hospitali nzuri sana pale Nyamuswa, Bukama, lakini hospitali hiyo toka mwaka 2019 mpaka leo ina waganga watatu. Sasa ni lini Serikali itapeleka waganga na wahudumu kwenye hospitali ili ifanye kazi vizuri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri wataalamu katika hospitali zetu zote nchini na tunakumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais, tuliweza kupata vibali vya kuajiri wataalamu zaidi ya 5,000 katika hospitali zetu na wamesambazwa kote nchini. Tayari tunaendelea kuratibu, kuona upungufu katika maeneo mbalimbali ili tuendelee kuongeza watu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Getere kwamba tutaendelea kuongeza watalaamu katika hospitali

zetu hizi ili wananchi waweze kupata huduma ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameikusudia. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alan Thomas.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika Wilaya ya Kakonko kipo Kituo cha Afya Mganza ambacho kipo karibu na Kakonko Mjini, kinahudumia Kata ya Kakonko, Kiziguzigu, Kanyonza, Kasuga na Lugenge. Ni upi mpango wa Serikali kuongeza gari la wagonjwa ili kuweza kuboresha huduma katika eneo la afya? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama alivyouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri Mheshimiwa Mbunge wa Kakonko tunafanya mawasiliano ya mara kwa mara, huwa anakuja kwenye dawati na pia pale Wizarani ili kuona namna gani tunaboresha huduma katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kulingana na tunavyopokea magari kutoka Wizara ya Afya tutahakikisha tunaangalia, kwa sababu na yeye anaingia kwenye vipaumbele vya halmashauri ambazo ziko pembezoni na majimbo ambayo yako pembezoni ili waweze kupata huduma ya gari la wagonjwa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula Magangila.

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wananchi wa Jimbo la Msalala, Kata ya Busangi na Kata ya Jana wanasafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya kituo cha afya na inasababisha akinamama wanajifungua njiani. Ni upi mpango wa

Serikali kupeleka pesa na kujenga vituo vya afya kwenye hizi Kata za Busangi na Vyalo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Msalala, ndugu yangu huyu, njia moja nikiwa ninaelekea Jimboni Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba zile fedha ambazo tuliomba za vituo vya afya vya kimkakati, ukiacha vile 120 ambavyo tayari tumejenga, tayari tumeomba fedha Hazina ili kuhakikisha tunajenga vituo vya afya vya kimkakati na yeye ni mnufaika katika Jimbo hilo la Msalala ili kuweza angalau kujenga kituo cha afya cha kimkakati kitoe huduma kwa mama na ndugu zetu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Bado tuko Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; namwita Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Kivule, aulize swali lake.

Na. 459

Ujenzi wa Barabara ya Kitunda – Nyangasa – Kibeberu hadi Magole kwa Kiwango cha Lami

MHE. DOUGRAS D. MASSABURI aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa madaraja na Barabara ya Kitunda – Nyangasa – Kibeberu hadi Magole kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu, kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Jimbo la Kivule, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kibeberu kwenda Magole ina urefu wa kilometa 2.89 na ni kiungo muhimu kwa wananchi wa Kata ya Mzinga na Kitunda. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 barabara hii imejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 127.13. Serikali imekuwa ikitenga bajeti kuhakikisha Barabara za Kitunda – Nyangasa – Kibeberu hadi Magole zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imejikita katika ujenzi wa Barabara ya Kitunda – Mwangati – Kwa Mpalange ambapo katika bajeti ya mwaka 2026/2027 kiasi cha shilingi milioni 950 kimetengwa. Ujenzi wa Madaraja na Barabara za Nyangasa – Kibeberu na Magole itawekwa kwenye bajeti baada ya kukamilika kwa Barabara ya Kitunda – Mwangati - Kwa Mpalange. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dougras Massaburi, maswali ya nyongeza.

MHE. DOUGRAS D. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali ya kaka yangu Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya TAMISEMI na Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kaka yangu Mheshimiwa Chalamila na *DC* wetu wa Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 8 Mei, niliuliza swali linalohusu Barabara ya Banana – Kitunda mpaka Msongola na hatua za haraka zikachukuliwa. Ninaipongeza Serikali yangu, zaidi ya shilingi bilioni nane zimelipwa na sasa mkandarasi yuko kazini kukamilisha barabara hiyo kwa kiwango cha lami, lakini pamoja na pongezi hizo sasa ninayo heshima kubwa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kivule, niulize maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; tunayo barabara inayotoka *Kampala University* kupita Majohe mpaka Chuo Rada, kilometa 6.35. Swali la pili, ni barabara inayotoka Njia Nne kupita Buyuni – *PSSSF* mpaka Taliani, inaunganisha Jimbo la Kivule na Jimbo la zamani la Ukonga; na kwa kuwa Serikali yetu sikivu ilitupatia jimbo hili jipya la Kivule, changamoto kubwa ni miundombinu ya barabara na nyakati hizi za mvua kumekuwa na changamoto kubwa ya kupitika kwa barabara hizo. Basi angalau siku ya leo tupate majibu ya Serikali kwenye maswali yangu mawili ya nyongeza katika Wizara yetu ya TAMISEMI. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Jimbo la Kivule kwa uchapakazi wake na kwa kweli anawawakilisha ipasavyo wananchi wa Jimbo la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napokea pongezi zake kwa Serikali yetu na kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli, kwa hakika Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kazi kubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya barabara na katika Jimbo la Kivule, Mheshimiwa Mbunge ameshuhudia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Barabara ya kutoka *Kampala University* – Magohe – Rada, kilometa 6.35 na Barabara ya Njia Nne - Buyuni, ni barabara muhimu sana ambayo inaunganisha wananchi wa Taliani – Magohe. Ni barabara ambazo kwanza kwa kutambua umuhimu wake Serikali imeshaziweka kwenye Mpango wa *DMDP II,* inakwenda kujengwa kwa ile 70%. Hivi sasa wanaendelea na taratibu za manunuzi ili kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa barabara hizi, Serikali imefanya maamuzi na sasa zitajengwa kwa kiwango cha

lami. Kwa mfano katika mwaka huu wa fedha wakati tunajiandaa na ujenzi wa lami, imekwishatengwa shilingi milioni 20 kwa ajili ya matengenezo madogo madogo. Mwaka wa fedha 2026/2027 imetengwa shilingi milioni 950 kwa ajili ya ujenzi kiwango cha lami kilometa 0.6. Pia imetengwa shilingi milioni 100 kwa ajili ya matengenezo madogo madogo *(periodic maintenance)*, na imetengwa shilingi milioni 20 kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi. Barabara hii yote jumla yake ni kilometa 5.26 na zote zitajengwa kiwango cha lami kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kivule kwamba Serikali iko kazini, itahakikisha barabara hizi zinajengwa na zinapitika vizuri kwa manufaa ya wananchi.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Exaud Kigahe.

MHE. EXAUD S. KIGAHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Ifwagi – Mdabulo; kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea lami kilometa 14 kutoka pale Mtili – Ifwagi.

Je, ni lini barabara hii itakamilika sasa kuendeleza ujenzi chini ya Mradi wa *RISE* kutoka Ifwagi – Mdabulo – Ibwanzi ambako pia kuna madaraja katikati yake?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Mheshimiwa Exaud Kigahe, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa Barabara ya Ifwagi – Mdabulo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwamba Serikali tayari imekwishaweka utaratibu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kupitia Mpango wa Kuboresha Uchumi na Huduma za Jamii

(RISE). Tayari tunaendelea na hatua za ujenzi wa barabara hiyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo itajengwa kwa wakati. Serikali ya Tanzania inashirikiana na Benki ya Dunia na kazi hiyo itafanyika.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya shughuli hiyo kuhakikisha kwamba barabara inajengwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunafahamu wakati ule wa mvua barabara nyingi zilizoharibika na madaraja yamekatika. Leo nilitamani kulisemea daraja moja ambalo liko katika Kata ya Mindu, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, maarufu linaitwa Daraja la Mto Lwangula, limekatika, mawasiliano na wananchi hakuna, pale wanapita kwa shida. Tathmini imefanyika, takribani shilingi milioni 400 zinatakiwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja lile.

Je, Serikali ina kauli gani katika kuhakikisha tunapeleka fedha na daraja lile linajengwa ili wananchi waendelee kunufaika na faraja hii ya Serikali yao ya Chama Cha Mapinduzi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli kwamba ziko barabara nyingi na madaraja ambayo yameathirika na kubomoka kutokana na mvua ambazo zimenyesha sana msimu huu, na ndiyo maana kwanza Serikali ilifanya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja hayo likiwepo daraja hili la Wilaya ya Tunduru ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisemea na barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa baada ya mvua kuwa zimepungua kwa kiasi kikubwa kote nchini, Serikali imekwishatoa maelekezo kwa Mameneja wote wa *TARURA* wa Mikoa na Wilaya

kuanza kutangaza zabuni za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja yote yaliyoharibiwa wakati wa mvua na shughuli hii inaendelea. Tunategemea mwishoni mwa mwezi huu wa Juni tutakuwa tumemaliza kupata wazabuni au wakandarasi na tutaendelea na hatua nyingine.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kwenye daraja hilo muhimu ambalo limeharibika katika Wilaya ya Tunduru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kalambo linapakana na Jimbo la Kwela, katika Kata ya Mkali Kijiji cha Myunga na Kata ya Kaengesa katika Kijiji cha Rula ni kilometa 22. Tathmini imefanyika kwa ajili ya kuunganisha hizi kata mbili na majimbo haya mawili; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inajenga barabara kilometa 22 kwa kiwango cha changarawe?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kipaumbele cha Serikali ni kuunganisha kata na kata, jimbo na jimbo, wilaya na wilaya. Ni kweli barabara hiyo ambayo ameisema Mheshimiwa Kanoni ni barabara inayounganisha Jimbo la Kalambo na Jimbo la Kwela kule kwa Mheshimiwa Deus Sangu, Waziri wa Masuala ya Mahusiano. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwenye bajeti ambazo tunaendelea tunapeleka fedha kwa ajili ya matengenezo ili kuwezesha barabara hii iweze kupitika vizuri hizo kilometa 22.

MWENYEKITI: Nimekuona, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange kwa kujibu vizuri maswali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale Mtwango eneo la Welela, kuna daraja moja limekatika kwenda Mawande. Pia liko daraja ambalo linaunganisha Welela na jimbo lake la Wanging'ombe, linaitwa Daraja la Sakalenga, limekatika, tumejenga kwa miti.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja haya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, Mbunge mahiri na mchapakazi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshatoa maelekezo. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kumsisitiza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Njombe, Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Njombe na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Wanging'ombe, washirikiane kufanya tathmini kwenye eneo la daraja hilo la Welela ambalo linaunganisha maeneo muhimu ya Jimbo la Lupembe na Jimbo la Wanging'ombe na maeneo mengine ili katika 60% inayotangazwa tuhakikishe kwamba barabara hizo zinapelekewa fedha na tuanze kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo la Bumbuli kuna Kata ya Baga na Kata ya Makanya kupitia kwa Bogo, Kata ya Milingano na Mkomole na Dule *'B'*, wakati wa mvua zinakuwa haziwasiliani kabisa.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga madaraja au vivuko katika kata hizi ili ziweze kuwasiliana muda wote?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Bumbuli. Nimhakikishie tu kwamba moja ya hatua ambazo Serikali imechukua kwanza ni kuboresha aina ya barabara tulizozijenga na madaraja ili yasiathirike sana wakati wa mvua na kurudia kujenga kila mwaka maeneo hayo, utaratibu huo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kutokana na mvua barabara zetu zinazounganisha kata kadhaa alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ziko kwenye mpango wetu wa 60% ya bajeti zetu kwa ajili ya matengenezo ili kuziwezesha kuweza kupitika vizuri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 460

Kero ya Mafuriko Kata za Lukobe na Kihonda

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza: -

Je, lini tatizo la mafuriko Kata za Lukobe na Kihonda litamalizika ambapo wananchi wamekuwa wakiathirika na baadhi ya nyumba kubomoka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Kihonda na Lukobe katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro zimekuwa zikiathiriwa na mafuriko ya mara kwa mara nyakati za mvua. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali imepanga kujenga mfereji ili kuyaelekeza maji katika Mto Ngerengere. Serikali imeunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini na kuandaa andiko la mradi ambalo litaonesha mahitaji halisi na njia nzuri ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya tathmini inatarajia kukamilisha kazi hiyo kabla au ifikapo Septemba, 2026.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abood.

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya ya Serikali, leo ni mwaka wa nne Kata za Lukobe na Kihonda wanaathirika kila mvua zinaponyesha. Wanapoona wingu watu wapanda daladala kurudi mjini kukimbia mafuriko. Tunataka jibu ambalo Serikali itamaliza kero hii ya Kata ya Lukobe na Kihonda. Je, Serikali itamaliza lini kero hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika hii miaka minne ya mafuriko wananchi wameathirika, nyumba zao zimebomoka na hasa kwa wanawake ambao walikuwa wajasiriamali ndiyo wamejenga nyumba zao na wastaafu. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuweza kuwafidia?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini kwa namna ambavyo anawawakilisha kwa umahiri mkubwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba eneo hili la Kata ya Lukobe na Kihonda limekuwa likiathirika mara kwa mara na mafuriko hususani wakati wa mvua na ndiyo maana Serikali katika kipindi hiki imeamua kuzitumia taasisi mbalimbali kufanya tathmini. Liko Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, wapo Bodi ya Maji Bonde la Wami-Ruvu, *TMA*, *SGR*, *TARURA*, Kamishna wa Ardhi wa Mkoa wa Morogoro na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua kushirikisha taasisi mbalimbali ili kupata suluhisho la pamoja na la kudumu kujua chanzo cha tatizo na njia sahihi ya kutatua changamoto hiyo ya mafuriko katika Kata za Lukobe na Kihonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Mjini na wananchi wa kata hizi kwamba Serikali ipo hatua za mwisho za tathmini na usanifu ili kuja na njia, mwarobaini wa kuondoa changamoto ya mafuriko katika kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia, Serikali imeweka utaratibu, yako majanga ambayo yanakidhi vigezo vya kuitwa majanga na yako madhara ambayo huwa yanajitokeza kutokana na mazingira tofauti tofauti. Ili tuweze kufikia hatua hiyo ni lazima tujiridhishe kwamba vigezo vya majanga vimefikiwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali ya Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Morogoro wanaendelea kufanya tathmini, ikiwa madhara yale yatakidhi vigezo vya kuwa majanga, watawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa kwa ajili ya hatua stahiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Nimwite sasa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Na. 461

Mafunzo na Mikopo kwa Vijana

MHE. SYLVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuwafikia vijana wenye ujuzi na kuwapatia mafunzo ya ziada na mikopo?

MWENYEKITI: Waziri, Mheshimiwa Joel Nanauka majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuwafikia vijana wenye ujuzi ili kuwaongezea uwezo wa kitaalamu, kuwajengea mazingira ya kujiajiri na kuwawezesha kupata mikopo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na maendeleo ya kiuchumi. Kupitia programu za uwezeshaji wa vijana zinazotekelezwa na Wizara za Kisekta, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano pamoja na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali, ubunifu, matumizi ya teknolojia na stadi za kazi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Aidha, vijana wanaendelea kunufaika na mikopo yenye masharti nafuu kupitia programu na mifuko ya uwezeshaji wa vijana ikiwemo 10% ya mapato ya halmashauri zinazotengwa kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi pamoja na sekta binafsi ili kuwafikia vijana wengi zaidi wenye ujuzi nchini kupitia utambuzi wa vikundi vya vijana, usajili wa miradi yao na utoaji wa elimu ya fedha na usimamizi wa biashara. Kupitia hayo yote Serikali inalenga kuongeza uwezo wa vijana kujitegemea kiuchumi, kuongeza ajira na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sylvia Sigula, kwa niaba ya Mheshimiwa Juwakali.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia nimpongeze, tangu ameteuliwa kwa kweli amekuwa faraja na tabasamu kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza; kwa kuwa kwenye mikopo hii ya 10% ya halmashauri zipo halmashauri ambazo zinafanya vizuri na zipo halmashauri ambazo hazifanyi vizuri kutokana na makusanyo yao kuwa madogo. Wizara ya Mheshimiwa Waziri inahusika na vijana na baadhi ya maeneo hayo vijana wamekuwa hawapati fedha kwa sababu makusanyo ni madogo.

Je, Serikali kupitia Wizara yake ikishirikiana na TAMISEMI imejipangaje kwa halmashauri zile ambazo makusanyo ni madogo kuzitengea fedha ya ziada ili vijana waweze kupata mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tumemwona Mheshimiwa Waziri maeneo mengi akienda kuzungumza na vijana. Vijana wa Rukwa wanaujuzi, ni wachapakazi, na wanatamani sana wamuone. Je, ni lini atafika Mkoa wa Rukwa kuzungumza na vijana wa Mkoa wa Rukwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Sylvia Sigula kwa niaba ya Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia masuala yanayowahusu vijana. Nipokee pongezi zao kwa niaba ya Mheshimiwa Rais ambaye ndiye ametuagiza na kututuma kufanya kazi hii kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huwa ina utaratibu wa kufanya tathmini katika maeneo ambayo ameyataja kuwa na changamoto ya kupata fedha sasa katika halmashauri ambazo zinahusika. Kupitia tathmini hiyo inatuongoza kuona namna ambavyo tunaweza kuweka juhudi za ziada katika maeneo ambayo yana uchache wa fedha kulinganisha na idadi ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kupitia tathmini hiyo ndiyo inatuongoza pia kutoa vipaumbele kupitia uwezeshaji mbalimbali ukiwemo uwezeshaji unaotokana na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, ameulizia kuhusiana na mimi kwenda Rukwa, si mara ya kwanza, najua ameuliza swali hili. Ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Sigula kwamba Rukwa pia kuna vikundi vilivyonufaika katika awamu ya kwanza ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; mojawapo ni katika Wilaya ya Kalambo. Baada ya Bunge hili kukamilika, ratiba itaanza kupitia maeneo mbalimbali na nitafika Rukwa, nitafika pia kukutana na vijana wa Rukwa.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Lucy Kombani.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati upi wa kuhakikisha vijana wa vijijini, hususani wa Mkoa wa Morogoro wanapata fursa hizi za ujuzi, mafunzo na hata mikopo kwa usawa, licha ya kuwa na changamoto ya miundombinu pamoja na ukubwa wa mkoa kijiografia?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Kombani. Nipende kumhakikishia kwamba katika utaratibu wa kiserikali tunaweka vipaumbele katika maeneo pia ambayo hayafikiki kirahisi. Wiki iliyopita tu nilikuwa Mkoani Morogoro, na tulishirikiana na vijana kutoka katika wilaya mbalimbali kuhakikisha kwamba wanapata taarifa hizi. Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba vijana wa maeneo mbalimbali ambayo yako pembezoni mwa mji wanafikiwa na programu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wamehamasika na hamasa iliyofanywa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na hasa kwa kutoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwakopesha vijana, wakiwepo vijana wa Jimbo la Bunda Mjini. Wamefuzu vigezo na yeye anajua wamekwishakwenda katika ofisi yake, amekutana nao. Je, ni lini watapata mikopo ili waweze kujiinua kiuchumi?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuendelea kufuatilia vijana wa Jimbo lake la Bunda. Kama anavyosema, ni kweli kwamba tumekwishaonana nao. Kwa sasa utaratibu uliopo ni kufanyiwa tathmini kupitia taasisi ya kifedha ambayo ni CRDB tulioingia nao makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba vijana wa Bunda ni kati ya vijana ambao wamepata katika awamu ya kwanza, na tutakwenda jimboni pia ili kuhakikisha kwamba tumetimiza ahadi hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge bado tunaendelea na swali lingine la Wizara hiyohiyo. Nimwite Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 462

Fursa ya Mkopo wa Shilingi Bilioni 200 kwa Wanawake

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza: -

Je, lini wanawake wajasiriamali wa Mkoa wa Arusha watafikiwa na fursa ya mkopo wa shilingi bilioni 200 uliotolewa na Mheshimiwa Rais?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango mkubwa wa wanawake katika kukuza uchumi na maendeleo ya Taifa. Kupitia shilingi bilioni 200 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya mikopo yenye masharti nafuu kwa makundi mbalimbali, wanawake wakiwemo wa Mkoa wa Arusha wamepewa wigo mpana wa kunufaika na fursa hiyo. Mbali na fedha zinazotengwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, wanawake pia wanaendelea kunufaika kupitia mifuko na programu za Wizara nyingine za kisekta, pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, wanawake vijana 147 wa Mkoa wa Arusha wanatarajiwa kunufaika na mikopo hiyo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana itakayotolewa mwanzoni mwa mwezi Juni, 2026. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wanawake wengi zaidi wanapata fursa hizi kupitia mifumo na taratibu zilizowekwa, kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, maswali ya nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninachukua fursa hii kushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wanawake wengi hawapati taarifa kwa wakati kuhusiana na uwepo wa mikopo hii na utaratibu ambao unapaswa kufuatwa. Je, Serikali inaweka utaratibu gani sasa wa uwazi ili wanawake wengi zaidi waweze kunufaika na mikopo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; changamoto kubwa ya wanawake wajasiriamali ni ukosefu wa elimu ya ujasiriamali husika. Sasa ili kuacha alama kutokana na mkopo huo ambao umetolewa na Mheshimiwa Rais kwa wanawake wa nchi hii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka utaratibu wa kuwapa mafunzo ya mara kwa mara ili kuhakikisha biashara zao zinakuwa endelevu na zina tija kwa wanawake husika na Taifa kwa ujumla?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kwanza nimpongeze kwa kuendelea

kuwasemea wanawake wa Arusha na Tanzania nzima. Kuhusiana na taarifa, tumeweka utaratibu mzuri wa kushirikiana kwanza na Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wanapatikana kila eneo katika nchi yetu na katika kila halmashauri tunao Maafisa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia Wizara ya Maendeleo ya Vijana, tunao Maafisa Maendeleo ya Vijana ambao pia wanapatikana katika halmashauri zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tunaendelea kushirikiana na wawakilishi wa wananchi wakiwemo Wabunge na Waheshimiwa Madiwani ambao wanafanya mikutano mara kwa mara kuhakikisha kwamba taarifa hizi zinawafikia wanawake wa Arusha, lakini pia wanawake kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Paresso kwamba katika suala la uwezeshaji, wanawake wanapewa kipaumbele sawasawa na sera yetu ya maendeleo ya vijana, lakini pia vipaumbele vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili ameulizia kuhusiana na mafunzo; ni kweli kumekuwa na changamoto ya muda mrefu na takwimu zimeonesha kwamba urejeshaji wa mikopo hii, moja ya changamoto imekuwa ni kukosekana kwa elimu. Serikali mwaka jana Novemba, 2025 ilitoa mwongozo maalumu ambao unahusiana na usimamizi na uratibu wa mikopo inatolewa katika halmashauri zetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huu kipengele 5.11 unaelezea umuhimu na uhitaji wa kufanya mafunzo kwa vikundi ambavyo bado havijapewa mkopo, lakini pia wakati wa mkopo na katika namna ya kuwafuatilia pia. Sisi kama Wizara tumeingia makubaliano maalumu na sekta binafsi ikiwemo taasisi za kifedha na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha kwamba tunatoa mafunzo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hatujatoa mikopo hii, sasa hivi kinachoendelea ni mafunzo yanayoendelea kwa ajili ya kuwapatia

mikopo hii. Juzi tu, mkoani Kigoma tumekuwa na mafunzo haya kwa ajili ya kuwandaa watakaopata mikopo. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kufanya hivyo kama sehemu ya kuimarisha wanufaika kwa mikopo hii. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Edward Olelekaita

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri, hujapita Kiteto kuzungumza na vijana. Swali langu ni hivi, hizi pesa za Mheshimiwa Rais, nia yake ziguse kila mahali. Sasa na sisi tunaotoka vijijini kama Kiteto, ni nini kipya kutoka Wizara yenu kinachoonesha kwamba wale wananchi wa Kiteto waliohamasika wakiwemo vijana na akinamama watapata hizi pesa za Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Olelekaita na ninamuahidi kwamba Kiteto nitafika ipo kwenye ratiba ya kuwafikia vijana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii kama nilivyoeleza awali huwa tunafanya tathmini maeneo ambayo yamepata na maeneo ambayo hayajapata, hasa yale ambayo yako pembezoni. Kwa sababu inatolewa pia kupitia Wizara za Kisekta, tumeweka utaratibu maalumu wa vipaumbele vya kisekta katika maeneo tofauti tofauti kama vile ufugaji, uvuvi na biashara za kawaida kwa kulingana na eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema hii ni awamu ya kwanza, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu zinazofuata pia zitagusa katika eneo lako kulingana na sekta za kipaumbele ambapo ninafahamu kule kwako suala la mifugo ni suala la msingi pia na tutalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Daktari Wilson Charles Mahera.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Butiama ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Vijana, ni mkakati gani uliopo kuhakikisha kwamba akinamama na vijana wa Wilaya ya Butiama kwa Baba wa Taifa nao wananufaika na huu mkopo wa shilingi bilioni 200?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Dkt. Mahera, Mbunge wa Butiama na ninamhakikishia tu kama ambavyo nimetoa hakikisho hili kwa Wabunge wengine kwamba tumeanza awamu ya kwanza na kila jimbo la kila Mbunge aliyepo katika Bunge hili atafikiwa kwa awamu yake itakapofika. Kwa hiyo, asiwe na shaka yoyote, aendelee kuandaa vijana, awaambie wakae mkao wa kula, kwa sababu uwezeshaji huu utamfikia kila kijana wa nchi hii ya Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Madini, ninamwita sasa Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, aulize swali lake.

Na. 463

Uchimbaji wa Madini Sesenga na Duthumi

MHE. ZUBERI Y. MFAUME aliuliza: -

Je, lini uchimbaji wa madini katika maeneo ya Sesenga na Duthumi utaanza baada ya leseni za uchimbaji kutolewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Madini, Mheshimiwa Salome Makamba, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Madini, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu maendeleo ya miradi ya madini nchini ili kuhakikisha leseni zinazotolewa zinatafsiriwa kwa uwekezaji halisi na ajira kwa wananchi, mapato kwa Serikali na maendeleo ya maeneo husika. Katika muktadha huo, maeneo ya Sesenga na Duthumi nayo yanaendelea kufuatiliwa kwa karibu ili yaanze kunufaisha wananchi wa Morogoro na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Sesenga lina leseni moja ya utafiti wa madini adimu *(Rare Earth Elements)* Namba. PL 13451/2025, iliyotolewa tarehe 22 Julai, 2025 kwa Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*. Hadi sasa shughuli za utafiti bado hazijaanza rasmi kwa kuwa *STAMICO* ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha majadiliano na mwekezaji kuhusu makubaliano ya pamoja ya kuendeleza mradi huo. Mara baada ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, shughuli za utafiti zitaanza. Serikali imeelekeza hatua hizi zikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Duthumi lina leseni ya uchimbaji wa kati ya madini ya Kinywe *(Graphite)* Namba. ML 644/2021, iliyotolewa tarehe 8 Februari, 2021 kwa Kampuni ya *Yudi Mining* (Tanzania) *Graphite Development Company Limited*. Kwa sasa kampuni ipo katika hatua za ujenzi wa mgodi na maandalizi ya uzalishaji ambapo usimikaji wa mitambo ya uchenjuaji umefikia takribani 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hiyo imefanikiwa kukamilisha taratibu za mkopo wa nje baada ya idhini kutolewa na Serikali, na fedha hizo zinatarajiwa kupatikana mapema mwezi Juni, 2026. Fedha hizo zitakapopatikana, kazi ya ukamilishaji wa ujenzi wa mgodi na mitambo itaendelea mara moja na uzalishaji unatarajiwa kuanza baada ya hatua hizo kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa upande wa Mgodi wa Duthumi, wananchi wamekuwa na wasiwasi mkubwa kutokana na shughuli zinazoendelea pale hasa kipindi cha usiku, shughuli za uchimbaji zinaonekana zikiendelea, lakini pia malori yakiingia na kutoka. Wasiwasi wao ni kwamba uchimbaji umeanza na madini yanatoroshwa na tabia yao ya kutotaka wananchi wanaozunguka mgodi ule kupata kazi hata zile ambazo hazihitaji ujuzi maalum.

Je, Serikali sasa ipo tayari kwenda kufanya utafiti na kubaini ni nini kinachoendelea katika mgodi ule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna hali ya uchafuzi mkubwa wa mazingira katika eneo lile la uchimbaji wa madini (utiririshaji wa maji na utupaji hovyo wa taka). Je, Serikali ipo tayari sasa kwenda na kuangalia na namna gani uhifadhi wa mazingira unafanyika katika eneo la mgodi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mfaume kwa kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha kwamba madini yanayopatikana katika Jimbo lake la Morogoro Kusini yanawanufaisha Wana-Morogoro Kusini. Kuhusu swali la kwanza, taarifa ambazo Serikali inazo, kama nilivyojibu katika swali la msingi, ni kwamba wako katika hatua ya ujenzi wa miundombinu na baada ya hapo wataanza uzalishaji mwezi Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, ndiye anatoka mahali husika na anayelala na mgonjwa ndiyo anajua mapigo yake. Ninaomba nitumie fursa hii kuwaelekeza wataalamu wetu wa Wizara ya Madini, kwenda kufanya uchunguzi na kujua nini kinaendelea

katika eneo hili, kwa sababu ni haki ya Wana-Morogoro Kusini kuhakikisha kwamba wananufaika na kupata ajira kwenye kazi ambazo Serikali imeelekeza zitafanywa na wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kwenye eneo la Duthumi, kabla mgodi huu haujaanza, kulifanyika tathmini ya athari ya mazingira pale na andiko la usimamizi wa mazingira na jamii yaani *Environmental and Social Management Plan* liliandikwa na kuhakikisha kwamba hakutatokea athari za mazingira. Ninakuahidi Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kupitia *NEMC,* tutakuja kufanya tathmini na kuhakikisha wananchi wa Morogoro Kusini hawaathiriki na uchimbaji wa madini unaoendelea katika eneo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, nimekuona, lakini ninadhani unatambua kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati anamwakilisha Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini. Sasa maswali yako ya Nyamongo yale, yanataka Waziri au Naibu Waziri. Unataka uendelee bado?

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamlegezea kidogo, lakini naomba uniruhusu niulize swali dogo, ni muhimu.

MWENYEKITI: Haya endelea Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kumekuwa na mtindo wa leseni zinatolewa Dar es Salaam kwenye mtandao, halafu wanaenda kuchimba kule Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hapa sasa hivi kuna mgogoro Kata ya Kiore na Kata ya Komaswa, kuna watu wawili wameshapoteza maisha. Kwa sababu kwenye leseni, wale wananchi wa kawaida hawajui, wameanza kuchimba akaibuka mtu mwenye leseni. Sasa kauli ya Serikali kwa sasa, kuhakikisha kwamba wanaenda, huyu mwenye leseni ambaye hajulikani kule, wakae na wananchi

wazungumze na waoneshe watu watanufaikaje na machimbo yale ili amani irejee katika eneo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la jumla hilo, unalimudu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waitara, kwa kweli amekuwa ni mfuatiliaji mzuri wa sekta ya madini na tunafahamu kwamba katika maeneo ya Tarime kule Nyamongo, kuna uchimbaji mkubwa na kuna *reserve* kubwa sana ya madini hasa ya dhahabu. Mheshimiwa Waitara, unafahamu utaratibu wa upatikanaji wa leseni, ni lazima uwe jumuishi na ushirikishe wananchi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hata leseni inapokuwa imetoka ni kazi ya maafisa madini wa eneo husika kwenda kuonesha *demarcation* za maeneo ambayo mwekezaji amepewa leseni. Kwa sababu hiyo, kama kuna mgogoro, sisi kazi yetu Serikali ni kuhakikisha kwamba watu wanafanya kazi katika mazingira salama na yenye amani. Niwaelekeze Maafisa Madini wa Tarime, waende pale kuweza kuonesha *demarcation* ya maeneo kwa ajili ya mwekezaji na eneo kwa ajili ya wananchi ili kuweza kuondoa migogoro na kuleta tabasamu la utu kwa Watanzania kama ambavyo Mheshimiwa Rais anataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Kilimo, nimwite Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 464

Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mazao ya Kilimo Wilaya ya Mlele

MHE. MARTHA F. MARIKI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga soko la kimataifa la mazao ya kilimo katika eneo la Majimoto, Wilaya ya Mlele, Mkoa wa Katavi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Silinde kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa masoko ya kimkakati ya mazao ya kilimo katika halmashauri mbalimbali nchini kwa lengo la kuendelea kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kufanya tathmini ya ujenzi kwa maeneo yenye kipaumbele kulingana na vigezo vya uzalishaji wa mazao, wingi wa biashara ya mipakani, pamoja na upatikanaji wa rasilimali na mahitaji ya miundombinu ikiwemo eneo la Majimoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara ya Kilimo itafanya tathmini ya ujenzi wa soko hilo na utekelezaji wake utafanyiwa kazi kwa kuzingatia tathmini hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanatoa matumaini kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi, hususan kwa wananchi wa eneo la Majimoto.

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Katavi ni wakulima wazuri sana wa mazao ya mpunga, mahindi, ufuta pamoja na tumbaku, upi mkakati wa Serikali sasa wa kuwatafutia masoko ya uhakika ili

wananchi waweze kujipatia kipato, kwa kuwa wamekuwa wakilima vizuri, lakini kuna wakati soko la uhakika limekuwa likisumbua? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Mheshimiwa Martha Festo Mariki, ameuliza swali jema na la msingi na nimpe tu taarifa kwamba moja; soko la kwanza la mazao kama mahindi na mpunga hapa nchini ni kupitia Wakala wetu wa Taifa *(NFRA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili *NFRA* kama sasa hivi tumefungua masoko nje ya nchi, tumefungua Kenya, Malawi na Congo, tunakwenda mpaka Misri sasa hivi na Zambia. Maeneo ambayo sasa tuna uhakika wa kuuza mazao yetu muda wote na imekuwa *guaranteed* hivyo. Kwa hiyo tu, nimthibitishie hilo ni soko namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la pili tumeshaelekeza balozi zote nchini kuhakikisha kwamba wanafungua masoko katika hayo maeneo ili wananchi waweze kufikisha hayo mazao. Kwa hiyo, watu wa Katavi lakini na maeneo mengine hapa nchini watakuwa na uhakika wa kuuza masoko yao bila kuwazuia kwa kufuata sheria na taratibu ambazo tumeweka hapa nchini, ahsante.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Thomas Maganga.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, unajua fika Jimbo la Katavi ni moja ya Jimbo ambalo linafanya vizuri kwenye kilimo cha mazao mchanganyiko. Pamoja na kufanya vizuri kwenye upande wa mazao, Jimbo la Katavi halina soko hata moja la mazao. Je, nini mkakati wa Serikali kujenga soko kwenye Jimbo la Katavi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninamthibitishia tu kaka yangu, Mheshimiwa Thomas Maganga Kampala, Mbunge wa Katavi, kama nilivyojibu katika swali la msingi kuwa yale maeneo ambayo tunakwenda kufanyia tathmini kulingana na vipaumbele ikiwemo uzalishaji mkubwa, ni pamoja na Jimbo la Katavi, lipo katika huo mpango. Tukishafanya maana yake hatua inayofuata ni ujenzi.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Josephine Kapoma.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakazi wa Morogoro Vijijini wanaendelea kuishukuru Serikali kwa kuendelea kuliongezea thamani zao la karafuu. Hivi karibuni tumefanikiwa kufungua maghala matatu; Kinole, Tawa na Kisemu. Kwa msimu wa mwaka jana tu, tumepata zaidi ya shilingi bilioni ya 41.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunakuwa na Stakabadhi Ghalani ili tupate kuongeza thamani ya hili zao la karafuu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Josephine Kapoma, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro kwa swali lake la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nipongeze Mkoa wa Morogoro kwa jitihada kubwa wanayoifanya sasa hivi ya kuzalisha karafuu kwa wingi na kutaka kuwa miongoni mwa maeneo ama mikoa itakayoongoza kwa uzalishaji hapa nchini. Ninafahamu na kwenye huo mkakati mimi mwenyewe nilikuwepo. Mkakati wa Serikali ni kwamba; cha kwanza tuongeze uzalishaji na baada ya hapo sasa tutafute masoko ya uhakika ikiwemo kuingiza hili zao katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, lakini baada ya kuongeza uzalishaji kwa wingi.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali fupi la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali ilitenga maeneo ya kujenga soko la kimataifa eneo lile la Karema, Kijiji cha Itetemya na mpaka sasa yapata miaka mitano eneo hilo halijaendelezwa. Ni lini mtaenda kujenga soko la kimataifa katika eneo hilo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimthibitishie tu kaka yangu Mheshimiwa Kakoso kwamba mpango wa Serikali kujenga Soko la Karema uko palepale. Tulikuwa na changamoto ya fedha na fedha inatafutwa ili tuanze huo ujenzi.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Rebeca Nsemwa.

MHE. REBECA S. NSEMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wananchi wa Wilaya ya Makete ni wazalishaji wakubwa wa zao la ngano. Licha ya zao hilo kutumika kutengeneza vitafunwa mbalimbali kama mikate, maandazi na chapati, lakini zao hili katika Wilaya ya Makete hutumika pia kupikia ugali ambao ni chakula kikuu kwa wananchi wengi wa Tanzania.

Je, ni lini Serikali itaweza kuwatafutia masoko wananchi hawa ili zao hili liuzwe kwa bei ambayo itaweza kuwanufaisha wakulima? Pia ni lini Serikali…

MWENYEKITI: Swali moja tu. Kwenye nyongeza swali ni moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri, masoko ya ngano.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimthibitishie tu dada yangu Mheshimiwa Rebeca Nsemwa kwamba soko la ngano nchini, ndiyo ninaweza nikasema ni soko la uhakika kwa sababu ngano tunaagiza, ninaweza nikasema karibu 100% kutoka nje ya nchi. Pia tunatumia fedha nyingi sana kwa mwaka, zaidi ya shilingi bilioni 400 kuagiza ngano kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni soko la uhakika na moja ya mkakati wa Wizara (Serikali), ni kuhakikisha zao la ngano

ndiyo linapewa kipaumbele. Katika hizo jitihada tunazofanya ni pamoja na Halmashauri ya Makete, Mbunge wa Jimbo hapa anafahamu, kila mwaka tumekuwa tukipeleka mbegu za ruzuku bure ili kuli-*boost* hilo zao. Tunaamini tukishaongeza uzalishaji kwa kiwango kikubwa, maana yake itatusaidia kupunguza ile tunasema *gap* ya uagizaji wa ngano kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, soko letu hapa nchini ni la uhakika na tutaingia katika kilimo cha mkataba ili kuhakikisha wale wananchi wanapokuwa wanalima, wanauza moja kwa moja kwa wadau, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Enock Koola, swali la nyongeza.

MHE. ENOCK Z. KOOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwenye ziara ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi kuwa soko la kisasa litajengwa Jimbo la Vunjo, Kata ya Makuyuni. Je, lini hiyo kauli au ahadi itatimizwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Koola, Mbunge wa Vunjo, ni kweli kauli hiyo tuliitoa na tuna uhakika hilo soko tutalijenga, tunachokifanya sasa hivi ni kutafuta fedha ili tuanze ujenzi katika eneo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Mwakyembe, swali la nyongeza.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inajenga masoko katika maeneo mbalimbali ya kimataifa, je, Serikali ina mpango gani ili kuweka mkakati katika baadhi ya mikoa kuweza kulima kilimo cha matunda kama kilimo cha biashara ili kuwatafutia soko nje ya nchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge Lucy Mwakyembe, mkakati wa Serikali tuna mazao ya kimkakati ya kibiashara, tuna mazao ya chakula. Hata hivyo, tumejikita sasa hivi vilevile kuhakikisha kwamba tunahamasisha mazao ya matunda katika maeneo mbalimbali na ndiyo maana utaona hata mikoa kama Mwanza maeneo ya Ukerewe tunahimiza watu kuongeza uzalishaji wa machungwa, ukienda kwenye parachichi utaona watu Mikoa ya Njombe inalimwa sana, yote tu ni katika kuhamasisha kwamba uzalishaji wa mazao ya matunda utumike kama sehemu ya mazao ya kibiashara ambayo yatasaidia kuongeza kipato cha mkulima. Kwa hiyo, ipo na ni makakati wa Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge, kuna swali lingine linaendelea nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, swali hili kwa niaba litaulizwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

Na. 465

Kuendeleza Kilimo cha Machungwa kama Mbadala wa Kiuchumi Wilaya ya Ukerewe

MHE. MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MHE. DKT. REGINA C. MALIMA aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza kilimo cha machungwa kama mbadala wa kiuchumi Kisiwa cha Ukerewe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri inalo eneo linalofaa kwa kilimo lenye ukubwa wa hekta 39,121.6 ambapo malengo ya kilimo cha machungwa msimu wa mwaka 2025/2026 ni hekta 1,731.7 eneo lililolimwa mpaka sasa ni hekta 1,312 sawa na 76% ya lengo, eneo

linalovunwa ni hekta 1,123 ambapo mavuno yaliyopatikana hadi sasa ni tani 37,075.5 za machungwa na uvunaji unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kupitia Halmashauri ya Ukerewe inatenga bajeti ya shilingi 30,000,000 kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa miche ya matunda na kuimarisha vitalu vya kuhifadhia miche. Katika msimu wa mwaka 2025/2026 halmashauri hiyo imenunua jumla ya miche 2,000 kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* kwa kutumia fedha za mapato ya ndani. Miche hiyo ilisambazwa kwa baadhi ya wakulima na taasisi 14 kwa ajili ya kupandwa. Aidha, Serikali itaongeza wataalamu watakaotoa elimu bora juu ya kilimo cha machungwa, kutafuta masoko na kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kuwa zao hili la machungwa Wilayani Ukerewe kwa sasa linalimwa kwa wingi, Serikali inaonaje kutafuta wawekezaji watakaowekeza kwenye kiwanda cha kuchakata zao hili ili kupata zao litakalokuwa na thamani zaidi? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa pia mazao haya mbadala yapo na yameenea maeneo yetu mbalimbali nchini na Jimbo langu la Maswa Magharibi tuna zao mbadala la alizeti; Serikali ina mkakati gani kutusaidia kupunguza bei ya mbegu za alizeti, lakini pia kutafuta soko la mafuta ya alizeti kutoka Wilayani kwetu Maswa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninamshukuru Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kwa maswali mawili ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu eneo la Ukerewe ambapo ameomba jitihada za Serikali kuhakikisha tunapeleka wawekezaji na sasa hivi moja ya mchakato tulionao Wizara ni

kuongea na wale wawekezaji wanaozalisha vinjwaji vinavyotokana na matunda hapa nchini huenda kama vile wale kina Jambo, watu wakina Bakhresa ambao ni Azam, kina Azania, wakina MO wote wale tumekubaliana kwamba tukae nao na tutengeneze mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kwamba wananunua matunda hapa nchini na kusaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu bei ya mbegu za alizeti, alizeti ni moja ya zao ambalo Serikali tunatoa ruzuku kwenye mbegu za zao la alizeti, kwa hiyo, ipo na tunachokifanya tu ni kuongeza idadi ya mbegu ambazo zitawafikia wakulima. Kwa hiyo, hilo nikuthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeweka ruzuku katika alizeti na Maswa Magharibi ni sehemu ya wanufaika na tutawafikishia mbegu hizo kwa wakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya kuweka soko la kuuzia mazao yanayoharibika haraka kama vile maembe katika Mikoa yetu ya Mtwara na Lindi badala ya wanaokwenda kununua kwenda kule mashambani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge dada yangu Mheshimiwa Agnes Hokororo, mkakati wa Serikali sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunajenga tunasema hizi *cold chain facilities* maeneo ambayo yanaweza kuhifadhi matunda kama maembe na machungwa katika maeneo ya mipakani kwenye *border* zetu ambapo mazao yanapita kutoka eneo moja kwenda lingine, lakini vilevile katika viwanja vya ndege na stesheni zetu ikiwepo *SGR,* huu ndiyo mpango tulionao Serikali ili kuhakikisha kwamba tunapunguza upotevu wa mzao yanayotokana na matunda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, nimwite sasa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 466

Mradi wa Maji wa Tsoray Tarafa ya Nambis - Mbulu Mjini

MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza Mradi wa Maji wa Kimkakati wa Tsoray katika Tarafa ya Nambis - Mbulu Mjini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado inaendelea na utafutaji wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 70.1 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa maji wa kimkakati wa Tsoray uliopo Tarafa ya Nambis, Wilaya ya Mbulu Mkoani Manyara. Miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 13.6 kwa siku, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house),* ununuzi na ufungaji wa pampu nne za kusukuma maji, sanjali na ujenzi wa vituo 160 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 109,228 wa Wilaya ya Mbulu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu unahitaji fedha nyingi ili uweze kutekelezwa, je, kwa nini Serikali isianze kutekeleza mradi huu kwa awamu ili kupunguza adha ya maji kwa wananchi katika maeneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Kata ya Bara Wilayani Karatu kuna mradi wa maji uliokamilika na umejengwa na sekta binafsi ambapo takribani wananchi 15,000 wataenda kufaidika, je, Serikali ina mpango gani wa kuweka miundombinu ya usambazaji hadi kwenye vijiji vya jirani ili kupunguza kero ya maji katika vijiji husika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay yaliyoulizwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kweli kabisa fedha ni nyingi na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa mawazo na ushauri wa namna ambavyo tunaweza kutekeleza mradi huu, na nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge tunapokea kwamba ni dhahiri kwamba inahitajika kuanza hatua kwa hatua ili tuone namna ambayo tunaweza tukafika. Hata hivyo, tutaangalia namna ambavyo tutaanza na chujio wakati tukiwa tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga maeneo mengine ya kimiundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye swali la pili kuhusiana na eneo la Karatu, Mheshimiwa Mbunge unafahamu mradi ule nilienda kuuzindua na kwa ushirikiano mkubwa sana na wadau wa maendeleo na wewe ukiwa sehemu ya kuhakikisha kwamba mradi ule unatoa matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimtoe hofu chini ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakuna kijiji, hakuna mtaa,

hakuna kata itakayobaki nyuma kwenye huduma ya maji safi na salama. Nikuhakikishie kwa kufanya hivyo tayari katika bajeti ya mwaka 2026/2027 tumeshaweka kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kwenda kutengeneza mtandao wa kusambaza maji katika vijiji vya jirani ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, nilikuona.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya ya Makete imekumbwa na miradi chechefu ya maji, Mradi wa Maji Ipelele, Mradi wa Maji Usarimwani, Mradi wa Maji Kidope, Mradi wa Maji Magoe, Igofi, Uganga, Kisinga lakini Matamba. Miradi hii Serikali imelipa fedha, wakandarasi hawaonekani *site* na leo wamekuja viongozi wa chama, wa Serikali, wa chama hapa hapa Bungeni, wa kutoka Makete, Mwenyekiti na Katibu tunahitaji majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali mtaunda timu maalum iende Makete kufuatilia miradi hii ambayo imekwama kwa takribani miaka mitatu haijaendelea na majibu hayapo? Naomba majibu Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hamu ya Mheshimiwa Mbunge na lengo la Serikali ni kupanga, kuanzisha miradi na kuikamilisha ili iweze kutoa matokeo. Hivyo basi kwa namna ambavyo Mheshimiwa Sanga ameliwasilisha, nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kumwelekeza Katibu Mkuu Wizara ya Maji aunde hiyo timu mara moja iweze kufika Makete na kujiridhisha kwa nini mkandarasi alipwe na asiwepo *site* kwa sababu hizi ni fedha za walipa kodi wa Tanzania ambao wanatarajia kuona uwekezaji wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, unatoa matokeo chanya na wao waone ni sehemu ya Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Hai hasa mji wetu wa Bomang'ombe kipindi cha mwezi wa tisa kuelekea mwezi wa 12 kumekuwa na changamoto ya maji sana. Katika kutafuta ufumbuzi *HUWASA* Wilaya ya Hai kwa kushirikiana na bodi za maji zimefanya tathmini na kupata mahitaji ya shilingi bilioni 10 ili kuanzisha mradi mpya na chanzo kipya na kuondoa tatizo hilo. Nataka kufahamu kwa kuwa wameshawasilisha kwenye ngazi ya Wizara, Serikali ina mpango gani sasa mradi huu uweze kukamilika na tatizo la maji wilaya liweze kwisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, Mbunge wa Hai na ninampongeze sana kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Wana-Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano unaoendelea kutupatia kwa sababu hata hii *CBWSO* chanzo cha kuanza kuandika andiko tunatambua ulikuwa ni ushauri wako kwa kutumia *window* ya *National Water Fund* ambapo *National Water Fund* inatoa mikopo kwa taasisi zetu ili kuweza kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimhakikishie kwamba andiko hilo limeshawasilishwa liko katika hatua nzuri kabisa za mchakato ili liweze kupelekwa Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa ajili ya idhini ili kuona kama andiko hilo ni *viable* katika uwekezaji wa huduma ya maji safi na salama. Lakini nikutoe hofu kipaombele cha Serikali ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kabla hatujaendelea nakuomba ukae tu kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea swali linalofuata la maji nimeona ni busara tuwatangaze wageni.

Tunao wageni wengi sana wanaongojea kuingia na leo ni siku ya Ijumaa. Kwa hiyo tungependa tu waingie wengi kadri itakavyowezekana na tuwatangaze wachache angalau waweze kutoa nafasi kwa wengine. Nitaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Riziki Silas Shemdoe - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hawa ni kama wafuatao:-

Tunaye Mheshimiwa Zefania Sumaye - Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, tunaye Mheshimiwa Whitney Mwizagi - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Lushoto, Mheshimiwa Christine Kika - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, na Ndugu Ali Dafa - Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Lushoto. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine Waheshimiwa Wabunge; wageni 81 wa Mheshimiwa Profesa Shemdoe, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Ramadhan Singano na Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa umoja wao ambao ni Waheshimiwa Madiwani, viongozi na wananchi kutoka Wilaya ya Lushoto, Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, hawa ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 69 wa Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, hawa ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Frey Luis Amigo ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, hawa ni familia yake kutoka Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, hawa ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo; Ndugu Justin Jafa kutoka Msalato Dodoma, kuna wananchi watatu kutoka Bunda Mkoani Mara, na wanafunzi 65 na walimu nane wa Shule ya Msingi Shree Hindu Mandal kutoka Dar es Salaam, karibuni sana wote kwa ujumla wenu. *(Makofi)*

Hata hivyo, tunao wanafunzi 42 na walimu saba wa Shule ya Msingi Uhuru kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Nimuite sasa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, aulize swali lake.

Na. 467

Mradi wa Maji Kata ya Maruku na Kanyengereko

MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza: -

Je, lini huduma ya maji itafika kwenye Kata za Maruku na Kanyengereko?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza na ya pili ya mradi mkubwa wa maji wa Kemondo - Maruku kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria ambapo zaidi ya kaya 1,000 na wananchi 36,150 wa Vijiji vya Rwagati, Kanazi, Katoju, Buganguzi na Minazi vilivyopo Wilaya ya Bukoba, Mkoani Kagera vimeanza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya tatu ya mradi huo itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo itahusisha ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 500,000, ujenzi wa nyumba ya mitambo ya kusukuma maji *(booster station),* ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 90.8, ujenzi wa vituo 119 vya kuchotea maji pamoja na maunganisho ya maji kwa kaya 550 zilizopo Vijiji vya Kata za Maruku, Kanyengereko na baadhi ya maeneo ya Kata ya Katerero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha zaidi huduma ya maji kwenye vijiji hivyo, Serikali inaendelea na mradi wa ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji pamoja na chanzo cha Kiholelo katika Vijiji vya Maruku na Kanyengereko kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 492. Mradi huo umefikia wastani wa 75% za utekelezaji ambapo unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza.

Washa kishikwambi. Sogea kiti cha pili hapo.

Waheshimiwa wengi hapa ninawaona mmewasha mkingojea maswali ya nyongeza, nimeshawaona watakaouliza.

MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya kutia moyo kwa wananchi wa Vijiji vya Maruku na Kanyangereko. Ni kweli nimeona kwenye bajeti ya juzi hapa ya Wizara ya Maji, mradi huu umetengewa fedha kwa ajili ya kutekelezwa. Ninaishukuru Serikali kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza; Mheshimiwa Naibu Waziri mradi huu ni muhimu sana Kanyangereko na Maruku. Je, unaweza kunihakikishia kwamba mradi utapewa kipaumbele cha kwanza kwa sababu umekaa miaka sita karibu saba tangu uanze kutekelezwa na haujakamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Rweikiza kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Jimbo lake la Bukoba Vijijini. Ninatambua wakati akiingia madarakani upatikanaji wa huduma ya maji ulikuwa hafifu na sasa umefikia 75%. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na mimi nimepata fursa ya kutembelea jimbo lile kwa mara tatu. Ninaamini kwamba kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaanza kuonekana kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimtoe hofu na kwamba Serikali inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haitapima mafanikio ya sekta ya maji kwa idadi ya miradi iliyoanzishwa, bali kwa idadi ya miradi iliyokamilika na kugusa wananchi moja kwa moja. Hivyo, hakuna mradi wa kimkakati utakaobaki kuwa kiporo. Ninataka kutumia fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Dkt. Rweikiza kuwa mradi wake wa Kemondo ni wa kimkakati katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tumehakikisha na tunahakikisha kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itauweka katika kipaumbele cha kwanza kabisa katika kuutekeleza na ndiyo maana tumeuingiza kwenye bajeti ya mwaka huu ili awamu hii ya tatu baada ya awamu ya kwanza na ya pili kukamilika na hii ya tatu tunaenda kuikamilisha kama ilivyo maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kumekuwa na shida kubwa sana ya maji katika Kata ya Ramadhani, maeneo ya Mgendela na Njombe Mjini; Kata ya Kitisi, Jimbo la Makambako na Kata ya Wanging'ombe, Kijiji cha Katenga na

Mbembe Jimbo la Wanging'ombe. Je, lini Serikali itamaliza shida hii ya maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge Viti Maalum Njombe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana kwa kazi kubwa ya kuwatetea akinamama na kwa ushirikiano mkubwa anaowapatia Waheshimiwa Wabunge ukiwemo Mheshimiwa Mwenyekiti. Nimtoe hofu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inao mradi mkubwa sana umewekezwa Njombe, Makambako mpaka Wanging'ombe una gharama ya shilingi bilioni 125.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaamini kwamba mradi huu ukishakamilika basi utaweza kutoa huduma huduma iliyotarajiwa kwa wananchi na iwapo kutakuwa na maeneo ambayo yatabaki na changamoto, tunayo programu maalumu ya vijiji 1,575 napo tutahakikisha kwamba tunaanza kuingiza kijiji kimoja baada ya kingine. Lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 vijiji vyote vitakuwa vimepata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba pamoja na jitihada kubwa na nzuri zinazofanyika ndani ya Jimbo la Segerea kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama, jitihada hizi hazijaleta matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali kwa kuliona hilo ikaagiza pampu nne. Pampu ambazo zikija kufungwa Mto Ruvu, wananchi wa Jimbo la Segerea pamoja na wakazi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam watakwenda kuondokana na adha hii kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu; ninatambua pampu tayari zilikwishakufika. Je, zoezi la kufunga pampu hizi limefikia wapi na ni lini mradi huu utakamilika ili wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam waweze kupata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Segerea, kwanza kwa ufuatiliaji na kwa kujua hatua kwa hatua sekta ya maji inavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhahiri na ni ishara tosha ya kuonesha kwamba Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya mambo yake kwa uwazi na kwa kushirikiana na ndiyo maana tumefikia katika hatua ya kuona Mheshimiwa Mbunge anakuwa anajua *chain* yote ya mchakato. Nikutoe hofu kazi kubwa ilikuwa kununua hizo pampu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyobaki na kwa wataalamu tulionao ndani ya sekta ya maji ninakuhakikishia kwamba hizo pampu tunaenda kuzifunga na wananchi wako wa Jimbo la Segerea wakapate huduma ya maji safi na salama na mradi huo utakuwa umeanza kutoa huduma inayotarajiwa kwa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kijakazi Mohamed.

MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata Lihimalyao, Wilayani Kilwa hususan akinamama wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu. Maji ambayo yamekuwa yakipatikana pale ni maji ya chumvi kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuleta maji kutoka kata jirani kwa kupitia Mradi wa *Pande Plot*. Ningetamani kufahamu ni upi

mpango wa Serikali au Serikali imejiandaaje kutekeleza ahadi ile ili kuweza kuikata kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kila mwanamke tunamtua ndoo kichwani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, Binti Lindi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na sisi sekta ya maji tunamwahidi ushirikiano kuhakikisha kwamba anatimiza falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua na Serikali inafahamu Lihimalyao ni eneo ambalo kweli maji yake hata kama ukitumia gharama yoyote ya kuyatibu matokeo yake maji yatafika kwa watumiaji yakiwa na changamoto ya gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokwenda kukifanya tunakwenda kuchukua maji kutoka *Pande Plot* ambapo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluh Hassan kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tumepata *KfW* ambao wamekubali kushirikiana nasi kwenda kuyatoa katika Kata ya Pande ambapo ya Pande haya ni maji safi na salama, hayana changamoto ya chumvi ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Kata Lihimalyao wanapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Lyamidati iliyoko katika Jimbo la Solwa, maji ya Ziwa Victoria yamepita kwenye miji ya watu, yale

mabomba yamepita kwenye mji wa mtu, lakini wananchi wale hawana maji. Nini kauli ya Serikali kuhusu wananchi hawa ambao wanalinda miundombinu, lakini maji hawana? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba bomba limepita katika makazi ya watu na linapita katika Jimbo la Solwa, lakini pia linapita katika Jimbo la Itwangi ambapo changamoto ni hiyo hiyo, lakini Serikali tumeliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tumeweka bajeti ya kwenda kuanza na baadhi ya vijiji ili tuhakikishe kwamba wanapata huduma ya maji safi sana na salama, lakini katika bajeti zijazo tutaendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba wananchi hao wanaendelea kunufaika na maji ambayo kimsingi wamejitolea maeneo yao na mabomba yamepita hapo. Kwa namna nyingine tunasema kwamba mradi huo wameufanya kuwa wao na sisi Serikali tutahakikisha kwamba tunazingatia hilo ili wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Wizara ya Maji. Nimwite Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana aulize swali lake, lakini swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory.

MHE. SILVERY L. SALVATORY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla swali halijaulizwa, ninaomba masahihisho kidogo yafanyike badala ya Fumagile, mtaa ule au kitongoji kile kisomeke Fumagila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana, swali lake namba 468 lipate majibu ya Serikali.

Na. 468

Ujenzi wa Matenki ya Maji Nyamazobe, Buhongwa na Fumagila

MHE. SILVERY L. SALVATORY K.n.y. MHE. JOHN F. NZILANYINGI aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa matenki ya maji ya Nyamazobe, Buhongwa na Fumagila ili kuongeza upatikanaji wa maji Jiji la Mwanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa chanzo cha maji cha Butimba kupitia maji ya Ziwa Victoria ambacho kina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 48 kwa siku. Aidha, utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji unaendelea kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa zaidi ya wakazi 450,000 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza na maeneo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unahusisha ujenzi wa vituo vitatu vya kusukuma maji katika maeneo ya Butimba na Sahwa, ujenzi wa matenki matano yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 31 katika maeneo ya Buhongwa, Fumagila, Nyamazobe, Kisesa na Usagara sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 40.5. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 53% na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2026 kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati na ubora stahiki. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silvery Salvatory kwa niaba maswali ya nyongeza.

MHE. SILVERY L. SALVATORY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; baada ya ujenzi wa matenki kukamilika Serikali imejipangaje ili kuhakikisha kazi ya usambazaji maji kwenye mitaa itafanyika kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni nini mpango wa Serikali kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo ambayo yamekuwa na changamoto sugu kwenye upatikanaji wa maji kama vile Kata ya Mahina na maeneo mengine ya pembezoni yakiwemo ya Jimbo langu la Misungwi hususan, Usagara, Mwasonge, Mayolwa pamoja na Chole?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa maswali ya nyongeza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa ya John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana yaliyoulizwa na Mheshimiwa Silvery, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni kweli ni mradi mkubwa na wa kimkakati na ni uwekezaji na ni mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wa Jiji la Nyamagana. Hii ni kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana kwa kuendelea kuwa sauti yao katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji unaendelea kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mradi huu unaendelea na tunao mpango unapokamilika kama ambavyo nimesema kwa jibu

la msingi utakamilika Disemba, 2026 baada ya hapo tutaanza kuhakikisha tunasambaza maji katika maeneo ya pembezoni, lakini pia kuna maeneo ya miinuko ambayo jiografia yake ina changamoto tutahakikisha maji yanafika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kuhusiana na maeneo ya Mahina kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameongelea. Upande wa Mahina mradi huu wa kwanza unapokamilika hautakuwa sehemu ya kupeleka maji katika maeneo ya Mahina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahina pamoja na Kishili na Igoma kwa sasa bado wanapata maji kwa mgao. Mheshimiwa Rais ameridhia kupeleka shilingi bilioni nane *specifically* kwa ajili ya maeneo haya ya Mahina, Kishili pamoja na Igoma ili wananchi wa Jiji la Mwanza waweze kuondokana na mgao ambao unapitia kwa sasa. Huu utekelezaji uko katika hatua za mwisho na ninaamini kwamba utakapokamilika zaidi ya wananchi 45,000 watanufaika na mradi huu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Mtwara Vijijini, Kata ya Dihimba inahitaji suluhisho la haraka. Kisima kilichochimbwa cha maji mwaka 1989 kimeharibika na wananchi zaidi ya 4,606 wanapitia changamoto hiyo ya maji. Ipi kauli ya Serikali ili kutatua hiyo changamoto kwa haraka? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Kauli ya Serikali kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Kwanza, kabisa ni mdau wa sekta ya maji. Pili, ametumia juhudi zake binafsi kuchimba visima ndani ya jimbo lake, lakini pamoja na hilo ameendelea kutupatia ushirikiano kwenye namna ya kutatua changamoto katika visima ambavyo ni kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Serikali kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge tutaenda kuhakikisha tunachukua hatua stahiki

ili kuweza kutatua changamoto ambayo imejitokeza katika jimbo lako Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kinamapula, Kata ya Uyogo, Ulewe na Kata ya Mapamba ni kata ambazo hazina mradi kabisa wa maji, lakini pia na watafiti wamefanya chini ya ardhi hakuna maji. Hata shule za msingi na sekondari wanafunzi wale wanateseka sana. Ni nini mkakati wa dharura wa Serikali kusaidia eneo hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana kaka yangu kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini pia tunao mradi mkubwa katika Jimbo lake la Ushetu ambapo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akiwa Waziri wa Fedha walienda kusaini ndani ya jimbo lake na huo mradi tunaamini kwamba unaenda kutatua changamoto nyingi, lakini tunatambua kwamba ukubwa wa tatizo bado unahitaji jicho la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge tutaenda kuhakikisha tunafanya tathmini na kujiridhisha katika maeneo ambayo bado hayatopitiwa na miradi inayoendelea ili tuweze kufanya usanifu na kufikisha huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kuzingatia na kuchukua hatua kutokana na maelekezo ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ya kuhakikisha shule, zahanati na taasisi zingine za umma zinapatiwa huduma ya maji safi na salama ili kutosababisha magonjwa ambayo ni ya mlipuko. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona. Maji ya Ziwa Victoria yameshafika katika Jimbo la Tabora Mjini na tenki la Itumba linapokea maji kutoka Ziwa Victoria na kufika pale kwa ajili ya kusambaza kwa ajili ya wananchi wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya mabomba kutoka Bwawa la Igombe kupeleka maji kwenye tenki la Itumba ili changamoto yoyote inapotokea katika Ziwa Victoria basi maji yale yaweze kusaidia wananchi kupata maji kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali kupeleka kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa mabomba haya ili tuweze kupata maji wakati wote hata kama kunapatikana changamoto katika mitambo ya Ziwa Victoria?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi imetekelezwa kwa kishindo ni katika Jimbo la Tabora Mjini. Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ndani ya Tabora Mjini ni zaidi ya 98%, lakini kinachotakiwa hapa, Mheshimiwa Mbunge anachohitaji, ni *resilience* au *backup, in case* linatokea jambo ambalo maji ya Ziwa Victoria yana changamoto, basi maji ya kutoka Igombe yaweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakutoa hofu Mheshimiwa Hawa, tumepokea kwa sababu wananchi wa Tabora Mjini ni wa thamani sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tutahakikisha fedha hizo tunazipeleka, tukaweke mabomba hayo ili yaweze kuhakikisha kwamba yanatengeneza *backup* ya kutosha kwa ajili ya maji ya wananchi wa Tabora Mjini. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, aulize swali lake.

Na. 469

Utoaji wa Elimu Bure Nchini

MHE. MWITA M. WAITARA aliuliza: -

Je, Serikali inatoa elimu bure au inatoa elimu bila ada?

MWENYEKITI: Majibu, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya utoaji wa elimu-msingi bila mzazi/mlezi kuchangia ada. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilitoa Waraka wa Elimu Na. 03 wa mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa elimu-msingi bila malipo ambapo umebainisha majukumu ya kila mdau na kuweka utaratibu wa namna wanavyoweza kuchangia michango mbalimbali katika kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hadi 2025/2026, Serikali imetoa jumla ya shilingi 1,394,885,918,000 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa shule. Kati ya fedha hizo shilingi 488,190,858,000 zimetolewa kwa shule za msingi na shilingi 906,695,060,000 zimetolewa kwa shule za sekondari. Utoaji wa fedha hizi umeendelea kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila

Malipo pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kusisitiza wadau wote wa elimu kuzingatia taratibu, kanuni na miongozo iliyowekwa ili kuimarisha mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji, kuongeza upatikanaji wa elimu na kuendelea kuboresha ubora wa elimu nchini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza ninafurahi kwamba Serikali imesema ni elimu bila ada, sio elimu bure. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa sasa wanafunzi wa *O-level* na *A-level* wanapewa yaani fedha ya uendeshaji shule inaenda pale shilingi 1,500 kwa mwezi, lakini fedha hiyo ni kwa ajili ya mitihani, ulinzi, upishi, *stationery*, umeme, ukarabati, vifaa vya maabara, michezo, posho na *extra duty*. Je, hii fedha kwa maisha ya sasa, Serikali inadhani kwamba inaweza kusaidia kuendesha shule zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; ada ya shule, *O-level* ilikuwa ni shilingi 20,000 na *advance level* ilikuwa ni shilingi 40,000, lakini ninayo hapa *joining instruction* ambayo inaendeleza michango ya uendeshaji, sijui ma-*counter book*, mafagio, majembe, magodoro; ukihesabu hii michango inaenda shilingi 400,000 hadi 600,000.

Sasa swali langu ni kwamba Serikali haioni kwamba ni wakati sasa iache wazazi na walezi walipe ada kwa sababu ni nafuu kwao halafu yenyewe ibebe mizigo ya hii michango ambayo ni mikubwa sana? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kwa kuwa mdau mzuri sana wa sekta ya elimu, lakini kwanza nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua chanzo na msingi wa kuwa na Waraka Namba 03 wa Elimu na Mafunzo wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wimbi la wazazi au walezi kutokuwapeleka kabisa watoto shule kwa hofu ya kutoweza kulipa ada, kwa hiyo, *enrolment rate* ya wanafunzi ilikuwa chini. Wanaostahili kuingia darasa la kwanza na kidato cha kwanza walikuwa hawapelekwi na sababu kubwa ya wazazi ikiwa ni kwamba hawana ada ya kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa elimu, ikaona iondoe kikwazo cha ada kwa kuanza kulipa yenyewe Serikali na wazazi wawapeleke watoto bila ada na hiyo ilileta matunda makubwa sana. Kuanzia Januari, 2016, wanafunzi wengi sana wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na hata shule za awali, waliweza kwenda shule. Kwa hiyo, dhumuni la Serikali lilitimia kwa eneo hilo kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanakwenda shule kwa umri unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali imeendelea kutoa fedha. Kwa mfano, wanafunzi wote wa shule za msingi wanalipiwa, kila mwanafunzi shilingi 10,000 na wanafunzi wote wa sekondari wanalipiwa shilingi 25,000 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na uchapishaji, lakini pia wanalipiwa shilingi 20,000 nyingine, kwa ajili ya ada, kwa maana ya wanafunzi wa kutwa. Wanafunzi wale wa bweni wanalipiwa shilingi 70,000 nyingine kama sehemu ya ada na kila mwanafunzi analipiwa shilingi 1,500 kila siku, kwa ajili ya huduma ya chakula. Kwa hiyo, unaweza ukaona kiasi ni gani Serikali imeweza kutenga fedha nyingi kuhakikisha kwamba wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri na kuepusha changamoto za michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu hoja yake kwamba labda Serikali iache kulipa ada ili iweze kulipia michango mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kuendelea kulipa ada kwa niaba ya wazazi na walezi ili kuwezesha wanafunzi kuendelea kusoma bila vikwazo. Ukiangalia waraka huu, umetoa maelekezo katika *section 3.3* majukumu ya mkoa, *section 3.4* na *section 3.7* majukumu ya mkoa na wilaya kwa utaratibu huo na wanaelekezwa kufuata taratibu ikiwa kuna uhitaji wa michango muhimu kuwezesha wanafunzi kusoma wanashirikisha wazazi kwenye mikutano ya pamoja kati ya Kamati na Bodi za Shule na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wanathibitisha na wanachukua hatua pale ambapo inajitokeza michango isiyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kujibu swali la Mheshimiwa Waitara kwa kutoa wito kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya kote nchini na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wasimamie kwa karibu utekelezaji wa Waraka wa Elimu Namba 03 wa mwaka 2016 kwa kuzuia michango holela ambayo haijafuata utaratibu. Natumia nafasi hii pia kuwahamasisha wananchi wa Tanzania, wazazi na walezi kuona umuhimu wa kushiriki kuchangia elimu za watoto wao katika yale maeneo madogo madogo yanayohitaji ustawi wa watoto, ili watoto wetu wasome katika mazingira mazuri na tujenge Taifa lenye elimu bora kwa manufaa ya kizazi hiki na kinachokuja. Ahsante.

MWENYEKITI: Jibu lilikuwa refu, bado mnahitaji maswali ya nyongeza?

Mheshimiwa Husna Sekiboko.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuondoa kikwazo cha ada kwenye elimu ya msingi na sekondari, jambo ambalo limesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kikwazo hicho cha ada kwa elimu ya kati na hasa elimu ya ufundi ili wanafunzi wote hawa waweze kupata ujuzi unaostahili?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Sekiboko, Mwenyekiti wa sekta hii ya elimu amekuwa Mwenyekiti bora sana na mwakilishi mzuri sana wa wanawake katika Mkoa wa Tanga na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ni sikivu ambayo tunaendelea kufanya maboresho mara kwa mara kwa sekta ya elimu kadri ambavyo tutaona inafaa. Tuchukue mawazo hayo, kwa ajili ya kuendelea kuyafanyia kazi, ili tuendelee kuboresha sekta ya elimu katika elimu ya kati, vyuo na maeneo mengine. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Motto, kwa kifupi.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali inahakikishaje shule zote za Serikali zinatekeleza kikamilifu Sera ya Elimu Bila Ada?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Asha Motto kwa uwajibikaji na ufuatiliaji wa karibu wa sekta ya elimu. Namhakikishia tu kwamba Waraka ule Namba 03 wa 2016 umeelezea kila mdau na majukumu yake; ngazi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mikoa, Wilaya, Mkurugenzi, Kamati na Bodi za Shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezea kwamba wajibu wa Serikali katika kila eneo ni kuhakikisha waraka unazingatiwa na kuepusha michango holela, kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge

kwamba Serikali kupitia Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Wakuu wa Mikoa, inapitia mara kwa mara michango inayotolewa shuleni na wazazi na kujiridhisha kuwa ina sababu za msingi. Ikiwa haina sababu za msingi, Serikali inazuia na kuchukua hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kipengele namba 3.5 inaelezea kwenye ngazi ya mkoa na wilaya kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watakuwa na wajibu wa kuchukua hatua pale ambapo kunakuwa na michango ambayo haijafuata utaratibu. Nakuhakikishia, Serikali itaendelea kusimamia utaratibu huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunamalizia na Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge, aulize swali lake.

Na. 470

Ufinyu wa Maeneo kwa Shughuli za Kiuchumi, Sikonge

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa mapori ya akiba kwa ajili ya ufugaji, kilimo na urinaji asali Sikonge?

MWENYEKITI: Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Amosy William Maganga, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasimamia maeneo ya mapori ya akiba kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori nchini, Sura 283. Sheria hiyo imeweka bayana shughuli mbalimbali zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa ndani ya maeneo ya hifadhi kwa kuzingatia malengo na umuhimu wa kutenga maeneo hayo kwa shughuli za uhifadhi. Kwa mujibu wa sheria hiyo, shughuli za kibinadamu, ikiwemo kilimo na mifugo, haziruhusiwi kufanyika ndani ya mapori ya akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza dhana ya ushirikishwaji wa jamii katika kuhifadhi rasilimali za wanyamapori na mazingira yake nchini kwa kuruhusu wananchi kutekeleza shughuli za kiuchumi, ikiwemo uvuvi na ufugaji nyuki ambazo ni rafiki katika baadhi ya mapori ya akiba. Lengo la kuanzisha shughuli hizo ni kuwawezesha wananchi kupata fursa ya kujipatia kipato na kujikimu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2025, jumla ya vibali 3,814 vya ufugaji nyuki vilitolewa kwa wananchi 3,354 kutoka katika Wilaya za Mlele, Sikonge, Kibondo, Kasulu na Kakonko. Vibali hivyo vilitolewa katika Mapori ya Akiba Moyowosi (2,625), Ugalla (478), Rukwa (117) na Inyonga (136) kutokana na mahitaji ya wananchi wa eneo husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Engineer Amosy Maganga.

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 Tume ya Mawaziri Wanane ilizunguka katika nchi hii ili kubaini changamoto na migogoro, hususan katika vijiji ambavyo vinapakana na misitu ya akiba. Wilayani Sikonge tunashukuru tume hiyo ilifika na kwamba katika Wilaya yetu ya Sikonge waliweza kutoa kiasi cha hekta 5,000 ili ziweze kugawanywa kwa wananchi wa Nyahua, pamoja na Kipili, lakini mpaka tunavyoongea hivi sasa hilo eneo bado halijagawiwa kwa sababu ya ukosefu wa takribani shilingi milioni 500, ili kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Je, Serikali haioni sasa kuna sababu ya kutoa hizo shilingi milioni 500 ili hawa wananchi waweze kugawiwa maeneo na kuondoa hizo changamoto zilizopo katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile swali la pili; hii tume ilienda muda mrefu kidogo, takribani miaka mitano na mpaka hivi sasa kilio cha wananchi kutafuta maeneo kimekuwa ni kikubwa sana.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba kuna sababu ya kuongozana pamoja na mimi ili kusudi aweze kuwasikiliza hawa wananchi na hatimaye aweze kutoa ushauri mzuri kwa Serikali, ili hawa wananchi waweze kuongezewa maeneo pamoja na maeneo ambayo tume hiyo haikuweza kufika?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nampongeza Mheshimiwa Amosy Maganga, Mbunge wa Sikonge kwa maswali mawili ya nyongeza yenye faida kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2021 Tume ya Mawaziri Nane ilifika katika eneo la Sikonge na mimi nilikuwa ni sehemu ya hiyo tume, nilifika eneo hilo. Ni kweli, tulitenga hilo eneo, lakini moja ya maelekezo ambayo tulitoa ni kwamba lazima eneo linalotolewa lipangwe na kuwe na matumizi sahihi ya eneo husika na halmashauri iliji-*commit* kutoa shilingi milioni 500, lakini kutokana na changamoto hiyo namthibitishia tu kwamba Serikali itakaa pamoja na halmashauri na Wizara ya Ardhi na kutafuta namna bora ya kuweza kupata ufumbuzi wa jambo hilo. Kwa hiyo, tutakaa pamoja *as a team* kabla hatujatoa jibu la mwisho, ili tuweze kutoka vizuri katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutembelea eneo hilo, jana Waziri wa Ardhi hapa wakati anahutubia Bunge, alisema moja ya eneo ambalo anakwenda kulifanyia kazi na ametengeneza mpango, ni ile Tume ya Mawaziri Wanane kumalizia ile kazi ambayo ilikuwa imebaki. Kinachotakiwa hapa ni sisi tu Wabunge tupitishe bajeti yake, ili ule mpango ambao Waziri ameuainisha wa Mawaziri Nane tuweze

kwenda huko. Kwa hiyo, ni tofauti na kumtaka Naibu Waziri peke yake, tume ifike katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ndiyo itakayotusaidia kufika katika eneo hilo, ukiacha Waziri kufika, lakini Mawaziri Nane na wenyewe watafika baada bajeti hii kuweza kupitishwa. Kwa hiyo, namthibitishia Mheshimiwa Mbunge, tume itafika, lakini na Naibu Waziri au Waziri husika atafika katika eneo lako. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa nafasi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza maeneo ya uzalishaji bila kuharibu mazingira na Hifadhi za Taifa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. Maeneo ya uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninafikiri mpango wa kuongeza maeneo ya uwekezaji ni sehemu ambayo ukiangalia wakati wa hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, aliainisha namna bora ya kuongeza maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya maeneo ambayo tunakwenda kuongeza, kutenga maeneo, kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi ni sehemu ya hayo mambo. Wizara ya Ardhi inafanya jukumu hilo la kuhakikisha kwamba wawekezaji wanapokuja hapa nchini, pamoja na wawekezaji wa ndani wanapata maeneo hayo bila usumbufu wowote na wanawekeza. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi cha maswali. Ninaomba nilete matangazo machache; kwanza kabisa ni wageni ambao wako Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Hawa ni wageni watatu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaye Kamishna Jenerali Aretas Lyimo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Tunaye pia Dkt. Peter Mfisi, yeye ni Kamishna wa Kinga na Tiba na yupo Ndugu Abel Mwakyeka, yeye ni Kamishna wa Utawala. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine ambao wako Jukwaa la Spika ambao ni wa Mheshimiwa Naibu Spika; hawa ni Ndugu Mchulila Sebabili, mpigakura wake, lakini tuna wageni wengine 32 wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Kijiji cha Olasiti, Kata ya Nkaiti, Babati, Mkoani Manyara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Vilevile tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga; hawa ni viongozi wa chama kutoka Makete. Tunaye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe - Ndugu Clemens Mumwite, lakini ameambatana na Katibu wa CCM Wilaya ya Makete - Ndugu Daniel Mhaza. *(Makofi)*

Wageni wengine tutawatangaza kadri muda unavyozidi kwenda. Majina yao hayajafika hapa kwenye Kiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine hapa linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake wa Majimbo; anawatangazia Wabunge Wanawake wa Majimbo kuwa leo Ijumaa, tarehe 29 Mei, 2026 mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, saa 7.00 mchana, mtakuwa na kikao. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi Namba 20, uliopo Jengo la *Utawala Annex.*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo Mheshimiwa Naibu Spika atakuja kuendelea na kikao chetu.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

29 MEI, 2026

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MAAZIMIO

Azimio la Bunge la Kuipongeza Timu ya Taifa ya Vijana Wanaume Chini ya Umri wa Miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa Kufuzu Fainali za *AFCON 2026* na Kukata Tiketi ya Kushiriki Mashindano ya Kombe la Dunia la Vijana Chini ya Umri ya Miaka 17, Mwaka 2026

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge la Kuipongeza Timu ya Taifa ya Vijana Wanaume Chini ya Umri wa Miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa Kufuzu Fainali za *AFCON 2026* na Kukata Tiketi ya Kushiriki Mashindano ya Kombe la Dunia la Vijana Chini ya Umri ya Miaka 17, Mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 ili niweze kuwasilisha hoja ya Azimio la Bunge la kuipongeza timu yetu ya Taifa ya Vijana ya Wanaume chini ya umri wa miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa mafanikio makubwa iliyoyapata hivi karibuni kwenye Mashindano ya Vijana ya Afrika, *AFCON Under 17*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tumeshuhudia jana tarehe 28 Mei, 2026 timu hii ya *Serengeti Boys* ikipata ushindi dhidi ya Timu ya Taifa ya Vijana ya Misri katika mchezo wa nusu fainali. Timu yetu ilishinda kwa mikwaju ya penati nne kwa tatu baada ya timu zote kutoka suluhu bila kufungana hadi mwisho wa mchezo huo uliofanyika nchini Morocco. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo Serengeti *Boys* imefuzu kucheza Fainali za Mataifa ya Africa *(AFCON under 17),* ambayo yanatarajiwa kufanyika mwaka huu wa 2026. Aidha pamoja na kufuzu kushiriki fainali za *AFCON under 17,* Timu yetu ya Selengeti *Boys* pia imefuzu tiketi ya kushiriki Mashindano ya Kombe la Dunia kwa

Vijana wa Chini ya Umri ya Miaka 17 ambayo yanatarajiwa kufanyika nchini Qatar mwaka huu 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huu wa *Serengeti Boys* na hatua waliofikia kimichezo ni jambo kubwa la kihistoria ambalo halijawahi kutokea hapa nchini kwa muda mrefu. Timu hii inapaswa kupongezwa na kupewa moyo, ari na hamasa kutoka kwa Watanzania wote tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ushiriki wa timu hii ya *Serengeti Boys* katika mashindano hayo ni fursa kubwa ya kuitangaza nchi yetu ya Tanzania kimataifa; kuitangazia dunia kuwa sisi ni nchi ya amani na kwa njia hiyo tutakuza utalii na uwekezaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Rais wetu ambaye ndiye mwanamichezo namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuimarisha sekta ya michezo kupitia uwekezaji mkubwa alioweka kwenye michezo ambao unaleta motisha kubwa kwa vijana wetu wanamichezo kwa ujumla, kuongeza juhudi za ushiriki katika mashindano mbalimbali ambayo timu zetu za Taifa zinashiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia; nitumie pia fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Rais wetu ambaye ndiye mwanamichezo namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuimarisha sekta ya michezo kupitia uwekezaji mkubwa alioweka kwenye michezo ambao unaleta motisha kubwa kwa vijana wetu wanamichezo kwa ujumla, kuongeza juhudi za ushiriki katika mashindano mbalimbali ambayo timu zetu na timu ya Taifa inashiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huu wa *Serengeti Boys* ni zawadi kubwa kwa Rais wetu mpendwa. Nasi Waheshimiwa Wabunge tunampa moyo wa kuendelea kuinua sekta ya michezo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa ninaomba uniruhusu niweze kuliwasilisha azimio hili mahsusi la

pongezi kisha nitoe hoja ambayo kwa ridhaa yako nitaomba ichangiwe na Waheshimiwa Wabunge. Azimio lenyewe ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge la Kuipongeza Timu ya Taifa ya Vijana Wanaume Chini ya Umri wa Miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa Kufuzu Fainali za *AFCON 2026* na Kukata Tiketi ya Kushiriki Mashindano ya Kombe la Dunia la Vijana Chini ya Umri ya Miaka 17, Mwaka 2026.

Kwa kuwa timu yetu ya Taifa ya Vijana Chini ya Umri wa Miaka 17 *(Serengeti Boys)* ambayo inashiriki michuano ya *AFCON* kwa vijana huko Morocco, jana tarehe 28 Mei, 2026 ilipata ushindi kwa mikwaju ya penati nne kwa tatu dhidi ya timu ya Vijana ya Taifa la Misri;

Na kwa kuwa ushindi huo wa *Serengeti Boys* umeiwezesha kufuzu fainali ya *AFCON* kwa vijana chini ya umri wa miaka 17 ambayo inafanyika mwaka huu. Vilevile, ushindi huo umewezesha *Serengeti Boys* kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia kwa Vijana Chini ya Umri wa Miaka 17 itakayofanyika mwaka huu nchini Qatar.

Na kwa kuwa ushindi huu ni jambo kubwa la kihistoria katika maendeleo ya soka na michezo hapa nchini kwani kwa miaka mingi timu zetu za hapa nchini hazijawahi kufikia mafanikio na hatua kama hiyo;

Na kwa kuwa ushirika wa timu ya *Serengeti Boys* katika mashindano haya umeiletea Tanzania sifa kubwa kimataifa, kutangaza utalii wa nchi yetu, kuvutia wawekezaji na kuidhibitishia dunia kwamba Tanzania ni nchi ya amani;

Na kwa kuwa maendeleo ya michezo hapa Tanzania yanachochewa na wadau mbalimbali akiwemo kiongozi mkuu wa nchi yetu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha michezo;

Na kwa kuwa ushindi wa *Serengeti Boys* ni jambo linapaswa kupongezwa na Watanzania wote, hususani sisi Wabunge ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi;

Kwa hiyo basi katika Kikao chake cha 39 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, Bunge linaazimia kuipongeza timu ya *Serengeti Boys* kwa ushindi ilioupata na hivyo kufuzu fainali za *AFCON,* na pia Kombe la Dunia kwa Vijana Chini ya Umri wa Miaka 17, mwaka huu 2026, kuipa timu ya *Serengeti Boys* moyo, hamasa na ari ya kupambana katika fainali hizo walizofanikiwa kuingia ili hatimaye wapate ushindi na kuiletea Tanzania sifa nzuri, na kumpongeza mwanamichezo namba moja Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuinua na kuhamasisha Sekta ya Michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Hoja imotolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Ester Amos Bulaya kwa kuwasilisha hoja mezani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja kutolewa na kuungwa mkono, tunayo orodha ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatana na Mheshimiwa Husna Sekiboko na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae. *(Makofi)*

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo imetolewa mezani. Kwanza, niseme kwamba ninaunga mkono hoja ya kuwapongeza *Serengeti Boys.* Pia ninampongeza aliyeleta hoja hii mezani, dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, jirani yangu kabisa hapa, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa na mafanikio makubwa sana kwenye michezo, inawezekana ukipima ni kuliko Marais wote ambao wamewahi kuwepo katika nchi yetu. Kwenye sekta ya michezo kipindi cha Dkt. Samia tumefanya vizuri sana kwenye riadha, ngumi, *football* na hata kwenye timu kubwa ya Taifa tumefika 16 bora kwenye *AFCON*. Ni kitu kikubwa sana kwenye nchi yetu. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa Mheshimiwa Rais na ndiyo maana *CAF* waliamua kumpa tuzo ya kutambua mchango wake kwenye michezo na kwenye mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa anamwapisha Mheshimiwa Paul Christian Makonda alizungumza maneno haya; alisema, "Nina uhakika kazi ninayokupa unaiweza na mchaka mchaka huu unauweza." Kwa haya yanayoendelea tunaona kabisa kwamba Wizara inafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri, Paul Christian Makonda. Wizara ya Michezo sio Wizara ya kulala, ni Wizara ya mchakamchaka. Ni Wizara ambayo kila siku tunahitaji kuona matunda na tunahitaji kuona watu wakishughulika hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata haya yanayoendelea ni kwamba ni kazi kubwa Wizara na Baraza la Michezo linafanya, lakini pia *TFF* wanafanya kazi kubwa. Nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri na nimpongeze na tuna uhakika diplomasia ya michezo inatafsiriwa kwa vitendo siyo kwa kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana walichokifanya kule Rabat, Morocco, diplomasia ya michezo kati ya Tanzania na mataifa mengine inakua. Watu wanaendelea kuiangazia Tanzania kwenye sekta ya michezo na ndiyo maana kati ya watu wabobezi wa soka duniani Arsene Wenger jana amejitokeza akiipongeza Tanzania kwa kile ambacho wamekifanya. Ni lini tungempata Arsene Wenger akaipongeza Tanzania kama si kupitia mafanikio ya Dkt. Samia Suluhu Hassan? Kwa hiyo, ninaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika *issue* yoyote ile Mheshimiwa Waziri, Rais akiwa na *political will* ya kuendeleza michezo ndipo tunapoenda kufanikiwa. Tumeiona *political will* ya Mheshimiwa Rais kwenye kujenga *infrastructures* za michezo. Viwanja vinajengwa kila kona. Pili ni hamasa anayoitoa, goli la mama, anayoyafanya na maeneo mbalimbali ambayo anachagiza kuhakikisha kwamba ana-*support* timu zetu za michezo. Ni vyema tukaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Pia Mheshimiwa Waziri asichoke, aendelee kuhamasisha michezo kwenye nchi yetu. Wapo watakaomkatisha tamaa, ni kazi yao lakini sisi tunachagua kusonga mbele katika kuhamasisha michezo. Mheshimiwa Makonda huu muziki anauweza kuucheza na ninajua kuwa yeye si kinara wa sifa tu, wakikuchukia wanakuchukia, wakikufurahia wanakufurahia, wewe unasonga mbele. Kwa hiyo, mimi ninamuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri kama tunawaunga mkono vijana hawa tafsiri yetu ni moja, Watanzania huko nje wanajiuliza swali moja, kwamba wakishatoka huko hatua gani zinafuata? Nitoe angalizo kwa Watanzania, tuna changamoto ya kuwa na mameneja uchwara, tuna changamoto ya kuwa na watu ambao wanaitwa mawakala, kwa hawa wachezaji na tuna changamoto ya kutokuwaandaa kisaikolojia hawa wachezaji. Kwa jinsi ambavyo wame-*perform* jana, ungekuwa unafuatilia michezo, wali-*perform* katika kiwango ambacho tunahitaji kama Taifa kuwaandaa vijana wakirudi basi tuwe na watu maalum ambao wataa nao kisaikolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko maalum yaandaliwe kwa ajili ya hawa vijana, kuliko wakija wakakimbilia kwenye hizi timu nyingine ambazo zimekuwa na tamaa kuwachukua na kuwakalisha wachezaji bila kuwatumia. Basi tuwaandalie masoko ya kimataifa wachezaji wetu wakafanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono wa hoja na ninaiunga mkono Wizara ya Michezo. Ninamtakia kila la heri Mheshimiwa Rais na hawa vijana tunaamini fainali tunabeba ubingwa, tunarudi nao nyumbani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FESTO R. SANGA: ... lakini nimtakie kila la heri Mheshimiwa Waziri, Makonda, pamoja na timu nzima ya Wizara ya Michezo kuhakikisha kwamba tunamuunga mkono. Zaidi na *TFF* kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kubwa zaidi ni kwamba...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FESTO R. SANGA: ...aliyeifikisha nusu fainali au fainali hii timu ni kocha ambaye ni mzawa, akina Mirambo na kocha mwenzake. Ni watu ambao ni Watanzania wenzetu. Ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kama mdau wa michezo nina furaha na Watanzania wanafurahi kuona *Serengeti Boys* inafanya vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa Husna Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, ni dakika tatu kuchangia.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa fursa ili na mimi niweze kuweka mchango wangu katika kuunga mkono pongezi nyingi za dhati na za upendo sana kwa vijana wetu na watoto wetu wa timu ya *Serengeti Boys.* Timu ya watoto chini ya miaka 17 ambao kwa kweli wameitangaza Tanzania. Dunia nzima jana imeijua Tanzania. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo haya yametokana na juhudi na jitihada na utayari wa Serikali katika kuwekeza katika sekta ya michezo. Ametangulia kusema hapa mzungumzaji aliyetangulia kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluh Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa na utayari wa

kuwekeza katika ujenzi wa viwanja, vilevile amewekeza katika ujenzi wa akademia za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tunaona watu wanapiga kelele kwa nini tusilee vipaji vya watoto tangu wakiwa wadogo. Ndani ya miaka mitano ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imefunguliwa akademia ya michezo pale Kigamboni, imefunguliwa akademia ya michezo pale Tanga, na zinafunguliwa akademia za michezo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Zinalea vipaji vya watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Samia Suluh Hassan ameweka miundombinu ya kulea vipaji vya watoto hadi shuleni. Watoto wa miaka 17 ni watoto walioko shuleni, lakini sasa kwa miundombinu na kwa nyenzo ambazo ameziweka Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari wameshajua kwamba wanalo soko la ajira la wazi kabisa katika mpira wa miguu. Tunaipongeza sana Serikali na tunawapongeza sana viongozi wote wa Wizara wakiongozwa na ndugu yangu Paul Makonda kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameifanya katika kuhakikisha kuwa jambo hili linatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza wenzangu, vijana hawa baada ya hapa sisi kama Taifa tunakwenda kuwatunuku nini kwa jambo kubwa walilofanya la kuitangaza nchi yetu? Hii timu inaitwa *Serengeti Boys.* Imeitwa Serengeti kwa lengo la kuitangaza mbuga yetu ya Serengeti. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii na *Serengeti National Park* yenyewe wanajua kwamba vijana hao wameitangaza Serengeti? Na je, wamejiandaa vipi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba angalau wanawapa nyenzo ya kuendelea kuwatia moyo na kuhakikisha kwamba wanaendelea kuitangaza nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai, pamoja na pongezi nyingi tunazotoa, lakini kama Taifa lazima tukubali kwamba vijana hawa wametuwakilisha vizuri. Wapewe zawadi kwa kuitangaza nchi yetu, na katika michuano mingine tuone kuwa kwenye jezi zao zinaendana na jina la Serengeti.

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: ... jezi zao ziwekwe nembo ya Serengeti.

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: ... Serengeti wawajibike kusaidia vijana hawa na waendelee kufanya vizuri na kuendelea kuitangaza nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ninawatakia heri sana. Soko lao la ajira limeonekana. Tumeona ma-*agent* wengi wa michezo wanawasifia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sekiboko.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani watapata ajira kimataifa na sisi tuwe tayari kuwasaidia. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Baraka umeomba taarifa wakati Mheshimiwa anahitimisha. Kwa hiyo, muda wa taarifa ulishaisha Mheshimiwa Asha Baraka, kwa hiyo ninaomba ukae.

Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula atafuatiwa Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuweka mchango wangu katika azimio hili ambalo liko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua Taifa waangalie vijana wake leo. Leo vijana wetu hawa *Serengeti Boys under 17* wamethibitisha kwamba vijana ndiyo wanaotoa dira ya Taifa. Katika sekta ya michezo tunakwenda kuona michezo inaenda kufunguka

kupitia vijana hawa. Kupitia vijana hawa, vijana wa shuleni na vijana wa mtaani wameona kumbe inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unasema ukiona mtoto yuko juu jua kuna mkono chini umembeba. Ushindi huu haujaja kwa bahati mbaya. Ushindi huu umekuja kwa sababu tuna kiongozi mwenye maono, tuna kiongozi shupavu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi wote ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais tangu ameingia madarakani tumeona mchango wake mkubwa katika sekta ya michezo. Kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais ameenda kuheshimisha sekta ya michezo, kuwaheshimisha wanamichezo na pia kutoa thamani katika wanamichezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara nyingi tumemuona Mheshimiwa Rais hata akitoa ndege kuwafuata wachezaji na tunaona hamasa kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais. Yote haya yameleta leo tunaona manufaa kwa vijana wetu hawa. Sisi Watanzania tujivunie sana kitu ambacho kimefanywa na vijana wetu hawa. Wameongea wazungumzaji Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli Tanzania imeenda kwenye ramani ya dunia hata kwenye sekta ya michezo na sisi Tanzania tunasomeka tunafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutumie nafasi hii kupitia vijana wetu hawa ambao wameenda kuitangaza Tanzania, kupitia vijana wetu hawa ambao wamefuzu kushiriki fainali za *AFCON* na fainali hizi tunaamini kupitia maombi ya Watanzania na hapa niwaombe Watanzania tuungane kwa pamoja kuwaombea dua vijana wetu hawa. Tuwaombee sala vijana wetu hawa ili ushindi uwe kwetu na ushindi utakapokuja kwetu Tanzania ikatangazwe kimataifa zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo tumeliona hapa. Tumeona uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na Serikali na hapa Mheshimiwa Waziri siwezi kuacha kukupongeza, hakika kazi imepata mtu. Tunaona hekaheka zako kwenye sekta hii ya michezo, kazi unaiweza, unaifanya vizuri. Tunaamini vijana hao watakaporudi

Mheshimiwa Waziri utafanya jambo kubwa kwa ajili yao. Hatuna mashaka na wewe. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia pongezi hizi ni za kwetu Watanzania wote, lakini zikiongozwa na Mheshimiwa Rais, mwanamichezo namba moja. Tunawapongeza sana vijana wetu *under 17*. Mungu awabariki sana kwa kuitangaza Tanzania kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Sylvia. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nitumie kuwapongeza sana timu yetu ya *Serengeti Boys* kwa kufuzu mashindano ya *AFCON* na kuweza kushiriki katika Kombe la Dunia la Vijana chini ya miaka 17 wa kiume. Tuna maneno tunasema kila kinachong'ara na kupendeza kimegharimiwa. Kwa hiyo, Serikali ninaipongeza sana kupitia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kugharimia kuwekeza katika sekta hizi za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu utatoa chachu kwa vijana wengine kushiriki katika michezo kwa sababu hapa timu yetu hii imeifanya sasa Tanzania kuendelea kutangazika zaidi duniani, pia inaonesha sasa namna Serikali na viongozi wake wanavyothamini michezo na wanavyothamini vijana wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ushindi huu wa *AFCON* vijana wengi watahamasika kuingia kwenye michezo kwa sababu sasa wanaona michezo inazidi kuwa ni ajira, michezo inazidi kuwa ni kipato kwao. Hapa tayari tuna mtaji wa timu zetu za Taifa, vilabu vyetu vikubwa kupata wachezaji bora ambao wataweza kushiriki hata

kwenye vilabu vingine vya kimataifa. Kwa hiyo, hapa zitapatikana ajira za ndani, lakini na ajira za nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea sana kuwapongeza vijana wetu. Katika kuongezea, pongezi ziende kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake. Mheshimiwa Waziri na timu yako unafanya kazi kubwa sana kumsaidia Mheshimiwa Rais katika sekta hii ya michezo. Tunaomba taasisi zote zinazoshughulika na michezo ziendelee kuongeza juhudi zaidi katika kuwekeza zaidi kwenye michezo kwa ajili ya kuliinua Taifa kuwasaidia vijana wasiingie kwenye vitendo viovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninashauri katika hili kuwe na namna fulani ambayo itaweza kusaidia Watanzania kwenda kushiriki kuwashangilia hao vijana wetu watakapocheza hizo fainali za Kombe la Dunia. Tuone namna ya unafuu wa kuwashirikisha wananchi na vijana wengine kwenda kuwa-*support* vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa kutumia fursa hii adhimu niweze pia kuwapongeza *Tanzanite Queens*, jamani timu yetu hii ya chini ya miaka 20 imefanya vizuri na wao wanaingia sasa kwenye Kombe la Dunia. Hapa tunaona uwekezaji mkubwa kwenye sekta hii ya michezo kwa vijana wa kike na kwa vijana wa kiume. Tunakwenda sambamba kuwawezesha na kuitangaza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninatumia fursa hii kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nimemtaja Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Paul Christian Makonda ajiandae.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaanza kuunga mkono hoja ya dada yangu Mheshimiwa Ester na niseme imekuja wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kwa moyo wangu wa dhati nimesimama hapa kuipongeza timu yetu ya *Serengeti Boys* kwanza kama mdau wa michezo, lakini na kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya vijana hawa kwa kuendelea kuipeperusha bendera yetu ya Taifa na kwa kuendelea kuonesha kwamba kumbe bado kama Taifa letu la Tanzania tunavyo vipaji mahiri vya vijana ambao wakiwezeshwa, wakipewa nguvu wanaweza kufanya vizuri katika soka la kimataifa. Vijana hawa kiukweli wametuonesha mfano mzuri sana wa kuigwa na nimesimama hapa kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya hayawezi kutokea hivi hivi. Kama mdau wa michezo lazima niseme, haya yanatokea ni pamoja na maono mazuri ya utekelezaji wa Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Michezo ni pamoja na mazingira unayoandaa, ushindi unatengenezwa kutokana na mazingira unayoandaa kwa timu yako ili uweze kushinda. Hawawezi kwenda kushinda kama hawajajiandaa kisaikolojia, hawawezi kwenda kushinda kama sera za nchi hiyo hamuwa-*support* vijana wale katika michezo na hawawezi kushinda kama mazingira yenyewe hayajakaa katika kuwawezesha hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya sasa ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia inawawezesha vijana hawa kwenda kifua mbele kushindana kwa sababu wanaamini nyuma yao yupo jemadari ambaye amesimama kwa ajili ya kuhakikisha kwamba michezo inapaa na ndiyo maana wamefanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, niseme upele umepata mkunaji. Mheshimiwa Waziri kazi yako tunaiona, sisi kama vijana wenzako tunakuombea, tunatamani uendelee kukanyaga hapo hapo ulipokanyaga. Ninaamini katika awamu yako, kipindi chako hiki michezo utaifikisha mahali ambapo itatengeneza historia katika nchi hii kwa sababu nyuma yako yuko jemadari ambaye anakupa *support* ambaye ni Dkt. Samia na wewe unakwenda na unafanya kazi katika kutekeleza maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia. Kanyaga hapo hapo Mheshimiwa Naibu Waziri tutafika kule tunakotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni furaha, lakini michezo katika Taifa letu ndiyo inayotuunganisha sisi kama Taifa moja. Sehemu ya michezo ndiyo haina itikadi za kisiasa, haina ukabila, haina udini. Kazi kubwa iliyofanywa na hawa vijana imetuunganisha sisi kama Taifa. Vijana hawa wametoka kwenye maeneo mbalimbali katika utendaji wao wa kazi na kazi kubwa na nzuri wametuunganisha sisi kama Taifa. Tunawapongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi kumshauri Mheshimiwa Waziri. Pamoja na mazuri utakayoyafanya vijana hawa wakirudi lazima tuone namna ya kuinua vipaji vyao. Tunazo *academy* hapa za *football academy* ndani ya nchi, lakini fikiria namna ya kuwapeleka vijana hawa kwenye *academy* za kidunia na *academy* zilizo bora za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini na sisi tunataka tupate wachezaji kama Messi wa kesho, tupate mchezaji kama Ronaldo wa kesho kwa kuwapeleka kwenye *academy* za kidunia, *academy* za kimataifa kama ambavyo zinavyofanya vizuri *Barcelona academy*, zipo *academy* kama *Manchester academy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwapeleka kule hawa vijana badala ya kubaki hapa Tanzania wanatapakaa, ukiwapeleka kule hawa vijana maana yake kesho yake tunakwenda kupata wachezaji wazuri wakirudi kutumikia Taifa hili kwenye timu ya Taifa. Pia utakuwa umewasaidia katika kuinua kipato chao na sehemu ya ajira kama sehemu ya ajira yao kwenye michezo ambayo wameamua kuichagua. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana iwe sehemu ya ahadi yako. Wape moyo hawa vijana waambie mkishinda nje na kubaki ndani ya Tanzania tuna namna ya kuwapeleka nje ili muendelee kuimarisha ujuzi, mpate maarifa na mtakaporudi kama Taifa muweze kutumikia Taifa kama Timu ya Taifa

na ndiyo chanzo kizuri cha mchango wa Taifa kupitia sehemu hii ya michezo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Paul Christian Makonda, mtoa hoja ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi nimesimama kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuweza kuleta Azimio hili la kuipongeza Timu yetu ya *Serengeti Boys*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwa kuweza kwa kweli kuingia fainali ya mashindano ya *AFCON Under 17* lakini zaidi kuweza kushinda kwenda kushiriki kwenye *World Cup*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza pia Menejimenti ya Wizara nzima ikiongozwa na Waziri na timu nzima ambayo imeenda kule kwa maana ya benchi na watu wote ambao wameshiriki kuhakikisha kwamba *Serengeti Boys* inafika pale ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na ushindi wa *Serengeti Boys,* lakini pia kwa kipindi hiki cha Awamu ya Sita tumeshuhudia michezo ikishika kasi kwa kasi kubwa sana ambapo timu zetu za *football* za wanawake; *Tanzanite Queens* wamesema hapa imeshinda kwenda *Under 20 Women World Cup*, pia tunayo Twiga inaenda kwenye *WAFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hapo tu, tumeona michezo ikikua kwenye riadha, *netball* na *basketball*. Tumeshuhudia timu yetu ya *Dar City* kwa mara ya kwanza kuweza kuingia kwenye robo fainali ya

mashindano ya Ligi ya Afrika imeandika historia. Haya yote kwa kweli yanatokana na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ameamua kuwekeza kwa vitendo. *(Makofi)*

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Asha Baraka.

TAARIFA

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwa mchangiaji kwamba *Tanzanite Queens* inacheza *World Cup* mwezi Septemba mwaka huu na hapo hapo *Twiga Stars* itashiriki *AFCON* Julai mwaka huu, Morocco. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, taarifa unaipokea?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ulindwe nilikuwa nimeanza. Ninakushukuru dada yangu Mheshimiwa Asha. Nimesema hayo yote, nimewatambua *Tanzanite Queens* wanashiriki *World Cup* na Twiga wanashiriki *WAFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni utashi mkubwa wa kisiasa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeshuhudia na hii ni dhahiri katika kipindi cha Awamu ya Sita kumekuwepo na maboresho kwenye miundombinu ya kimichezo kwenye viwanja mbalimbali ikiwepo ile ya Benjamin, tunaona tunajenga kule Arusha na hapa Dodoma, lakini pia maendeleo ya vijana kuweza kuibua vipaji mbalimbali na ndiyo maana leo tuko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni katika kuhakikisha kwamba Tanzania inafunguka kimataifa kupitia diplomasia ya kimichezo, ndiyo maana leo katika utashi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Taifa limekubali kuwa wenyeji wa mashindano ya *AFCON* ambapo tunawekeza mabilioni ya fedha kuweza kujenga miundombinu ya *AFCON*. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. JAMES K. MILLYA): Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa James Millya.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. JAMES K. MILLYA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sana mzungumzaji anayeongea akaelewa pia kwamba michezo ni diplomasia na kwamba nchi yetu pamoja na kwamba vijana hawa wanacheza vizuri, lakini pia wanapeperusha bendera ya nchi yetu. Hivyo basi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tunatoa wito kwa balozi zetu zote duniani kwamba popote ambapo vijana hawa wanacheza *Under 17*, kwanza tunawapongeza, lakini wapokelewe na waandaliwe mazingira mazuri kwa sababu wanaandaa mazingira ya kupeperusha bendera yetu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, pamoja na maneno mazuri ambayo Mheshimiwa Mbunge anayaongea akumbuke kwamba jambo hili pia ni suala la diplomasia na kwamba Serikali inawaunga mkono sana vijana hawa na tuko tayari kuwapa msaada wa aina yoyote. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa James. Mheshimiwa Esther Matiko, Taarifa unaipokea?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ulindwe. Ninaipokea na nimetaja hapa diplomasia ya kimichezo, Tanzania imefunguka kimataifa. Ninashukuru sana wanaonipa taarifa, lakini muda wangu ulindwe, dakika tatu ni ndogo sana. Kwa hiyo, naomba nianze maana yake hata sijamaliza wanani-*interrupt* sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther, taarifa ni sehemu ya mchango wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumesimama hapa kuwapongeza vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwa kushinda *penalty* nne dhidi ya Egypt. Hii ni tafsiri kwamba ushindi wao siyo tu kwamba ni ushindi wa hayo magoli bali ni uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa vijana ambayo inaonesha dhahiri kwamba inaweza kugeuka kuwa heshima ya Taifa, kuwa uchumi wa michezo, ajira, lakini zaidi kuweza kuipa nguvu Tanzania ya *soft power* duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba anaunganisha michezo, utalii na uchumi wa Taifa. Sasa hivi ndugu zangu watu wengi kwenye utalii hawawekezi kwa wanyamapori tu. Mataifa makubwa yamejielekeza kwenye utalii wa kimichezo ambapo yanaamini kabisa kwamba yataleta watalii, wawekezaji, ajira na uchumi utaenda kukua sanjari kama tulivyosema hapa kuweza kuitangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *Serengeti Boys* wanaitangaza Tanzania duniani, yaani watu duniani wanavutiwa kuangalia nchi yetu, wanatamani kuja Tanzania kupitia *Serengeti Boys*. *(Makofi)*

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tunapotambua ushindi wa *Serengeti Boys* kuandika historia katika Taifa letu, tuweze kumpa kongole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejipambanua kwa utashi wake wa kisiasa kwa mambo mbalimbali, lakini ametamalaki kwenye michezo. Leo hata ligi zetu za Tanzania zinafahamika duniani, leo wachezaji mbalimbali ukiwaambia kuja kushiriki kwenye ligi ya mipira Tanzania wanakuja. Hii yote ni kwa sababu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo ameamini kupitia michezo anaenda kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther, hujaunga mkono hoja bado, unga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo ninaunga mkono Azimio hili ambalo limeletwa hapa

kuwapongeza vijana wetu wa *Serengeti Boys* na kwa kweli tuweze kuwapa zawadi. Tuwatafutie zawadi kama motisha ambayo itaweza kutoa morali kwa vijana wengi kuweza kushiriki kwenye sekta ya michezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Paul Christian Makonda, mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa na mimi ninaungana na Bunge lako Tukufu kuunga mkono hoja nzito iliyotolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya ikiwa ni kuwapongeza vijana wetu *under 17* kwa historia waliyoiandika usiku wa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake binafsi na mapenzi yake ya dhati kwa watoto wa Kitanzania na vipaji tulivyonavyo na kuamua kuichukua Tanzania na kuiweka kwenye ramani ya dunia katika michezo hii tunayoshuhudia leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika uwekezaji uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia katika michezo, morali aliyoiweka katika michezo inatutoa kimasomaso Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wote kwa pongezi walizompa na kwa kweli anastahili kwa kazi nzuri na njema aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirudi kwenye historia utakuja kuona namna ambavyo kipindi ambacho Taifa hili lilipigana vita na Uganda. Baada ya vita ya Uganda Wizara ya Michezo ilinyimwa hata shilingi 100 na kutokea pale Wizara hii ikaonekana ni ya michezo michezo tu. Rais pekee aliyeamua kuwekeza kwenye michezo hapana mwingine bila haya ninaweza kutaja ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi na utashi wake alioweza kuweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, uniruhusu pia niwapongeze sana sana kwa moyo wangu wa dhati *TFF*. *TFF*

wanaosimamiwa na Baraza letu la Michezo *(BMT)* wanafanya kazi kubwa, kazi nzuri ya kuendelea kutambua na kukuza vipaji tulivyonavyo katika Taifa letu. Leo tunaposema *Serengeti Boys* watu wanafikiri labda ni vijana waliotoka kwenye mataifa tofauti na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu, vijana hawa *Serengeti Boys* ni matokeo ya UMISSETA. Ni matokeo ya watoto wa Tanzania, ni watoto wetu, ni vijana wetu waliopatikana kwa njia ya UMISSETA na wapo kwenye vituo vyetu ambavyo Serikali imewekeza kupitia *TFF*. Ukienda pale Tanga, ukienda pale Kigamboni na ukienda kwenye *sports academy* nyingi ambazo zimetengenezwa ndani ya nchi yetu zaidi ya 91. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia nimpongeze kocha. Kocha huyu ni mtoto wa Kitanzania aliyeibeba timu yetu ya Taifa na kuipa heshima ya kuingia kwenye fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu pia ninaomba uniruhusu nimpongeze kepteni, kijana mdogo aliyesimamia kijana wangu Kassim kuhakikisha kwamba timu inakwenda vizuri. *(Makofi)*

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaomba uniruhusu nimpongeze golikipa wetu kijana mahiri, aliyefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Makonda, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

TAARIFA

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Waziri, Paul Christian Makonda kwamba hivi punde kocha wa *Taifa Stars*, Gamondi, amewachagua wachezaji wawili kati ya hawa ambao tunawasifia sasa kuingia

kwenye *Taifa Stars*. Wachezaji hao waliochaguliwa ni Lukman Mbalasalu pamoja na Kassim Juma. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Makonda, Taarifa unaipokea?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ninaipokea kwa unyenyekevu mkubwa na kwa sababu kaka yangu alivyosikia tu jina huku limetajwa la kepteni akajua tayari mambo yameitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza sana golikipa wetu, kijana huyu Haji Ali amefanya kazi kubwa na kwa ujasiri mkubwa. Hakuogopa wala hakushangazwa na aina ya uwanja waliokuwa nao, lakini aliamua kusimama kuhakikisha kwamba analinda goli la Tanzania na kuhakikisha hakuna mtu anayefunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu nimalizie mambo mawili tu ya mwisho; la kwanza, Waheshimiwa Wabunge wametaka kujua baada ya hapa Serikali ina mpango gani? Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ametupa maelekezo baada ya jana tu kuona matokeo. Matokeo haya ya mechi hii Mheshimiwa Rais mwenyewe ameifuatilia mwanzo-mwisho kwa sababu ni mapenzi yake kuona Taifa lake linapiga hatua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yake amesema, vijana hawa wote walioonesha uwezo mkubwa na kuhakikisha kwamba wanaibeba bendera ya Taifa kwa kuitoa Egypt na kwenda Jumanne kucheza na timu ya Senegal watakapomaliza *AFCON* ya mwaka 2027, anataka vijana hawa wote wawekwe kambi kwa ajili ya maandalizi ya Tanzania kushiriki *World Cup* mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini yake ni kwamba vijana hawa ambao wameonesha uwezo na kwa kweli tunamuomba mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake juu ya Taifa letu kuhakikisha kwamba siku ya Jumanne tunabeba kombe na kuja hapa tukiwa washindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa kumalizia tu tunafahamu ya kwamba Bunge hili limeunga mkono Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia, nami ninaomba kutumia nafasi hii kuwaomba Wakuu wa Mikoa, siku ya Jumanne vijana hawa wa *Serengeti Boys* watakuwa wanacheza na timu ya Senegal. Basi kila mkoa kwa kuwaunga mkono tuweke *screen* kubwa kuangalia heshima inayojengwa na vijana wetu wa Kitanzania ikiwa ni sehemu ya kuweka hamasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja na kwa kweli tumepata…; Mheshimiwa Sanga amesema kuna wale mameneja uchwara, vijana hawa hawatakwenda kwa mameneja uchwara, vijana hawa wanaenda kwenye *sport academy* za kimataifa ikiwa katika mkakati wa kujenga heshima ya Taifa letu, maandalizi yetu ya kuingia *World Cup 2030. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu, ninaanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kusimama mbele ya Bunge Tukufu kwa ajili ya kutoa hoja hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninamshukuru Mheshimiwa Spika wetu pamoja na Katibu wa Bunge na *staff* wote baada ya kuipokea hoja hii usiku na kunipa fursa mbali ya kwamba kuna shughuli inaendelea leo ya Wizara ya Ardhi, lakini kwa uzito, kwa heshima na kwa malengo ya Taifa letu katika diplomasia ya michezo, wameona wanipe nafasi hii niwasilishe Azimio hili ili tuweze kuipongeza timu yetu ya vijana *under 17*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao hoja hii imechangiwa na takribani Waheshimiwa Wabunge saba, Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa

Sylivia Sigula, Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na Mheshimiwa Paul Christian Makonda. Ninawashukuru sana kwa michango yenu, ninashukuru sana kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea kwa ujumla, hoja hii ambayo nimeitoa; mosi, wengi wametambua mchango wa mwanamichezo namba moja Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya kwenye sekta ya michezo na imesababisha vijana wengi kuona kwamba michezo siyo suala la afya, siyo suala la kujifurahisha, lakini michezo ni ajira ambayo inawafanya vijana kujiajiri kupitia sekta ya michezo na kupata kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ku-*invest* kwenye michezo, ni Mheshimiwa Mbunge wa *term* ya nne, tulikuwa tukizungumza masuala ya *academy* kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo iko Tanga, leo ipo Kigamboni. Tulikuwa tunazungumzia uwekezaji kwenye timu za vijana, leo vilabu vyetu wana timu za vijana. Tulizungumzia kurudisha michezo shuleni, leo michezo imerudi shuleni na matokeo yake hawa ni watoto wa kawaida kutoka kwenye mikoa mbalimbali, kutoka kwenye familia maskini kabisa ambaye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita imeamua ku-*invest* kwenye michezo. Mosi, wakijua zaidi ya 70% ya Taifa hili ni vijana ambao wameamua kushiriki kwenye michezo ili ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anahitaji kuwatoa kina Cristian Ronaldo wengine kutoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anawataka kuwatoa akina Messi kutoka Tanzania, ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka kuwatoa kina Leo, kina Drogba kutoka Tanzania. Hii isingewezekana bila uwekezaji ambao umefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ndugu zangu, michezo huunganisha Taifa, michezo huweka watu pamoja. Nami ninakushukuru Mheshimiwa Waziri, jana umetoka kumteua kaka yangu Haji Manara nami ninampongeza kuwa Msemaji wa Timu zetu za Taifa, ninaamini huko aliko ameanza kazi kuwaunganisha Watanzania, kuwaomba Watanzania wote tuungane, tui-*support* timu yetu ya *Serengeti Boys* ili Jumanne tuweze kuchukua kombe na tukawapokee kwa bashasha kubwa *airport* wakilileta heshima ya kombe hili nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa anayoifanya. Wizara yako ni Wizara ya hekaheka, upele umepata mkunaji, Mheshimiwa Dkt. Samia amejua kumpanga mchezaji kwenye Wizara ya Michezo ambaye anaifanya kazi kubwa na sisi tutakupa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, uwekezaji huu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambao umesababisha si tu *Serengeti Boys* kuingia fainali na kufuzu michuano ya dunia mwaka huu, hivi tunavyozungumza *Tanzanite Queens* ya *under 20* imefuzu kwenda kushiriki michuano ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza timu yetu ya wanawake ya *Twiga Stars* mwaka huu itashiriki michuano ya *WAFCON*. Huu ni uwekezaji na ushuhuda tosha ya kwamba vijana wameona kwenye michezo kuna ajira. Ninawaomba Watanzania, michezo ni heshima ya nchi, michezo inalitangaza Taifa letu si tu kwenye diplomasia ya michezo, lakini vilevile kwenye diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Wenger anaizungumza Tanzania, aki-*post* kwenye *page* yake tu watu wengi wataiona *Serengeti Boys,* lakini watajua kuna mbuga namba moja duniani iliyopewa tuzo inaitwa Serengeti. Tutaongeza watalii kupitia michezo, tutaongeza wawekezaji kupitia michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Watanzania, tuungane, tuipe *support* timu yetu vijana wetu waweze kufanya vizuri kwenye

fainali, lakini vilevile waweze kufanya vizuri kwenye michuano inayokuja ya Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninachukua fursa kuipongeza Serikali, nimemsikia Mheshimiwa Waziri, wamesema wataandaa kambi mapema kwa ajili ya kuwaweka vijana hawa kuelekea kwenye michuano ya *World Cup*. Nami, kwa kumalizia, ninaamini Wizara ya Maliasili itakuwa imesikia, Serengeti itakuwa imesikia, vijana wameitangaza nchi, wametangaza utalii, wameitangaza Mbuga ya Serengeti, waseme jambo kwa vijana hawa ambao wameletea heshima kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na baada ya kusema hayo, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia. Ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana mtoa hoja, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni nitawahoji kuhusu Azimio la Bunge la kuwapongeza Timu ya Taifa ya Vijana wanaume chini ya umri wa miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa kufukuza fainali za *AFCON 2026* na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Vijana, chini ya umri wa miaka 17 mwaka 2026. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Azimio la Bunge la kuwapongeza Timu ya Taifa ya Vijana wanaume chini ya umri wa miaka 17 *Serengeti Boys* kwa kufukuza fainali za *AFCON 2026*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nami ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa

aliouweka katika sekta ya michezo. Tumeshuhudia, zimetajwa hapa *Twiga Stars, Serengeti Boys* na timu nyingine. Ni uwekezaji mkubwa, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii kubwa sana. *(Makofi)*

Hata hivyo, ninapongeza Wizara yetu ya Michezo chini ya Mheshimiwa Waziri Makonda, tunaamini makubwa zaidi yatakuja kutokea katika sekta hii ya michezo. Pia ninawapongeza vijana wetu hawa walioshinda na kuwaambia kila la kheri katika mchezo unayokuja, watuletee heshima katika nchi yetu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Hata hivyo, jambo moja ambalo nimelipenda Waheshimiwa Wabunge, ni hii kutumia majina ya hifadhi zetu kwenye timu zetu, inatangaza sana utalii wa Taifa letu. Kwa hiyo, ninadhani ni vizuri Wizara mkaangalia wakati mwingine kuwa na *Manyara Boys*, *Burigi Boys*, ni katika nia hiyo hiyo ya kutangaza utalii hapa nchini. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kabla ya majadiliano, tuna matangazo ya wageni walioko Bungeni.

Tunao wageni wengine sita wa Mheshimiwa Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi, marafiki zake na mpigakura wake kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waheshimiwa Madiwani, Wajumbe na wataalam kutoka Ruangwa, Mkoani Lindi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Fadhili, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ambao ni wanafunzi wenzake wa *postgraduate* Chuo cha Kodi cha jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari *New Vision* kutoka Mkoani Singida, karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 150 na walimu saba kutoka Shule ya Sekondari ya *Everlasting Academy* ya Misugusugu, Halmashauri ya Kibaha Mkoani Pwani, karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wanakwaya wanawake 51 wa Dayosisi ya Dodoma Usharika wa El-Shadai Mnadani na wanakwaya wa Ulanga Mkoani Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, tunao wadau wa sekta ya ardhi ambao wanajulikana kama *Gwamaka Construction Limited*, karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila ajiandae.

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali yote ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, lakini pia ninachukua nafasi hii kumshukuru sana

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ameyafanya katika Wizara hii ya Ardhi, ni kumteua kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Akwilapo pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Mmuya kuongoza hii Wizara na kwa hakika wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite katika mchango wangu; Mkoa wa Mtwara na Lindi katika upimaji wa ardhi tuna jumla ya wakulima kwa Mkoa wa Mtwara peke yake wakulima 333,543 ambayo jumla ya korosho zote zinazolimwa, hawa ni wakulima wa korosho wana ekari 2,336,830. Hata hivyo, kwa Mkoa wa Lindi ambako anatoka Mheshimiwa Naibu Waziri pia kuna jumla ya wakulima wa korosho, pia wakulima kutoka Wilaya ya Ruangwa 127,260 hawa wote wana jumla ya ekari 1,221,922.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa hesabu inayofanyika leo hii, Mkoa wa Mtwara na Lindi mashamba yaliyopimwa ni 0.01% ya mashamba yote na kaka yangu Mheshimiwa Akwilapo, ukitaka kuacha *legacy* katika Wizara hii, twende tukapime mashamba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara, Lindi na wananchi wa mikoa yote ambayo wanalima korosho, wanaolima pamba, wanaolima tumbaku, tuanze na kwenye korosho kama *pilot study*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa korosho, ekari moja inaweza kupimwa kwa shilingi 80,000 na hii shilingi 80,000 kwa ekari hizo 2,336,000 tunaweza kupata jumla ya fedha shilingi bilioni 186. Serikali isitoe hata shilingi kwenye upimaji huu, sisi wenyewe wakulima wa korosho tutachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachotaka kitu kimoja tu hapa Mheshimiwa Waziri, tuanze na wilaya moja na mfano mzuri tuanze na Wilaya ya Newala, tuanze na Jimbo la Newala Vijijini. Sisi wananchi wa Newala Vijijini jumla ya ekari ambazo tunazo ni ekari 496,170. Tukizidisha mara shilingi 80,000, maana yake tutahitaji shilingi bilioni 39 kupima mashamba yetu yote, hizo fedha sisi tunazo. Hata hivyo,

wewe umebarikiwa, una Kamishna Mkuu mzuri sana kaka yangu Mathew, anaweza kuifanya hii kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wenyewe wananchi tutachangia na tukiweza kuchangia kupima mashamba yetu yote, maana yake tunaenda kumsaidia mwananchi wa Mkoa wa Lindi, Mtwara na mikoa yote inayolima korosho. Kwanza watakuwa na ulinzi wa kisheria wa maeneo yao na urahisi wa kupata mikopo, pia thamani ya mashamba yao yanaenda kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, la mwisho uhamisho salama wa miliki zao, na hapa wewe ndiyo unaenda kutengeneza historia, tukianza kupima mashamba yote ya mikorosho, tutawasaidia wananchi kwanza kupata *mortgage*, lakini ile falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia ya Dira 2050 ya kila mwananchi ikifika ya mwaka 2050 apate dola za Marekani 7,000, sisi wananchi tunaolima mazao ya korosho, ninataka nikuambie tukipima mashamba yetu, tunahitaji miaka mitano tu kufikia *this target*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakuomba kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Akwilapo, unapokuja kuleta hitimisho, tuanze sasa kupima mashamba ya mikorosho ili tuwasaidie hawa wananchi, wamekaa na yale mashamba, lakini hayapimwi. Hata hivyo, na wewe una nguvu, kazi nzuri sana, una timu mzuri sana, na Mathew ambaye ni Kamishna Mkuu anaweza kuifanya hii kazi *in a proper way* na wala msianzie Masasi usije ukapata shida, twende tukaanzie Newala Vijijini. Nami nitahamasisha wananchi wangu wote na wameshakubali kila shamba ekari moja ikipimwa shilingi 80,000, kwa hakika tutapima ekari zote 400,000 tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, faida ya kupima haya mashamba ikoje, sisi tukishapima kuna kitu kinaitwa *Certificate of Customary of Occupancy* ambayo hizi ni hati zinazotolewa katika vijiji. Tukisema tu kila kijiji kimoja tuweze kutoa shilingi 5,000 tunaweza kupata shilingi bilioni 11 kwa mkoa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake tunaweza kutengeneza matundu ya vyoo 6,400 bila kutegemea hela za Serikali, lakini kwa

Newala Vijijini tunaweza kutengeneza matundu ya vyoo 1,378 bila kutegemea hela za Serikali sisi wenyewe na tunaweza kutengeneza madarasa 100 ambayo kwa miaka mitano naweza kujenga shule zote za msingi katika Jimbo langu la Newala Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri akija atuambie na atuletee mkakati mzuri wa kuhakikisha haya maeneo yanapimwa ili tuongeze thamani na tuwasaidie hawa wananchi wa korosho, wakiwemo wananchi kutoka Masasi na ikifanikiwa hivyo basi tutaenda kwenye mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ambalo ningependa kuchangia sasa ni muda muafaka wa kupima makao makuu ya halmashauri zetu *especially* hizi halmashauri kuu mpya. Sisi katika halmashauri yetu ya Newala Vijijini sasa Mji wa Kitangari na maeneo mengine yote tuletee mpango tukaanze kupima ili wananchi wale wasikae kiholela na faida za kupima yale maeneo zinajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatengeneza thamani ya miji yetu, lakini *accessibility* itakuwa nzuri, lakini kuwepo kwa huduma za kijamii. Sasa naomba unapokuja kuleta hitimisho basi utuletee mkakati wa kupima makao makuu za halmashauri mpya ili sasa hii miji ikatengenezwe vizuri, lakini ukianza na Newala Vijijini na Jimbo letu Newala Vijijini katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala pale Kitangari itafurahisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri mimi ningechangia kwenye *concept* moja ni nzuri sana ya *Affordable Housing Act,* tuanzishe huu mpango wa *Affordable Housing Act* itatusaidia sana *NHC* kupata fedha za kutosha kuanza kujenga nyumba katika halmashauri zote, kwa sababu tutaweka sheria, Serikali itatoa fedha, itatafuta vyanzo vya fedha na mwisho wa siku tutakuwa tumewasaidia wananchi na wafanyakazi *especially* vijana *Gen Z*. Tutakuja na mpango mzuri na mwisho wa siku tutawasaidia sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nikupongeze wewe binafsi kwa kazi nzuri na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa orodha ni ndefu sasa ni dakika tano, tano. Kila mmoja atumie dakika zake tano vizuri, orodha bado ndefu sana.

Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila ajiandae.

MHE. MARIAM A. MUNGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Tarehe 01 Julai, 2026 Bunge hili ndiyo litakuwa Bunge la kwanza kushuhudia Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ikianza kazi rasmi. Katika Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa kumeainishwa nguzo tisa ambazo zitaifanya Dira yetu itekelezeke na moja ya nguzo hizo ni sekta ya ujenzi pamoja na mali zisizohamishika ikimaanisha kwamba ni makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Dira yetu imeeleza kwamba kuna upungufu wa nyumba milioni 3.8 kwa mwaka huu na zinaendelea, upungufu huu unaendelea kukua kwa kila mwaka mpaka hapo tutakapofikia mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hapa tunapoongea sasa kwa bahati mbaya sana nchi yetu haina Sera ya Nyumba. Tuna Sera ya Ardhi lakini vilevile, kuna Sera ya Makazi ambazo zinatumika kama Sera ya Nyumba hapa na pale. Kwa bahati mbaya sana sasa ili Dira yetu iweze kutekelezeka kiufasaha na kwa umakini zaidi tunahitaji kuwa na Sera ya Nyumba ambayo hatuna mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere mwaka 1962 baada ya kupata uhuru alianzisha Shirika la Nyumba la Taifa kwa madhumuni ya kuchangia katika kuleta makazi ya bei rahisi kwa Watanzania, kwa sababu ndiyo tulikuwa tunatoka katika kupata uhuru, kwa hiyo watu wengi walikuwa hawana makazi mazuri na makazi rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kutumika kama ndiyo shirika linaloweza kutoa makazi haya.

Baada ya muda kwenda mwaka 2005 Shirika la Nyumba la Taifa lililetewa sheria ambayo iliruhusu kujiendesha kibiashara. Kwa hiyo, tunavyoongea sasa hivi tuna *gap*, kuna *gap* au *vacuum* ya taasisi au upatikanaji wa nyumba hizi za bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu jukumu hili linaweza likachukuliwa, linachukuliwa na Shirika la Nyumba la Taifa peke yake lakini nchi nzima tuna uhaba wa nyumba milioni 3.8 mpaka sasa. Uhaba huu unaendelea kukua. Kwa hiyo, jukumu hili ni kubwa sana kuchukuliwa na Shirika moja la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapokuwa na Sera ya Nyumba itawezesha na mashirika mengine au taasisi binafsi, wajenzi wengine kuingia katika kuchangia, ku-*provide* au kuleta suluhisho la kuwa nyumba nyingi. Kwa hiyo, hii itatusaidia zaidi katika kuongeza idadi ya nyumba ambazo tunazihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuna tatizo kwamba miji yetu inakua kwa haraka na kwa nchi yetu hili siyo tatizo, ni neema tunaweza tukasema kwamba nchi yetu inakua kwa haraka na Watanzania tunaongezeka kwa wingi, lakini sasa jinsi *population* inavyokua na hili tatizo la uhaba wa nyumba nalo ndiyo tunazidi kwenda nalo. Tumetokanalo tangu enzi za uhuru mpaka sasa na litazidi kuongezeka tusipochukua hatua za haraka za kulifanyia kazi. Bunge hili, ndiyo Bunge litakaloshuhudia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa kwa miaka yake mitano ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa nina ombi; tunaomba Wizara yetu ya Ardhi ituletee...; Mheshimiwa Waziri anapokuja kwenye kuhitimisha atuletee ahadi au kusema kwamba hii Sera ya Nyumba siyo Sera ya Ardhi. Kuna tofauti katika Sera ya Nyumba na Sera ya Ardhi. Atuletee ahadi kwamba ni lini sasa Wizara yake itakuwa tayari imeandaa hii Sera ya Ardhi ili Bunge hili liweze kupitisha sheria ya nyumba ambayo itarahisisha utekelezaji wa Dira yetu na vilevile itakuza upatikanaji wa makazi ya bei rahisi au bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam ahsante sana.

MHE. MARIAM A. MUNGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hii hoja ya Wizara ya Ardhi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima. Nimesimama hapa na mimi nikiwa mwenye afya tele kuweza kuchangia na kushauri mambo mbalimbali katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya na hususan kwenye Wizara hii ambayo imekuwa na changamoto nyingi sana. Amepambana kuhakikisha kwamba angalau changamoto hizi zinapungua na kuweza kuwapa Watanzania na wananchi wetu tabasamu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba sana nimpongeze Kamishna Mathew, Kamishna huyu amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri sana, amekuwa akipambana hadi huko *field,* kazi yoyote ama changamoto yoyote utakayomweleza Kamishna Mathew amekuwa akiifuatilia na kuifanyia kazi kwa karibu hata mwenyewe kufikia hatua ya kufika *site* ili kuweza kujionea hali halisi. Mimi ninampongeza kwa moyo wa dhati na ninajua kazi yake anayoifanya, lakini tuendelee kumtia moyo kwa sababu kazi ni ngumu huko chini, changamoto bado ziko kedekede.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze *DG* wa *National Housing* kwa kazi kubwa anayofanya. Leo hapa ninapozungumza

pale kwangu Tabora kuna eneo lilikuwa linaitwa changamoto limekwenda kuwa eneo ambalo kwa kweli limeleta mabadaliko makubwa katika Mji wa Tabora na sasa hivi pale panajengwa jengo kubwa la *National Housing* ambalo litakuwa ni jengo la kitega uchumi kwa ajili ya *frame* pamoja na nyumba za kuishi watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimpongeze sana *DG* wa *National Housing* kwa kazi kubwa. Niseme endeleeni tu jamani, jengo lile liishe angalau mpaka *by* mwezi wa ngapi mambo yaweze kuwa mazuri na watu waweze kutumia jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nishauri mambo kadhaa na hususani nijielekeze zaidi kwenye Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi. Bahati nzuri sana mimi nimekuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Ardhi, na Maliasili, jambo hili siyo jambo geni sana watu wanalizungumza, wanalisema lakini tumeshauri sana kwenye Bunge hili. Laiti kama Wizara ingekuwa inatekeleza maelekezo ama mawazo ya Wabunge leo hapa tungekuwa hatuzungumzi suala la Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Hapa tunapozungumza ni katika vijiji 12,000 *plus* ni vijiji 2,000 *plus* tu ndivyo ambavyo vimepangiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda ama tunapiga *mark time* pale tulipo. Tumeshauri, tumesisitiza lakini na leo naomba nishauri na Serikali iko hapa, niombe sana hii Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi iondoeni huku ipelekeni kwa Mheshimiwa Kitila kule ndiko kwenye mipango, pengine kule mipango hii ya kuhakikisha kwamba watu wanapangiwa na kutengenezewa matumizi bora ya ardhi yanaweza yakafanyika vizuri kwa sababu ndiko kwenye mipango yenyewe, huku yawezekana kabisa fedha ndiyo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe utakuwa shahidi umekuwepo Bunge la Kumi na Mbili, tunapanga bajeti, tunapitisha hapa shilingi bilioni 1.5 labda inakwenda kupelekwa shilingi milioni 400, shilingi milioni 500 unapima vijiji vingapi? Unapanga vijiji vingapi? Kwa hiyo, bado tunaendelea kupiga *mark time* hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendelee kushauri hapa tutapiga kelele kila siku kuhusu tume hii, kama hatutafanya mageuzi makubwa kwenye tume hii basi itakua ni historia vijiji kwenda kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili jambo linaitwa Kliniki ya Ardhi, hakuna eneo ambalo linaleta migogoro kwa wananchi kama eneo hili la Kliniki ya Ardhi. Kliniki ya Ardhi tunajua ni darasa, darasa ambalo litakwenda kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na masuala mazima ya migogoro ya ardhi na mambo mengine yanayohusiana na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili Mheshimiwa Waziri naomba ulijue pale wanapofika kwenye hizi kliniki ndiyo kumekuwa kunaleta migogoro ya hali ya juu. Unakwenda kwenye kliniki unaenda kutoa hati kweli? Kwangu mimi Tabora nimefanya mkutano mmoja tu na wananchi kero za ardhi zaidi ya 15 na sasa hivi ninavyozungumza na wewe kero nyingine mbichi ziko pale ofisini kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anauziwa ardhi anaambiwa na mtu mwingine hii ardhi ni ya kwangu, hii ardhi ni hivi, changamoto ni nyingi kuliko tunavyofikiria, hii Kliniki ya Ardhi kuna mtu alisema hapa kwamba kesho mtaita sasa badala ya Kliniki ya Ardhi mtaomba Hospitali ya Ardhi, ndiyo tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama kliniki inashindakana, inaenda kuleta matatizo makubwa zaidi, tutakweda kuomba hospitali ili matatizo haya yaweze kutatuliwa. Mimi nimekuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa vipindi viwili, hakuna kipindi ambacho nakutana na changamoto za ardhi zinazotia aibu kama kipindi nimekuwa Mbunge wa Jimbo na ni palepale kwangu Tabora Mjini.

Mheshimiwa Waziri twende *site* ukaone huko watu wanavyolia, twende *site* ukatusaidie, twende *site* utuondolee miiba kwenye njia zetu tuweze kupita salama ili na wewe uweze kuendelea kuwa salama, kwa sababu hali ni mbaya ya ardhi kuliko tunavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mifumo, kuna mfumo lakini huu mfumo uko Dar es Salaam, uko Dodoma, uko na Arusha; kati ya mikoa

26 ni mikoa mitatu peke yake ndiyo huu mfumo upo, huku kwingine kunatumika nini? Bado Wizara imeendelea kuleta mifumo mingine tofati tofauti inazidi kuwachanganya wananchi wetu, inafanya wananchi wasielewe upi ni mfumo sahihi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alishasema kwamba jamani mfumo uwe mmoja, mifumo ikiwa mingi inapoteza hata hao wananchi. Hii mifumo ndiyo inaleta rushwa, ndiyo inaleta watu kudhulumiwa ardhi zao, ndiyo inaleta kila aina ya changamoto katika Taifa letu na nchi yetu kwa ujumla kwenye Wizara hii…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza na mimi niipongeze Wizara ya Ardhi kwa hotuba nzuri ya bajeti, lakini ninayo tu mambo machache ya kuweza kushauri. Wizara ya Ardhi, Kitengo chetu cha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, hapa bado tunahitaji kuweka jitihada ya makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo letu la Msalala lenye *square kilometer* 3,400 ni *square kilometer* 1.5 peke yake ndiyo imepimwa, lakini eneo hili linafaa kwa matumizi ya kilimo, linafaa kwa matumizi ya mifugo, linafaa kwa uchimbaji kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto tunayoipitia sisi sasa hivi Wizara ya Ardhi haina mawasiliano na Wizara ya Madini. Sehemu ambayo ina leseni ya uchimbaji kuna viwanja vya makazi. Kwa hiyo, unaona kabisa changamoto ambayo tunapitia pale sehemu ambayo inafaa kwa ajili ya mifugo hapajatengwa kwa ajili ya mifugo, sehemu ambayo inafaa kwa ajili ya mabonde ya kilimo hapajaainishwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira haya tunawachelewesha Watanzania wenzetu kutajirika kwa kutokupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu. Tunakosa mashamba makubwa ya kilimo chenye tija kwa sababu ya ardhi kutokupangwa. Tunakosa migodi mikubwa ambayo wawekezaji wangeweza kufika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbaji na mipango kwa ajili ya uchimbaji na kusiwe na migogoro yoyote kwa maana hakuna makazi maeneo hayo yametengwa maalumu kwa ajili ya shughuli za uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa kuvutia wawekezaji, wawekezaji wanaona kuwekeza kwenye maeneo hayo ni gharama kwa sababu tunakwenda kulipa fidia watu wengi ambao wangeweza kupangwa kwenye maeneo mengine na maeneo hayo yakaachwa wazi kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inakusanya kodi ya ardhi, tungeweza kusema kodi ya ardhi ya mwaka mmoja tu irudi ikaweze kupanga miji yetu, tutapiga hatua kubwa mno. Halmashauri ya Msalala peke yake mpaka sasa tumekusanya shilingi milioni 290 kwenye kodi ya ardhi na ukumbuke halmashauri hii bado ni vijijini; je, halmashauri za mjini zimekusanya shilingi ngapi?

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mabula, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

TAARIFA

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji tatizo lililoko Halmashauri ya Msalala ni tatizo pia lililopo katika Halmashauri ya Ushetu, maeneo makubwa hayajapimwa, lakini bado kuna mgogoro kati ya Hifadhi ya Msitu wa Kigosi na *Usumbwa Forests Reserve,* mpaka wake pia ni mgogoro ambao tulishaufikisha Wizara ya Ardhi, lakini bado hatujapatiwa majibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, unaipokea hiyo Taarifa?

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa ya kaka yangu Mheshimiwa Cherehani, ninaomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linaitia gharama hata Serikali kwa ujumla, maeneo ambayo hatukupaswa tupeleke barabara za lami, hatukupaswa tukajenge madaraja kama ni maeneo ya kilimo tunalazimika kupeleka miundombinu hiyo kwa sababu wananchi wameenda kuishi wanavyochagua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo nguzo za umeme zinafuata kaya tano kwa sababu wananchi hatujapanga matumizi bora ya ardhi. Kuna maeneo tunalazimika leo hii, ni kwa sababu gani miji yetu hata hapa Dodoma tu, miji yetu imejengwa kutazama *highway* ni kwa sababu gani leo hii mtoto anagongwa na gari akienda shuleni? Anavuka barabara ya *highway,* kwa sababu gani, unaendesha gari kwenye *highway* unagonga ng'ombe? Hii yote ni matumizi ya mipango mibovu ya matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miji yetu ingeweza kutizama upande mwingine, *highway* kusingekuwa na matuta, kusingekuwa na alama za *zebra*, lakini kwa sababu tunajichanganya wenyewe, tunajenga shule huku, watoto wavuke upande huu, waende wakasome huku, kwa hiyo, watoto wanagongwa na magari. Matumizi bora ya ardhi

yatatuokoa na tunawategemea sana Wizara ya Ardhi waweze kutukomboa kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye migogoro ambayo inawezekana kwa asilimia kubwa imesababisha mpaka Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kunyang'anywa mihuri. Sisi kwetu kwenye majimbo, tunaotoka vijijini Usukumani, Mwenyekiti wa Kitongoji ana kazi nyingi zaidi ya kuuza ardhi. Mwenyekiti wa Kitongoji ndiye anayebaini, ndiye anayemtambua raia wa kitongoji hicho, muhuri wake unatumika kumwandikia barua mtu aende akapate *NIDA*, muhuri wake unatumika, kwa ajili ya kutoa kibali cha kwenda kuuza ng'ombe. Leo hii kule kwetu, tunapozungumza hatujui mtu anayeswaga ng'ombe amewaiba au ni wa kwake au ni mfanyabiashara, hatujui! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kitengo cha utambuzi kimeondolewa kwa sababu ya migogoro ya ardhi, ninaomba ikiwezekana litoke tamko, Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji wasihusike kuuza ardhi, ila waendelee na zoezi lao la utambuzi, tutatoa *NIDA* kwa wakimbizi! Watendaji wa Vijiji hawakai kwenye maeneo yao wanayofanyia kazi, hawajui mipaka ya maeneo yetu, hawamjui nani ana ng'ombe, nani ni mfanyabiashara, nani si mfanyabiashara wa ng'ombe! Watatoa vibali vya kuswaga ng'ombe kwa wezi. *(Makofi)*

(Hapa kengele Ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Hitimisha.

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Nimemtaja Mheshimiwa Cecilia Daniel Parreso, atafuatia Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika

hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ardhi. Naanza kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi mnayoendelea kuifanya. Ni ukweli kwamba ardhi tuliyonayo hapa nchini haiongezeki, lakini watu kwa maana ya Watanzania wanaongezeka na matumizi na mahitaji ya ardhi yanaendelea kuongezeka. Hata hivyo, ardhi hii tuliyonayo tukiitumia vizuri kwa kuipangilia ni chanzo muhimu na cha uhakika cha mapato ya Serikali na pia pato la mtu mmoja mmoja kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya, kama utangulizi, mchango wangu utajikita katika suala zima la Mabaraza ya Ardhi na Nyumba. Naanza kwa kueleza kidogo chimbuko la Mabaraza haya ya Ardhi na Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1991 Serikali iliunda tume ambayo iliongozwa na Profesa Issa Shivji. Pamoja na mambo mengine, tume hii ilikuja na mapendekezo ya namna ya kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi tuliyokuwanayo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tume hiyo ikapendekeza kwamba migogoro hii itoke kwenye mfumo rasmi wa kimahakama na ishughulikiwe na mabaraza, lakini pamoja na hayo, mapendekezo haya yalijikita katika nguzo kubwa tatu; moja, kuanzishwa kwa mabaraza kuanzia ngazi za kijiji, kata na wilaya, lakini pia kutenganishwa kwa hizo shughuli kutoka kwenye mfumo rasmi wa kimahakama kwenda kwenye mfumo wa mabaraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi au nguzo nyingine ulijikita zaidi katika usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Pamoja na haya yaliyotajwa, ndiyo ulikuwa msingi wa kuanzishwa kwa Sheria ya Ardhi, Namba 04 na Namba 05 ya mwaka 1999 ya masuala yote ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya kuanzisha mabaraza haya, kwanza ni kupunguza urasimu uliokuwepo wa utatuzi wa

migogoro ya ardhi au upatikanaji wa haki kwa watu ambao walikuwa na migogoro. Pia ilikuwa ni kutumia mfumo rahisi na shirikishi wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kuwa umiliki wa ardhi wa nchi hii ulikuwa unaendeshwa au kusimamiwa na mila na desturi za makabila mbalimbali hapa nchini. Pia kipindi hicho tulikuwa tuna uchache wa mahakama za mwanzo hivyo, kulikuwa kuna mlundikano na ucheleshwaji mkubwa wa haki pale ambapo wananchi walikuwa wana migogoro na ikawa ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kulikuwa kuna gharama kubwa ya uendeshaji wa kesi katika mahakama za kawaida, lakini pia iliwagharimu wananchi kuzitafuta au kuzifuata huduma katika Mahakama za Hakimu Mkazi, kwa maana ya Mahakama za Mikoa. Kwa hiyo, kwa uchache haya ndiyo malengo na makusudi ya kwa nini tulianzisha mabaraza haya kwa wananchi kipindi hicho cha mwaka 1991, chini ya Tume ya Profesa Issa Shivji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabaraza yalianzishwa, lakini hali ikoje kwa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa katika wilaya 139 tunayo mabaraza 118, bado wilaya 21 mpaka leo toka mwaka 1999 hazina Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Tafsiri yake ni kwamba bado kuna wilaya changamoto ya utatuzi wa migogoro ya ardhi imekuwa ni kero kwa sababu hakuna mabaraza haya. Hata hivyo, pamoja na kwamba kuna baadhi ya wilaya zina Mabaraza na Wenyeviti, lakini huduma zinazotolewa zimekuwa ni changamoto na kero kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wenyeviti ambao wanaendesha mabaraza hayo wako wachache na watumishi kwa ujumla. Mwenyekiti mmoja anaweza akahudumia wilaya mbili mpaka tatu jambo ambalo linafanya ucheleweshwaji mkubwa.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresso, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sigrada.

TAARIFA

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba nimpe Taarifa mchangiaji kwamba miongoni mwa mikoa ambayo haina hayo Mabaraza ni Mkoa wa Njombe wenye wilaya tano, lakini na Mwenyekiti wa Baraza ni mmoja na anazunguka mkoa mzima mpaka sasa. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresso, Taarifa unaipokea?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashindwa kuipokea, siipokei mpaka nifanye utafiti kujiridhisha haya anayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba mfano Wilaya yangu ya Karatu ninayotoka, pale tuna Mwenyekiti, lakini yule Mwenyekiti anaishi Arusha. Huduma anazitoa mara chache sana kwa wiki au kwa mwezi jambo ambalo ni kero. Mwenyekiti huyo huyo anaenda kuhudumia wilaya nyingine za jirani jambo ambalo limekuwa ni changamoto na ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa ya utoaji wa rushwa ili uweze kupata haki. Rushwa imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi. Tafsiri ni kwamba kwenye mabaraza haya mtu hataweza kupata haki yake mpaka atoe chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nini kifanyike au ushauri wangu kwa Serikali. Kwanza, ifanyike tathmini ya kina kuona kama malengo ya uanzishaji wa mabaraza haya yamefikiwa. Kwa maoni yangu hayajafikiwa. La pili, wakati tunaanzisha kipindi hicho, kulikuwa kuna makusudio; je, hali halisi ya sasa ikoje? Tunahitaji bado kuendelea nayo au sivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ushauri; kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Mahakama ndiyo chombo cha utoaji wa haki. Pale ambapo panatokea migogoro, maana yake ni kuna haki inatafutwa hivyo, masuala haya yarudishwe kwenye utaratibu wa kawaida wa

kimahakama ya utafutaji wa haki, tuondokane na mfumo wa utumiaji wa mabaraza haya katika migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando. Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule ajiandae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Wizara ambazo niliomba kuchangia zinaisha, lakini kila nikikaribia kuchangia ninaambiwa dakika tano, dakika sita, nimejiandaa kwa dakika 10, ninaambiwa dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninadhani siyo sawa, hata kama Kiti hakipingwi. Nilikuwa nimejiandaa kuchangia Wizara zote, kila nikisimama tu, jana, Bunge limeisha hapa muda wake... *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa changia, unapoteza muda.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ahsante, lakini ujumbe umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara ni Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, lakini kule Tarime inaitwa Wizara ya migogoro ya ardhi na makazi holela, kule Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi imetuchonganisha sana na wananchi na imejenga chuki na Serikali, imejenga chuki na chama, wananchi wanalalamika sana. Mheshimiwa Waziri mimi ni mwalimu wangu wa *chemistry* pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, umepewa mfupa mgumu na nitachangia hapa bila kumuangalia mtu usoni ili ujumbe ufike. Mheshimiwa Waziri, Wizara hii sio ya kuvaa suti na tai, hii Wizara ni ngumu, siyo Wizara ya kukaa humu ndani kwenye kiyoyozi *my brother.* Ni Wizara ya kwenda *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu jana nimesikiliza Wabunge wanasema umeahidi kwenda, haujaenda. Utamtuma Naibu Waziri, hajaenda. Nimekuandikia barua tarehe 20 Aprili Mheshimiwa Waziri, *file* hili hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo wananchi wamekaa, pale Kata ya Bumera, Kijiji cha Kwisarara, Kitongoji cha Bunyama; wamekaa tangu mwaka 1974, ni umri wangu hapa, mimi nimezaliwa mwaka 1974, lakini nimeenda *site* kwa gharama zangu. Waziri na Naibu Waziri wana magari ya Serikali, posho wanalipwa, mafuta hawaweki kwenda tu *site* kule. Watu wanauwana, huendi Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetoka hapa na gari langu *private,* nimeenda jimboni, nikafanya mkutano, nikakupa *clip* ya malalamiko. Mwenyekiti wa Kijiji aliyekuwepo kwa miaka hiyo anasema hakuitisha mkutano mkuu kutoa eneo ekari 351, kuna kaya 75 katika eneo hilo. Wameenda wananchi wamekaa, Serikali ya Kijiji imeandika barua, mpaka sasa hivi hata majibu hawajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimetangaza kule kwamba kwa kuwa kuna mtu anaenda kwenye Baraza la Ardhi anawaambia kwamba atawakamata wamevamia eneo. Tangu mwaka 1974 hati imetolewa mwezi wa Februari mwaka huu, wameongea huyu mtu anasema mwekezaji uchwara ameongea na Afisa Ardhi wa Wilaya, ameenda pale Musoma, akaja makao makuu, anayo hati kwenye begi anatembea nayo, sasa wananchi wote pale ni mateka. Nimewaambia hapa kila mtu ajilinde, mtu asiingie kwenye eneo lile mpaka Waziri aende, haki itendeke, atuambie yeye alipataje eneo?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Tarime Vijijini wamesikia na hiyo ndio kero kwa sababu, Waziri hajanisikiliza Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro mwingine pale ni watu wameuana kwa muda mrefu. Wanagombana, hawajengi, uhasama kwenda kuangalia mipaka tu. Mgogoro kati ya Tarime na Rorya watu wameshikiana mishale. Nimelalamika, nimeandika, hawasikilizwi. Mgogoro wa vijiji saba, Kata ya Kwihancha, Kata ya Girong'a,

Nyanungu, wameenda watu wa ardhi wanaweka *beacon* wenyewe bila wananchi kushirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara ni miongoni mwa Wizara ambazo Wabunge wangekuwa na akili kama ya kwangu na wangekuwa kama mimi, hii Wizara tungeiweka kando kwanza hii bajeti yake tujadili habari ya migogoro na Waziri atuoneshe kama kweli uwezo huo wa kwenda kutatua changamoto upo?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mnazungumza hapo, hivi inawezekanaje kwenye Baraza la Ardhi lile wanaenda, kwanza lazima watu wale wawili uwachangie gharama. Anayemdhulumu mwananchi wa kawaida maskini ni tajiri, huyu maskini hana pesa. Kigezo kimojawapo ni lazima kwanza mtoke muende *site*. Sasa yule mwenye nacho anatoa gharama, maskini hatoi. Hivyo, wakienda *site* unafikiri nani atapewa haki? Katika hiyo *scenario* nani atapewa haki pale? Maana yake ni watu wenye pesa. Mheshimiwa Waziri, ingekuwa mimi nimekalia hicho kiti, kwa muda ambao umekaa hapa, ningejaza magereza watu wa Ardhi, wengi sana pale kwa sababu hivi anatoaje hati mbili-mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, hati zipo kwenye mfumo, mimi nina hati yangu, ninalipia ardhi, unakuta kuna mtu amejenga eneo hilo na vibali anavyo. Yaani mimi nina *file* la ardhi hiyo hiyo na mwenzako ana *file* la ardhi hiyo hiyo! Sasa inaonekana nani amem-*time* mwenzake?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu sio mpango. Hii Wizara, Waheshimiwa Wabunge, tutachangia mwaka huu, mwaka ujao wakija na majibu na maelezo kama haya, tuwe na mtindo mwingine kwa sababu haiwezekani. Hivi ninyi mnaona furaha kukaa kwenye majumba, kwenye Bunge ambalo wananchi wanalalamika, wanalia. Maliasili kuna matatizo, Ardhi kuna matatizo, Mifugo kuna matatizo, Maji kuna matatizo, Madini kuna matatizo, TAMISEMI kuna matatizo! Hivi hamuoni kama kuna shida hapo Waheshimiwa Wabunge? Hamuoni kwamba kuna shida?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waliopo nje wanataka tutoe suluhu, kwa hiyo, Waziri inabidi ajipange kweli kweli. Mbunge analalamika eti Waziri asiende *site?* Ni kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wamepewa kazi na Mheshimiwa Rais, Rais hawezi kuelekeza cha kufanya. Wana miongozo, waende *site* watatue matatizo. Tujadili hoja bila kuangalia sura ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitashika shilingi, kama inakimbizwa-kimbizwa nitashika shilingi. Kwa kweli, sitaunga mkono hoja hizi mpaka nijue namna ambavyo suluhu inapatikana kwenye migogoro. Kata zote watu wanalalamika, sasa mimi ninaungaje mkono?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mudawa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waitara, muda wako umeisha. Ahsante. *(Makofi)*

Nilimtaja Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule. Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima ajiandae.

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, na mimi ninapenda kumshukuru Mungu aliyenipa afya na pumzi siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi anayoendelea kuifanya kututumikia kwenye nchi yetu. Mimi leo nina jambo moja tu ambalo linaweza kuniumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawapongeza sana Wizara ya Ardhi toka tulikotoka mpaka kufikia hapa. Sisi Mkoa wa Ruvuma hati tulikuwa tunachukulia Mbeya mara ya kwanza, baadaye tukachukulia Mtwara, lakini muda ulivyoenda tumefikia sehemu tunachukulia mkoani kwetu. Tumeletewa Kamishna pale na Msajili.

Ninawapongeza kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kufanyika, lakini kwenye mazuri hayakosi mabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tunatambua hati ndiyo maisha, hati ndiyo afya ya mtu, hati ndiyo *investment*. Mtu akiwa na hati anaweza kupata mtaji, lakini kwa sisi Mkoa wa Ruvuma tunapata taabu sana, wananchi wanapata taabu kupata hati. Tunatamani huu mfumo ambao wameuongelea Wabunge wengine ungeenda na kwetu Mkoa wa Ruvuma, lakini pale tumepewa kama *demo*, *Mbinga DC* pamoja na *Songea DC* wameanza kufanya huo mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo ungetusaidia sana kuepusha huu urasimu ambao hauna sababu kwa sababu kwa kutumia *analogue* inatusumbua sana kwenye suala la ardhi kupata hati. Unakuta watumishi ni wachache sana, lakini bado hawa wateule ni wachache, Tunduru unakuta mmoja, ukienda Songea Manispaa ni mmoja, ukienda Mbinga mmoja, kwingine hakuna, Madaba hakuna, lakini inatakiwa huyo huyo ndiyo aidhinishe kila kitu kwenye halmashauri. Kwa hiyo, akiumwa na ofisi imesimama, hati hazitoki. Ikitokea amelazwa hati haitoki, akiwa na tabia zake zile ngumu za kuringa, maana yake na sisi wote tunamngoja yeye. Watumishi ni wachache hii Wizara, tunaomba sana mjitahidi kutuongezea watu. Mteule kwa nini awe mmoja na anatuhudumia wananchi 300,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumekuwa na muamko mkubwa kwa sababu hati inatumika benki. Kila mmoja anatamani kuwa na kiwanja, anatamani kuwa na nyumba, angalau hela yake ataishika kwenye hati na atafainyia kazi, benki zitatusaidia, lakini utoaji wa hati ni mgumu, ni mgumu. Tunaomba sana, wakati mfumo unaendelea kutengenezwa/kutekelezwa mfumo huu wa *electronic*, basi tunaomba sana miundombinu ipelekwe kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya watumishi wa halmashauri kwenye Idara ya Ardhi si waaminifu. Ukienda kwenye upande wa ramani mtu anaambiwa bado ramani, huwezi kupewa hati yako au kuanzishiwa kitu chako cha kiwanja hadi kuwe na ramani. Mchora ramani ni mmoja, wakati huo huo unakuta wengine wanaojitolea

wanaishi kwa *remote*. Hawezi kufanya kazi kulingana na ambavyo yeye anataka, labda bosi wake anamtuma kazi nyingine, kwa hiyo, hiyo ramani haitachorwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Ardhi Mkoa, kwa Kamishna na Msajili, pale kuna bwana kijiji anajitahidi sana. Ikifika hati mkoani haichelewi, kama itakavyochelewa huku chini. Tunaomba, kwa nini chini ichelewe na juu kule isichelewe? Yaani huku umefanyiwa *assessment,* umekadiriwa, umetoa pesa zote, lakini ukifika kupata hiyo hati kupelekwa mkoani inasumbua. Ikifika mkoani hutoi chochote, hati inatoka, yaani muda mfupi sana unakuwa umepata. Ninawashukuru sana watu wa mkoani wanatuhudumia bila kujali hadhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, hili suala la ramani. Ramani tunaomba, mimi ninashauri hapa, mkoa uandae bajeti na uhakikishe unafanya *research* ya ramani kila kata. Kwa sababu unafika unamwona mtu mmoja mwenye ramani anamtafuta; kule kwetu kuna mtu anaitwa Mzee Hyera; anatafutwa huyo Mzee Hyera kama fedha. Yeye ndiye anayeijua ramani ya mwaka fulani. Kwa nini wasifanye *research* wakajua ramani kuwa yetu ni hii? Hata kama ni mtumishi mpya, mgeni, akibonyeza *computer* ajue hii ramani ipo wapi, ninafanyaje ili mwananchi ahudumiwe, lakini mlolongo unakuwa mrefu. Kila mmoja kwa nafasi yake, kila mtu anaringa anavyotaka ilhali kitu hiki ni muhimu sana, mnatuumiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu kliniki. Kliniki ya Ardhi imekuwa tofauti kidogo kwenye mkoa wetu, sisi hatuna malalamiko sana. Tunaomba iongezewe bajeti kwa sababu kitu kinachotuumiza kwenye kliniki ya ardhi ndani ya wiki moja anatoa hati 300, lakini mtu mmoja mmoja anapata taabu miezi miwili hajapata hati. Kwa nini, ni kwa sababu siku ya kliniki inawezekana kutoa hati 300, lakini mtu mmoja mmoja hapati hiyo hati? Waongezewe bajeti, wapewe weledi, wafundishwe. Kwetu hamna kelele za kuzidi. Wizara iwape bajeti watu wa ardhi ili waende wakafanye hizo kazi. Kwa wiki hati 300 hadi 400 tutapunguza kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ajiandae.

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia kwenye Wizara hii nyeti kabisa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kabisa kwa kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kazi njema ambazo anafanya na hata kuweza kutuletea sasa Waziri mpya kabisa Dkt. Leonard, Naibu Waziri Kaspar Mmuya pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Anthony Sanga; pia tuna Naibu Katibu Mkuu Bi. Lucy, mwanamke. Kwa kweli tumefurahi sana kuweza kupata watendaji hawa ambao tunaamini kabisa wanaenda kutuvusha kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nimpongeze tena Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niwapongeze pia Marais waliopita kwa tendo hili kubwa sana la kutokuruhusu mahusiano yoyote au labda Jumuiya ya Afrika Mashariki au nchi zozote kuhusika na ardhi. Ardhi ni ya Watanzania na ardhi itabaki kuwa ya Watanzania kwa vizazi vyote. Sisi hatutaki mahusiano yoyote ya ardhi na nchi nyingine. Ardhi yetu bado ni kubwa na ardhi hii inatutosha sisi na tunaendelea kuifanyia maendelezo, ikiwepo kilimo, mbuga zetu za wanyama pamoja na makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niipongeze sana Wizara ya Ardhi kwa ajili ya Dodoma. Ni kweli kuwa tulikuwa na migogoro mingi sana tulipokuwa na *CDA,* lakini mpaka sasa hivi jiji limefanya kazi kubwa sana. Kwa kupitia kliniki ya ardhi wametatua migogoro mingi. Ni lazima tuseme ahsante na tutambue. Pia wame-*document* kila migogoro ipo kwenye *document*. Ukienda kutaja mgogoro wowote wana-*reference*

ya kwamba mgogoro huu uliwahi kufanyiwa kazi mahali fulani, bado mahali fulani utaisha. Pia wametenga viwanja kwa ajili ya watu wanaokwenda kupata *double allocation* wameweza kupewa viwanja na bado wanaendelea kutoa hivyo viwanja. Nipongeze jitihada hizi za Mkuu wangu wa Mkoa Rosemary Senyamule, DC wangu Alhaj Jabir Shekimweri pamoja na Mkurugenzi wa Jiji Dkt. Fred, wanaendelea kufanya kazi nzuri ili kumaliza migogoro ya Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nichangie mambo matatu; jambo la kwanza, umilikishaji wa ardhi kwa wanawake bado. Tumepewa takwimu hapa kwamba wamiliki wa ardhi mpaka sasa hivi walio na hati ni kama 26% tu. Kati ya hao wanawake waliomiliki ni 28% tu. Kuna ugumu gani kumilikisha wanawake ardhi? Je, ni mila zetu na desturi ndizo zinazotufunga wanawake wasimiliki ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitoe wito kwa Wizara yangu, huko vijijini kuna hati za kimila, wanawake wapewe usawa kwenye kumiliki. Kuna shida gani kusema heka hii moja itakuwa ya huyu mwanaume na heka hii nyingine itakuwa ya huyu mwanamke, ili wanawake nao wamiliki ardhi, waweze kukopesheka mikopo benki na taasisi za kifedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu inapunguza migogoro baada ya kinapotokea kifo. Kwenye mambo ya mirathi wanawake wananyanyasika sana. Wanawake wamilikishwe ardhi ili nao wawe na haki sawa kama Watanzania wengine. Hadi sasa hiyo 28% haitoshi, jitihada za dhati zifanyike ili kumilikisha wanawake ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; Wizara hii ni ya nyumba pia na makazi. Bado kuna nyumba nyingi za tembe, bado kuna nyumba nyingi zimejengwa kwa udongo, *full suit* udongo mpaka kwenye kuanzia nani, kwenye ukuta hadi paa. Wizara hii kama tumeweza kupata ruzuku ya mbolea ikaweza kutusaidia kwenye kilimo, tumepata ruzuku ya nishati safi imetusaidia kutunza mazingira, kwa nini tusipate pia ruzuku ya bati na *cement* ili watu hawa wajenge nyumba za viwango na nyumba ambazo zitaweza kustahimili mvua zinazoendelea nchini kwetu? Ni kwa sababu gani tuna madarasa mazuri, tuna vituo vya afya vizuri, lakini nyumba za wale

wanaozunguka hizo taasisi nzuri sana ni duni, kwa nini tusipate ruzuku? Mimi ninaomba tuje na mkakati huo au tuweze na sisi kupata ruzuku ya mabati ili kuboresha makazi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, mimi niiombe sana Wizara iendelee kumilikisha ardhi kwa watu wa vijijini. Hizi hati za kimila zitolewe tu bila kujali, zinasaidia angalau umiliki wa mtu ili wawekezaji wanapokuja wakute kuna mtu anamiliki hati na tusikubali kabisa kutoa ardhi yetu kwa wawekezaji, labda tuingie ubia na mwekezaji. Mwekezaji akiwekeza awe anampa na huyo mwananchi gharama au mapato yale anayopata ili mwananchi huyu asipoteze hati. Mwisho kabisa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaunga mkono hoja na ninaipongeza sana Wizara yangu ya Ardhi, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Neema Majule. Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga ajiandae.

MHE. RASHID M. MTIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na leo ku-*appear* katika Bunge lako Tukufu. Nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendelea kusimamia Serikali yetu na hasa katika Wizara hii muhimu sana ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza katika eneo moja tu ambalo ninaona kwamba tukienda anavyotaka na alivyopanga tutatatua matatizo makubwa yaliyopo kwenye Wizara hii; eneo la Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana tumeona ilivyotendewa haki na hata bajeti hii ambayo inakuja tunaona dhamira ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vyote vinapimwa baada ya miaka mitano. Jambo hili litaondoa migogoro ya ardhi kule vijijini, migogoro ya wakulima na wafugaji. Twende tukafanye ili tutekeleze maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa namna ninavyoona wanavyojipanga kufanya kazi. Tunawaona wanavyokimbizana kuangalia maeneo gani wanatatua matatizo au migogoro mikubwa ya ardhi katika nchi nzima. Tuendelee kuwapa nafasi na kuwa-*inform* katika maeneo mbalimbali. Ninaamini kwa namna nyoyo zao zilivyo na tunavyokaa nao kwenye Kamati, wanadhamira njema kabisa ya kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi inatatuliwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka nichangie eneo moja tu, nalo ni upangaji wa ardhi. Tumejipanga vizuri kwenye kupanga ardhi ya vijiji, lakini ninataka nisisitize kwenye kupanga ardhi ya miji. Ninasema hivi kwa nini; ni hali ya ukuaji wa miji tuliyokuwa nayo nchini. Tanzania kama nchi ipo kwenye *rank* ya juu kabisa ya ukuaji wa miji katika Afrika. Katika nchi sita za juu Tanzania ni ya sita. Tunatarajia inapofika mwaka 2050 nusu ya Watanzania watakaa mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Dar es Salaam ni jiji linalokua namba tano kati Afrika. Ukuaji huu ukiangalia kwa namna inavyokuwa mwaka hadi mwaka, Dar es Salaam na Tanzania unaenda kwenye nafasi ya juu kabisa ya ukuaji wa miji kutoka namba sita tulipo leo kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa *East Africa*, sisi Tanzania ndio tunaoongoza kwa kukua katika miji. Dar es Salaam katika *East Africa* ndilo jiji la kwanza kwa ukuaji; linakua kwa zaidi ya asilimia tano. Ukuaji huo ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba halmashauri zote ambazo zina makao makuu kwenye maeneo ambayo siyo maeneo yao ya utawala zihame.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio hili limekuza vijiji vyetu vingi kwenda kwenye miji. Kwa mfano tu maeneo ya Mkoa wa Mtwara, leo Halmashauri ya Newala imehamia kwenye eneo la Kitangali ambalo lilikuwa kijiji. Kwa upande wa Masasi, Wilaya ya Masasi imeenda Mbunyuni ambako kilikuwa kijiji. Sasa kwa Mkoa wa Mtwara tu vijiji vitatu vimebadilika kuwa miji kwa haraka kwa tamko hilo tu la Rais, je, nchi nzima tunavijiji vingapi? Kwa hiyo, tuombe tukapange miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme upangaji wa miji una faida kubwa kwenye nchi yetu. Unafaida kubwa, hii migogoro tunayoisema leo ya ardhi kama miji itapangwa na kupimwa, viwanja vitakuwepo, watu hawatagombania, tutaondoa migogoro...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. RASHID M. MTIMA: ... lakini ...

MWENYEKITI: Hitimisha Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. RASHID M. MTIMA: ..., tunaenda kuweka maeneo ya huduma. Tukipanga maeneo kama vile ya shule yanakuwepo. Kwa hiyo ni jambo ambalo linafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kusema sasa sisi watu wa Newala Mjini, mji wetu tunataka tuupange. Tunaomba Serikali itusaidie, itupe fedha. Tumeandika andiko tunalileta Wizarani, itupe fedha tulipange na Mbunge wao ni Afisa Mipango Miji. Kwa hiyo, tunahakika ya kuusimamia mji ule ukae vizuri na hizo fedha tutarejesha...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. RASHID M. MTIMA: ...nilirejesha hizo fedha nikiwa nafanya Tandahimba, zitarejeshwa nikiwa Mbunge pale Newala Mjini. Tunaomba mtupe fedha za KKK ili tupime mji ule, tuusimamie vizuri ili tuweze kusimamia miji yetu nchi nzima...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. RASHID M. MTIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga hoja mkono, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya Kiti tunaongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli iliyopo mbele yetu.

Nilimtaja Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Naibu Waziri Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, ajiandae.

Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nishukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu wa mawazo katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaenda kuchangia maeneo matatu; eneo la kwanza ni eneo la kliniki ya ardhi. Ni eneo ambalo limeonesha mafanikio makubwa sana katika Wizara yetu hii, hivyo tunatakiwa sisi Waheshimiwa Wabunge, tuone namna gani wanaweza wakaboresha huduma hii kwa sababu imeonesha inatatua matatizo kwa haraka na upatikanaji wa haraka wa hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kliniki ya ardhi limefanya vizuri sana katika mikoa mingi hususani Mkoa wetu wa Dar es Salaam katika upatikanaji wa hati. Mathalani, kwa miaka mitatu mfululizo imetatua migogoro zaidi ya 4,000 na pia imetoa hati zaidi ya 100,000 kiasi kwamba miaka ya nyuma huko idadi hii ilikuwa ni ngumu sana kuweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane kwamba kliniki ya ardhi inafanyika katika maeneo mengi, kwa maana ya kutoa elimu kwa

wananchi, inawasaidia kutatua migogoro ya papo kwa papo na pia inasaidia kusukuma upangaji na upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa haraka kwa sababu hili linakuwa *one stop centre* ya watumishi wote ambao wanakuwa wanatumika au kuhusika na upatikanaji wa hati. Hivyo, mimi ninapenda kuwapongeza sana Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna faida chache ambazo ninaweza nikazitaja, kwamba Serikali inaweza kukusanya mapato kirahisi kwa sababu wananchi wote wanakuwa wanafuata huduma na pia kunakuwa na makusanyo makubwa. Mathalani Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2024/2025 wameweza kukusanya shilingi bilioni 84 kati ya shilingi bilioni 89 ambayo walikuwa wamepangiwa kama sehemu ya lengo. Kwa hiyo, unaweza kuona namna gani mpango huu unaisaidia sana Serikali kuweza kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kubwa sana kwa Makamishina wote wa Ardhi pale Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na watumishi wenzao kwa namna wanavyojituma katika kushughulika na hizi kliniki za ardhi kwa kuzifanya mara kwa mara, kwa sababu wana utaratibu ambao wamejiwekea katika Mkoa wa Dar es Salaam kwamba kila baada ya miezi mitatu wanaenda kila halmashauri au kila manispaa. Kwa mfano Kigamboni walishafanya mwezi uliopita, mwezi wa tatu, wanaondoka pale wanaenda Temeke, Ubungo na sehemu zote. Kwa hiyo, kufanya hivi wanasaidia sana kupeleka huduma kwa wananchi, lakini pia Serikali inaweza kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa ninaomba pia kupitia Kiti chako, Wizara hii inahitaji kuangaliwa sana katika hii *angle* ya kliniki ya ardhi kwa maana ya kuiwekea fedha ambazo ziweze kutumika. Pia Wizara ya Fedha wasichukue fedha zao kama zile ambazo zinakuwa zinapelekwa kwenye Mfuko Mkuu kwa sababu ukichukua zile fedha hawa wanaendelea kupambana kutumia *own source* kiasi kwamba wanakuwa wanapata shida sana kwa maana ya kuweza kuendesha hizi shughuli. Sasa ili waweze kuwa na tija waachiwe hizi fedha, waweze kuzungusha na kufanya kwa faida na kuiletea Serikali mapato makubwa kama ambavyo inavyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kigamboni kwangu kuna changamoto tu mbalimbali za uvamizi wa maeneo. Maeneo mengi kwa sababu Kigamboni ni jimbo ambalo limekuwa linaendelea na linakua kwa kasi, lakini pia limekuwa na migogoro mingi sana ya ardhi ambayo nimshukuru sana Mheshimiwa Kamishna Mathew ambaye amekuwa akija mara kwa mara tunakaa na wananchi na kuweza kuangalia utatuzi wa ile migogoro, kwa maana ya kuhakikisha maslahi ya wananchi yanakuwepo, lakini pia Serikali inakuwa imefanya kazi yake vizuri. Ninampongeza sana Kamishna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kuzungumzia; mwenzangu aliyetoka kuzungumza hapa alikuwa anasema kwamba Dar es Salaam ni jiji la sita kwa kukua duniani, lakini pia ni jiji la kwanza kwa kukua *East Africa*. Mimi niombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake ya Makatibu Wakuu na viongozi wengine, watupie jicho Dar es Salaam. Dar es Salaam sasa hivi ilivyofikia imetapika, hakuna sehemu nyingine ya kujenga. Sehemu za kujenga zinazotakiwa zijengwe zina migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo ninataka nishauri kwamba watumie ile *world class planning mode* ambayo wenzetu wanatumia huko duniani kwa maana ya kwamba tubadilike, tutoke kwenye jiji, twende kwenye *Dar es Salaam Metropolitan Authority*. Tupanue lile jiji liwe kubwa. Mheshimiwa Waziri akilifanya hili katika wakati wake atakuwa umetengeneza *legacy* kubwa sana, kwa maana gani? Dar es Salaam inatakiwa sasa tuanze kuandaa miundombinu ya *metropole* kama zile ambazo tunaona maeneo mengine, kama vile Johannesburg na Dubai; wanatumia zile *metropole* na zile *metropole* zinaenda mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo nilikuwa ninatamani sana Wizara waje na mpango ambao utasaidia kupanua Dar es Salaam, itoke Dar es Salaam kwenda hadi Chalinze, itoke Dar es Salaam twende hadi Mkuranga, itoke Dar es Salaam iende hadi Mkuranga, itoke Dar es Salaam iende hadi Bagamoyo ili tupanue makazi ya watu. Kwa sababu Wizara ndio wenye nafasi ya kuweza kupanga na kumilikisha maeneo, tutakuwa tumeiweka ile *population* ya watu itakuwa imekaa vizuri, pia tumepunguza foleni ya watu Dar es

Salaam. Kwa sababu mtu anakuwa anakaa Chalinze anakuwa na uhakika wa kufika Dar es Salaam kwa nusu saa kwa sababu ya kutumia *metropole* ....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, ahsante.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sanga.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na kuchangia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa maelekezo ya kuhakikisha migogoro ya ardhi inatatuliwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha kliniki ya ardhi na hatimaye kutatua migogoro mingi ya ardhi nchini, lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yote ya Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia na kuanzisha mabaraza mapya yanayoshughulikia mashauri mbalimbali ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya kuendelea kushughulikia migogoro ya ardhi, ninaomba nijikite kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi na nitazungumzia zaidi Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali kuu ya maendeleo katika nchi yetu. Uzoefu mbalimbai unaonesha kuwa binadamu ndiye mtumiaji mkuu wa ardhi ambapo ukubwa wa ardhi hauongezeki bali

matumizi ndiyo yanaongezeka. Kama ilivyo katika maeneo mbalimbali ya nchi, ardhi ya Mkoa wa Lindi ambayo sehemu kubwa ina sifa ya vijiji inatumika zaidi kwa shughuli za uzalishaji kwenye kilimo, uvuvi, utalii na madini. Vilevile ina misitu ya asili, uhifadhi wa wanyama pori na uwindaji.

Aidha, ardhi hiyo imebarikiwa kuwa na gesi ya asilia ambayo inafaa kwa kupikia na kuendeshea magari na matumizi ya umeme nchini. Ardhi yetu ina fursa nzuri ya uwekezaji wa viwanda na bado haijatumika kwa wingi.

Mhesimiwa Naibu Spika, hivi karibuni matumizi ya ardhi ya Mkoa wa Lindi yameongezeka kutokana na kuongezeka kwa kasi ya mifugo. Tunashuhudia jamii ya wafugaji inahamasika kupeleka mifugo mingi Mkoa wa Lindi. Sababu zinazoelezwa ni kuwepo kwa malisho ya uhakika kutokana na ardhi yenye rutuba, uwepo wa vyanzo vingi vya mito isiyokauka, na mazingira bora ambayo hayashambulii wala kuathiri afya ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa ya kuchochea maendeleo yanayoonekana kwa Mkoa wa Lindi. Ninaishauri sasa Wizara itekeleze Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa Mkoa wa Lindi ili kuainisha maeneo mahsusi yatakayotumika kwa mifugo kwa kutenganisha shughuli za ufugaji na shughuli za kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna athari kubwa ya uharibifu wa ardhi endapo mifugo itaendelea kufugwa kiholela bila kuwa na utaratibu na maeneo mahsusi, ikiwemo uharibifu wa mazingira, ardhi kupoteza rutuba ya asili kwa matumizi ya kilimo, lakini athari mbaya zaidi ambayo inaendelea hadi hivi sasa ni kuwepo kwa migogoro ya wananchi hivyo kukosekana kwa amani baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba jukumu hili lisiachiwe halmashauri za wilaya bali Wizara hii ijikite kuainisha maeneo ya matumizi ya ufugaji sambamba na maeneo yatakayofaa kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata nyama, viwanda vya ngozi na

kadhalika, hii itasaidia kuchochea ukuaji wa uchumi kwa jamii, kwani ajira itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo ninaitakia utekelezaji mwema wa bajeti ya mwaka 2026/2027 nikiamini kwamba kwa umakini na umahiri wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ushauri huu utapokelewa kwa mikono miwili. Nawasilisha.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa inazoendelea kuzifanya katika kuimarisha sekta ya ardhi, upangaji wa miji na maendeleo ya makazi nchini. Hakika sekta hii ni uti wa mgongo wa maendeleo ya Taifa kwa sababu hakuna uwekezaji, kilimo, viwanda wala maendeleo ya wananchi yanayoweza kufanyika bila usimamizi bora wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali, bado kuna changamoto kubwa katika suala la upimaji wa ardhi na utoaji wa hati miliki hasa katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji yetu. Wananchi wengi bado wanamiliki ardhi kiholela bila hati rasmi jambo linalosababisha migogoro ya mara kwa mara na kuwanyima fursa ya kutumia ardhi yao kama dhamana ya kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi na utoaji wa hati kwa kutumia teknolojia za kisasa pamoja na kushirikisha sekta binafsi kwa ufanisi zaidi. Tukifanya hivyo tutapunguza migogoro ya ardhi, tutaongeza mapato ya Serikali na pia tutachochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni kuendelea kuongezeka kwa makazi holela katika miji yetu. Kasi ya ukuaji wa miji

haijaenda sambamba na mipango bora ya matumizi ya ardhi. Leo hii maeneo mengi yana upungufu wa barabara, mifereji ya maji, maeneo ya wazi na huduma muhimu za kijamii kutokana na ukuaji usio rasmi wa makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iongeze fedha za kupanga na kurasimisha makazi holela pamoja na kuandaa mipango kabambe ya miji inayozingatia ongezeko la watu na mahitaji ya baadaye. Tusipofanya hivyo leo, gharama ya kurekebisha miji yetu huko mbele itakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya ardhi bado linaumiza wananchi wengi nchini. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wananchi na wawekezaji pamoja na migogoro ya mipaka ya vijiji imeendelea kusababisha taharuki na wakati mwingine kuondoa amani katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara iimarishe Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuongeza watumishi, vitendea kazi na huduma za kisheria ili wananchi waweze kupata haki kwa haraka zaidi. Aidha, elimu kwa wananchi kuhusu sheria za ardhi iongezwe ili kupunguza migogoro inayotokana na kutokuelewa taratibu za umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la vijana na makazi. Vijana wengi wa Tanzania wana ndoto za kumiliki nyumba na viwanja lakini gharama zimekuwa kubwa mno kiasi cha kuwafanya wengi washindwe kufikia ndoto hizo. Naishauri Serikali kupitia Wizara hii kuanzisha programu maalum za viwanja na nyumba za gharama nafuu kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na taasisi za fedha. Hii itasaidia kuongeza ajira katika sekta ya ujenzi na kuwawezesha vijana kuwa sehemu ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia ya sasa ya teknolojia, bado wananchi wengi wanapata shida kupata huduma za ardhi kutokana na urasimu na ucheleweshaji wa mifumo. Naishauri Wizara kuendelea kuboresha mifumo ya kidijitali ili huduma zote za ardhi

zipatikane kwa uwazi, haraka na kwa gharama nafuu. Hii pia itasaidia kupunguza mianya ya rushwa na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba Serikali iongeze bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Sekta ya ardhi ni msingi wa maendeleo ya Taifa letu, hivyo ikipewa nguvu itasaidia kukuza uchumi, kuimarisha uwekezaji na kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kushiriki mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbele yetu kuna hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2026/2027, hotuba hii ni nzuri na nitumie fursa hii kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba yenye mwelekeo mzuri. Mheshimiwa Spika, Naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2026/2027 nikiangazia mambo kadhaa, hasa namna ya uandaaji wa mipango miji, ni wajibu wa Serikali kuwa na mipango miji yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inasema eneo la Masaki na Oysterbay ujenzi wowote utakaofanyika usizidi ghorofa nne, lakini kumekuwepo na baadhi ya watu wengine wamejenga ghorofa zaidi ya nne huku wengine wakikosa fursa hiyo, hali hii inapelekea wananchi kuona kuna *double standard,* aidha kwa mustakabali wa maendeleo na dunia ilipo sasa sheria hiyo ni ya kizamani ukizingatia maeneo hayo niliyoyataja ni maeneo mazuri kiuwekezaji na wawekezaji wananunua maeneo hayo kwa gharama kubwa, hivyo kumwambia mwekezaji ajenge ghorofa nne tu kunasababisha mwekezaji huyu kupata hasara kwani itamchukua muda mrefu kurejesha fedha zake alizowekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ibadilishe mfumo huu na watu wanaotaka kujenga wangepewa uhuru wajenge majengo marefu ya kisasa na kusiwe na *double standard,* Masaki na Oysterbay ni maeneo yanayohitaji majengo ya kisasa kiuwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tuhakikishe mipango yetu inakuwa madhubuti na ya kimkakati na kuendana na wakati wa sasa hasa kutenga maeneo maalum ya biashara na sio kuruhusu kila eneo mtu afanye anachotaka, kwa maeneo kama ya Mbweni ambayo kwa sasa ukuaji wake ni mkubwa, ni vema kuchukua tahadhari mapema kwa mamlaka husika kuzingatia mipango miji ya kisasa yenye taswira. Dar es Salaam na Dodoma ni miji miwili ya kimkakati zaidi nchini. Dar es Salaam ni kitovu cha biashara na bandari, Dodoma ni makao makuu ya nchi, lakini miji yote miwili inakabiliwa na msongamano wa ardhi, makazi yasiyo rasmi na changamoto za mipango miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka wa fedha 2026/2027, naziangazia changamoto na mapendekezo ya utekelezaji.

Kuhusu uhaba wa nyumba za gharama nafuu; Dar es Salaam ina upungufu wa nyumba zaidi ya 500,000. *NHC* imejenga nyumba nyingi, lakini nyingi ni za bei juu shilingi milioni 80 hadi 300. Mwalimu, askari na mhudumu wa afya hawawezi kumudu. Matokeo yake wanapanga Tandale kwa shilingi 200,000 chumba kimoja kisicho na choo cha ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Dodoma makao makuu ya nchi; tangu Serikali ihamie Dodoma bei ya kiwanja 20x20 Nzuguni, Ihumwa na Mkonze imepanda kutoka shilingi milioni mbili mwaka 2016 hadi shilingi milioni 25 kwa sasa. Wafanyabiashara wananunua viwanja vingi na kuvilaza wakiota faida. Mwalimu, daktari na polisi hawawezi kumudu kununua. Matokeo yake wanapanga mbali na maeneo ya kazi na wanachelewa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji Kampeni ya Kitaifa ya Urasimishaji, Wizara itenge fedha kwa ajili ya kurasimisha mitaa 200 ya

Dar es Salaam kwa mwaka 2026/2027. Kila mwananchi alipie shilingi 100,000 tu kupata Hati ya Hakimiliki ya Mazoea. Lengo ni kutoa hati 300,000. Hati hizi zitumike kukopa benki kuboresha nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Dodoma udhibiti wa bei ya ardhi na kufuta viwanja vilivyolala; Bunge litunge sheria ya kodi ya ardhi tupu. Mtu mwenye kiwanja zaidi ya miaka mitatu bila kukiendeleza alipe faini ya 5% ya thamani ya kiwanja kila mwaka. Hii itawafanya hao wanaomiliki viwanja hivyo ama wauze au wajenge kwa maana ya kuviendeleza. Pia Serikali ipange bei elekezi ya viwanja maeneo ya Nzuguni na Ihumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini ni lango kuu la kibiashara na uwekezaji, mipango miji na ardhi ni sehemu muhimu kimkakati. Wizara hii ndiyo msingi wa maendeleo yote. Bila hati miliki, hakuna mkopo benki, bila mipango miji, hakuna *TAMCO* itakayokua, bila makazi bora, hakuna nguvu kazi yenye afya. Kibaha Vijijini ni lango la Mkoa wa Pwani na tunashuhudia kasi ya ukuaji kutokana na *TAMCO, Expressway* na Bandari Kavu ya Kwala, lakini kasi hiyo inaleta msongamano wa ardhi na changamoto za makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuainisha mahitaji ya msingi ya Jimbo la Kibaha Vijijini katika sekta hii ya ardhi na makazi.

(a) Upimaji na umilikishaji wa ardhi; zaidi ya 70% ya wananchi bado wanamiliki ardhi kimila bila hati. Kata za Gwata, Bokomnemela na Dutumi zina mashamba makubwa ya wakulima wadogo wa muhogo, mpunga na korosho, lakini wakulima hawawezi kukopa benki kwa sababu hawana hati za hakimiliki ya kimila. Pia wawekezaji wanaokuja *TAMCO* wanataka maeneo ya viwanda vya malighafi Ruvu na Kwala, lakini wanakwama kwa migogoro ya mipaka. Mahitaji ya haraka ni kupima vijiji vyote na kutoa hati za hakimiliki ya kimila zisizopungua 15,000 kwa mwaka 2026/2027.

(b) Mipango ya matumizi ya ardhi na mipango miji; Mlandizi, Ruvu na Kwala zinakua kwa kasi sana. Mlandizi sasa ni mji mdogo lakini unakua bila mpango kabambe. Viwanda vidogo vinajengwa karibu na shule, nyumba za makazi zinajengwa kwenye njia za maji, na stendi

ya zamani imejaa. Tunahitaji *master plan* ya Mlandizi kutengwe eneo maalum la kibiashara, kujengwe jengo ambalo kutakuwa na *frame* za biashara na eneo hilo liwe kitovu cha biashara, watu wote wakitaka mahitaji muhimu wanakwenda hapo, hii itaondoa uholela wa kila eneo watu kufanya biashara na kupoteza taswira ya mji wetu, Ruvu Kijiji na Kwala inayobainisha maeneo ya viwanda, biashara, makazi, kilimo na hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunahitaji mpango kabambe wa maeneo ya jumla kwa vijiji vyote ili kutenganisha maeneo ya malisho, kilimo na makazi kupunguza migogoro.

(c) Nyumba za gharama nafuu kwa wafanyakazi wa *TAMCO* na walimu, wafanyakazi wa umma na wananchi wa kawaida; *TAMCO* ina ajira 853 na itaongezeka hadi 2,000 ifikapo mwaka 2027 kwa kuingia kwa Hyundai na Goodlife, lakini wafanyakazi wengi wanapanga Mlandizi kwa kodi kubwa ya shilingi 80,000 hadi shilingi 150,000 kwa chumba. Walimu wa Shule za Ruvu Sekondari na Mlandizi A nao wanakosa nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji Mradi wa Shirika la Nyumba *(NHC)* kujenga nyumba 500 za gharama nafuu Mlandizi na Kwala. Nyumba hizi zitapangishwa kwa shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000 kwa mwezi.

(d) Ofisi za Ardhi na huduma kusogeza karibu; wananchi wa Gwata wanalazimika kusafiri zaidi ya kilometa 45 hadi Ofisi ya Ardhi Kibaha Mjini. Mafaili kupotea, gharama za usafiri na urasimu unakithiri. Tunahitaji Ofisi ya Ardhi ya Wilaya Ndogo kufunguliwa Mlandizi. Ofisi hiyo iwe na huduma zote za upimaji, hati, uthamini na usajili.

(e) Hifadhi ya ardhi ya umma na maeneo ya wazi; kwa sababu ya kasi ya ujenzi, maeneo ya wazi, viwanja vya michezo na hifadhi za mazingira yanavamiwa, Mto Ruvu unaendelea kuvamiwa. Tunahitaji Wizara itamke wazi maeneo ya hifadhi na kuyapima ili kuyakinga na sheria kali zitumike kwa yeyote atakaekiuka ili iwe mfano kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tambua kazi kubwa inayofanywa na Serikali kwenye Wizara hii hasa kuhakikisha makazi bora, pamoja na masuala mazima ya ardhi, ila sisi watu wa Kibaha Vijijini tunazo changamoto kadhaa tunazokabiliana nazo, naomba Wizara wazitafutie ufumbuzi kwa upana wake na kuja na suluhisho la haraka, changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na wawekezaji; Kata za Dutumi na Bokomnemela zimeripoti migogoro mikali kati ya wakulima wa muhogo na wafugaji wanaohama Rufiji. Pia wawekezaji wanaotaka kununua ekari 500+ kwa kilimo cha kisasa wanashindwa kwa sababu mipaka ya kijiji na kijiji haijulikani. Mahakama ya Ardhi iko Kibaha Mjini na kesi zinachelewa miaka mitatu hadi mitano. Matokeo yake ni mapigano na kupoteza uzalishaji.

(b) Uvamizi wa ardhi na ujenzi holela; kwa sababu Mlandizi haina mpango kabambe, watu wanajenga kiholela. Njia za maji zimezibwa na ndio sababu Mlandizi inapata mafuriko kila mvua. Pia wawekezaji wa *TAMCO* wanalalamika kuwa wanapimiwa viwanja lakini majirani wanavivamia kabla ya ujenzi. Kamati za Ardhi za Vijiji hazina uwezo wa kudhibiti kwa sababu hazina ramani rasmi.

(c) Gharama kubwa za upimaji na hati; mwananchi wa kawaida anatakiwa kulipa kati ya shilingi 250,000 hadi shilingi 400,000 kupima kiwanja na kupata hati. Hii ni kubwa kwa mkulima wa kijijini. Matokeo yake wananchi nane kati ya 10 wanaamua kuendelea kumiliki kimila. Benki zinawakataa wakikopa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha korosho.

(d) Ucheleweshaji wa fidha kwa miradi ya maendeleo; Mradi wa *Expressway,* Bandari Kavu ya Kwala na upanuzi wa *TAMCO* yote yalihitaji wananchi kupisha mradi. Baadhi ya wananchi bado hawajalipwa fidia zao tangu mwaka 2024. Hii inajenga chuki kati ya wananchi na Serikali na inachelewesha miradi. Pia tathmini ya mali inafanywa bila mwananchi kushirikishwa ipasavyo.

(e) Ukosefu wa wataalam wa sekta ya ardhi ngazi ya kijiji; kila kijiji kinatakiwa kuwa na Kamati ya Ardhi ya Kijiji na Mtaalam wa Ardhi,

lakini Kibaha Vijijini tuna Maafisa Ardhi wanne tu kwa vijiji vyote ambao hawawezi kufika kila mahali. Matokeo yake, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yanatoa maamuzi yenye makosa na migogoro inaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri wangu wa kina kwa Serikali ifanye nini ili kuboresha sekta hii Jimbo la Kibaha Vijijini.

(a) Kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

(i) Zindua Operesheni Hati Kijiji 2026; tenga shilingi bilioni 1.8 kwa mwaka 2026/2027 kupima vijiji vyote vya Kibaha Vijijini na kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila 20,000. Ruzuku, gharama kwa wananchi walipie shilingi 50,000 tu badala ya shilingi 300,000.

(ii) Kamilisha mipango kabambe; maliza *master plan* ya Mlandizi, Ruvu na Kwala kabla ya Juni, 2027. Kataza ujenzi wowote mpya bila kibali cha Mipango Miji kuanzia Januari, 2027.

(iii) Jenga Ofisi ya Ardhi Mlandizi; Wizara itenge fedha kujenga na kuanza Ofisi ya Ardhi ya Wilaya Ndogo Mlandizi. Iwe na maafisa nane, gari moja na vifaa vya kisasa vya upimaji vya *GPS RTK*.

(iv) Nyumba za *NHC;* agiza *NHC* ianze mradi wa nyumba 500 za gharama nafuu Mlandizi na Kwala. Serikali itoe ardhi bure na *NHC* ijenga. Nyumba hizi zikodishwe kwa wafanyakazi wa *TAMCO* na walimu na watumishi wengine wa umma pamoja na wananchi wa kawaida.

(v) Serikali imalize malipo ya fidia; hakikisha wananchi wote waliopisha miradi ya *Expressway,* Kwala na *TAMCO* wamelipwa kabla ya Desemba, 2026. Unda dawati maalum la malalamiko Mlandizi ili kusaidia usikilizwaji wa malalamiko na Wizara iweze kuyapatia ufumbuzi.

(vi) Tupunguze siasa kwenye migogoro ya ardhi; ili ardhi iendelee kuwa bora ni lazima tukubaliane kupunguza siasa na kuwaachia watendaji wafanye kazi zao.

(vii) Boresha maslahi ya watumishi; ili kuepuka vitendo vya rushwa Serikali iboreshe maslahi ya watumishi kwenye sekta hii, kwa kuwapa *extra duty* itasaidia sana kupunguza rushwa na kusaidia utendaji wa kazi usiotia shaka.

(b) Kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani na Halmashauri ya Kibaha:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ajiri wataalam; ajiri Maafisa Ardhi 10, Maafisa Mipango Miji wanne, na Wapima sita ili kila kata iwe na afisa wake.

(ii) Kwa kushirikiana na Wizara, tenga maeneo ya wazi; halmashauri itamke na kupima maeneo yote ya wazi, viwanja vya michezo na hifadhi ya Mto Ruvu. Wavamizi wachukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho na onyo kwa wengine.

(iii) Baraza la Ardhi la Wilaya; anzisha Baraza la Ardhi la Wilaya linalokaa Mlandizi mara moja kwa mwezi kupunguza kesi zinazopelekwa Kibaha Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni uhai, kama hatutapanga vizuri sasa, miaka mitano ijayo Mlandizi itakuwa na msongamano usiopitika, wakulima watakuwa hawana mashamba na *TAMCO* itakosa ardhi ya kupanuka. Tukitekeleza ushauri huu, Kibaha Vijijini itakuwa mfano wa Tanzania ya Viwanda yenye mipango miji bora na wananchi wenye hati mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nichangie mambo machache kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji. Serikali ije na mpango madhubuti wa kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya wafugaji na wakulima ili kusiwe na mwingiliano wa matumizi na jambo hili lisimamiwe na ikiwezekana litungiwe sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna ujenzi holela, Serikali ije na mpango wa kutenganisha matumizi ya maeneo kwa mfano kuwe na eneo ambalo litaruhusu nyumba za kawaida *(bungalows)* na hapa haitaruhusiwa kujenga ghorofa, kuwe na eneo la kujenga ghorofa moja, vivyo hivyo na eneo la kujenga zaidi ya ghorofa moja. Sasa hivi maeneo ambayo yaliitwa *low density* kama Oysterbay yamegeuzwa kuwa maeneo ya *high density* kutokana na utitiri wa maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na *housing colour code* hasa kwenye majiji makubwa ili kupandisha hadhi maeneo. Aidha, kumekuwa na maombi ya kubadilisha matumizi ya ardhi na vibali vimekuwa vinatolewa. Niombe eneo hili pia liangaliwe kwa umakini maana sasa hivi katika mji wa Dar es Salaam kunajengwa *petrol stations* nyingi kwenye maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vinavyopimwa kwa sasa vizingatie kuacha maeneo mahsusi ya kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia kunapotokea migogoro ya watu kuvamia eneo la mtu ambalo tayari lina hati halali, basi Serikali ichukue hatua ya kumlinda mwenye hati halali, kwani kwa sasa wamiliki halali wamejikuta wakihangaika wenyewe mahakamani huku Wizara ikiwa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu Maafisa wa Ardhi ambao wanakuwa chanzo cha migogoro ya ardhi badala ya kuwahamisha toka kituo kimoja kwenda kituo kingine kwani huko ni kutoa ugonjwa eneo moja na kuuhamishia eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha wa Serikali huwa unaanza tarehe 01 Julai mpaka tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata, ninashauri hapa hata kwenye malipo ya kodi ya pango kanuni hii ifuatwe kama ambavyo walipa kodi wote wanavyolipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ije na mpango kujenga nyumba za bei nafuu kwa watu wa kawaida maana hizi zinazojengwa kwa sasa bado ni ghali sana hasa ukilinganisha na pato la watu wetu. Mpango uliopo haujawanufaisha wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe elimu juu ya matumizi ya nyaraka za ardhi. Mfano nini maana ya *town plan (TP),* je, *town plan* ni nyaraka inayompa mtu umiliki wa ardhi au ni nyaraka inayoelezea mpango mji maana kuna watu wanaamini *town plan (TP)* ni nyaraka ya umiliki wa eneo.

Pia Serikali iangalie upya Mabaraza ya Ardhi kwani kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu utendaji kazi wao na hasa yale ya kata. Aisha, Serikali iyalinde maeneo ambayo yalitengwa kwa madhumuni mahsusi mfano *open space,* maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma maalum mfano masoko. Kumekuwa na uvamizi wa maeneo haya au watumishi wa ardhi kuyamilikisha maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa mipango miji siku zijazo wanapotenga maeneo ya barabara wazingatie kuweka *provision* ya *lane* ya *ambulance* na magari ya Zimamoto maana tunaona jinsi ilivyo shida kwa *ambulance* kuwafikisha wagonjwa mahututi hospitalini au janga la moto linapotokea gari la Zimamoto kufika kwa wakati ni kipengele kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ije na mpango wa matumizi sahihi ya ardhi kwa kutenga maeneo yatakayotumika kama makazi, shule, hospitali, masoko, nyumba za ibada, nyumba za burudani, viwanja vya michezo na kadhalika, kwani ilivyo sasa unakuta baa iko katikati ya eneo la makazi, ili makosa yaliyofanyika huko nyuma yasijirudie, tujifunze kutoka kwa jirani zetu Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Dar es Salaam kama inawezekana *ambulance* na gari za Zimamoto kwa sasa ziruhusiwe kupita kwenye *lane* ya mwendokasi kunapotokea dharura ili kupunguza majanga maana kwa sasa haiwezekani kujenga hizo *lane* kutokana na ufinyu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yatakayotumika kama makaburi nayo yapangiliwe vizuri kwani kwa sasa maeneo hayo maziko hufanyika kiholela bila kuzingatia kuacha nafasi kuruhusu watu kupita wanapoenda mazikoni. Kuwekwe *distance* kati ya kaburi na kaburi ili kuruhusu watu wanapokuja kuzika waweze kupitisha majeneza kwa urahisi.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi mahiri na wenye maono uliowezesha mageuzi makubwa katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa sekta husika kwa kazi nzuri na maendeleo yakiwemo ya TEHAMA upande wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri ufuatao kwa Serikali :-

(i) Serikali kupitia Wizara itatue mgogoro wa muda mrefu wa mpaka kati ya Wilaya ya Muleba na Karagwe katika Kata za Rutoro na Rugera, Vijiji vya Rutoro na Omukakajinja, Vitongoji vya Rwamisha B na Kamzinzi.

(ii) Serikali iwezeshe usafiri wa ofisi za ardhi katika Halmashauri ya Muleba.

(iii) Serikali iwezeshe upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika visiwa vilivyopo Wilaya ya Muleba.

(iv) Maafisa Ardhi ajira zao ziwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ili wawajibike kiutendaji. Hii itafanya shughuli za

ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kupewa kipaumbele katika halmashauri. Ofisi za ardhi katika halmashauri ziwezeshwe zaidi ili ziongeze kasi ya kupanga na kupima ardhi.

(v) Mapitio ya sheria yafanyike ili madalali wa ardhi/mashamba/viwanja na *estate developers* wadhibitiwe kisheria.

(vi) *NHC* wajenge nyumba za gharama nafuu zaidi zinazoweza kununuliwa au kupangishwa na wananchi wa kima cha chini kama madereva wa bodaboda na mama ntilie. Kuna haja ya Serikali kufanya mapitio ya sheria au kuweka utaratibu wa kuwa na mradi wa *affordable houses* na *affordable houses fund.*

(vii) Serikali iendelee kuweka mifumo thabiti zaidi ya kudhibiti udanganyifu unaoleta migogoro ya ardhi. Maafisa wa Wizara wanaoshiriki katika vitendo vya uvunjaji wa sheria wawajibishwe. Udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi.

(viii) Serikali iweke madawati maalumu ya wanawake wajane, walemavu na wazee katika halmashauri ya kutoa huduma za ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi.

(ix) Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya na Kata yavunjwe na utaratibu wa mahakama utumike kwa kuwa yamekuwa hayafuati taratibu za kutatua migogoro

(x) Serikali iongeze kasi ya uhuishaji wa kumbukumbu za ardhi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi 500,000. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, kumbukumbu za ardhi 146,345 zimehuishwa.

(xi) Serikali iongeze kasi ya uandaaji na usajili wa hati na nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi kwa wananchi na taasisi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Ardhi, Nyumba

na Maendeleo ya Makazi ilipanga kuandaa na kusajili hatimiliki 500,000 na hati za hakimiliki ya kimila 520,000. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara ilikuwa imeandaa na kusajili hatimiliki 107,683 sawa na asilimia 21.54 ya lengo; hati za hakimiliki ya kimila 99,762 sawa na asilimia 19.19 ya lengo.

(xii) Serikali iongeze kasi kutoa huduma za uthamini na usajili wa nyaraka zinatolewa kupitia Mfumo wa *e-Ardhi* nchi nzima.

(xiii) Serikali ifanyie kazi na kuondokana na uwepo wa mitaa mingi ambayo imeendelezwa bila kupangwa na kupimwa.

(xiv) Serikali ifanyie uwepo wa *trading centers* nyingi ambazo zinahitaji kutangazwa, kupangwa, kupimwa na kumilikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwa Rais wa maono kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mapenzi makubwa naipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hasa Waziri Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kaspar Mmuya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia Katibu Mkuu *Engineer* Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu wake pamoja na watumishi wote walioko chini yao. Nina matumaini ya mapinduzi makubwa katika sekta hii ikiwa bajeti yao ikiendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi kwa Wizara hii ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yenye maono, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa jumla (kitaifa); utangulizi; mipango bora ya matumizi ya ardhi ni msingi muhimu wa maendeleo endelevu ya vijiji, usalama wa milki za ardhi, uwekezaji wenye tija, uhifadhi wa mazingira, kupunguza migogoro ya ardhi na kukuza uchumi wa wananchi. Hata hivyo, kasi ya kufikiwa kwa vijiji vyote nchini bado ni ndogo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo za kifedha, kiufundi, kiutawala na kiteknolojia. Ili kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa, ipo haja ya kuwa na mkakati wa kitaifa wenye kasi, ufanisi na ushirikishwaji mpana kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa kimkakati na kiutendaji; kuanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa Wingi *(Mass Land Use Planning Programme)*. Wizara ianzishe mpango maalum wa kitaifa wenye malengo mahsusi ya kila mwaka badala ya kufanya mipango kwa mtawanyiko usio na kasi. Aidha, mfumo huu uzingatie ratiba ya kitaifa ya utekelezaji kwa awamu; malengo ya kila wilaya na kila mkoa; mfumo wa kufuatilia utekelezaji kidijitali; na upimaji wa utendaji kwa maafisa wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake ni pamoja na kuongeza uwajibikaji; kuondoa urudufu wa kazi; kurahisisha usimamizi wa rasilimali; na kuongeza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia teknolojia za kisasa za kidijitali; moja ya sababu ya ucheleweshaji ni matumizi ya mifumo ya zamani ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa. Hivyo Wizara inashauriwa kuongeza matumizi ya *GIS (Geographic Information Systems); drone, satellite imagery; GPS* za kisasa; na mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia hizi zisaidie katika uchoraji wa ramani kwa haraka badala ya kutegemea upimaji wa kawaida unaochukua muda mrefu.

Pia utambuzi wa matumizi halisi ya ardhi kama makazi, kilimo, misitu, malisho, hifadhi na maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhifadhi taarifa kitaifa na kupunguza upotevu wa nyaraka na kuongeza uwazi. Aidha, kuongeza ushirikiano na sekta binafsi, Wizara pekee haiwezi kufanikisha kazi hii kwa kasi inayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ianzishwe mfumo rasmi wa ushirikiano na kampuni binafsi, vyuo vikuu, taasisi za utafiti, na wataalamu binafsi wa mipango miji na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa *Accredited Planning Firms,* makampuni yaliyoidhinishwa yapatiwe kazi kwa viwango maalum vya kitaifa ili kuongeza nguvu kazi, kuongeza ushindani, na kupunguza miundikano wa kazi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga uwezo wa halmashauri za wilaya; changamoto kubwa ipo katika uhaba wa Wapima Ardhi, Wataalamu wa *GIS*, wapangaji miji, na Maafisa Ardhi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Wizara ifanye yafuatayo; kuajiri wataalamu zaidi kwa kuzingatia mahitaji ya kila wilaya; kutoa mafunzo endelevu katika *Geographical Information System (GIS),* upangaji shirikishi, usimamizi wa migogoro, matumizi ya *drone*, na mifumo ya kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuanzisha vituo vya kikanda vya kitaalamu vitakavyosaidia wilaya nyingi kwa pamoja. Aidha, kurahisisha taratibu za kisheria na kiutawala, baadhi ya hatua za uidhinishaji huchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inashauriwa kupunguza urasimu, kuharakisha vibali, kutumia mfumo wa kielektroniki wa

uidhinishaji, na kuweka muda maalumu wa kushughulikia kila hatua. Kwa mfano, mpango wa matumizi ya ardhi usizidi miezi sita kuandaliwa na miezi miwili kuidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuongeza ushirikishwaji wa wananchi; mipango mingi hukumbwa na migogoro kwa sababu wananchi hawashirikishwi vya kutosha. Hivyo basi ushirikishwaji uwe katika utambuzi wa mipaka, upangaji wa maeneo, maamuzi ya matumizi ya ardhi, na utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake ni kuongeza umiliki wa wananchi; kupunguza migogoro; kurahisisha utekelezaji; na kuongeza uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzisha kanzidata moja ya kitaifa ya ardhi; taarifa nyingi za ardhi zimetawanyika, hivyo Wizara iunde *National Integrated Land Information System*. Mfumo huu uwe na ramani zote, hati, mipango ya matumizi ya ardhi, taarifa za vijiji, maeneo ya hifadhi, na taarifa za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake ni pamoja na kurahisisha maamuzi; kuzuia migogoro ya mipaka; kuvutia wawekezaji; na kuongeza uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka kipaumbele kwa vijiji vyenye migogoro mikubwa kwa kuandaliwa *priority index* ya vijiji kulingana na migogoro ya wakulima na wafugaji, shinikizo la uwekezaji, ongezeko la watu, ukataji miti, na migogoro ya mipaka. Hii itasaidia kupunguza migogoro mapema, kuzuia uvamizi holela, na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuweka mfumo wa ufadhili endelevu; mipango mingi husimama kwa ukosefu wa fedha. Vyanzo vya fedha kama bajeti ya Serikali; washirika wa maendeleo; halmashauri; miradi ya kimataifa ya mazingira; na ushirikiano wa umma na sekta binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuunganisha Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Uchumi wa Vijiji; mipango isiwe ya kinadharia

pekee, bali ihusishe maeneo ya kilimo cha kisasa, maeneo ya viwanda vidogo, masoko, maeneo ya mifugo, uhifadhi wa mazingira na miundombinu. Hii itasaidia kuongeza mapato ya wananchi, kuvutia uwekezaji, na kukuza uchumi wa vijiji.

Kuhusu kuimarisha ufuatiliaji na tathmini; Wizara iwe na mfumo wa kupima idadi ya vijiji vilivyopangwa, ubora wa mipango, utekelezaji wake na athari zake kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mfumo uwe na dashibodi ya kitaifa; taarifa za kila robo mwaka; ukaguzi wa kitaalamu; na mfumo wa kutoa mrejesho kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuweka mkazo katika uendelevu wa mazingira; mipango izingatie vyanzo vya maji, misitu, maeneo oevu, njia za mifugo na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya haraka ya utekelezaji; ili kuongeza tija ya utekelezji mawazo yafuatayo yanaweza kutumika au kuboreshwa kwa ajili ya matumizi.

Na.	Kipindi	Hatua
1.	Miezi 6	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali
2.	Mwaka 1	Kukamilisha tathmini ya vijiji vyote
3.	Miaka 2	Kuongeza wataalamu na vifaa
4.	Miaka 3 – 5	Kufikia vijiji vingi nchini
5.	Miaka 5 –10	Vijiji vyote kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ili kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi, Wizara inapaswa kuhamia kwenye mfumo wa matumizi makubwa ya teknolojia, ushirikiano mpana, usimamizi wa kidijitali, ushirikishwaji wa wananchi na utekelezaji wa kimkakati wenye malengo yanayopimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya mpango huu yatasaidia kupunguza migogoro ya ardhi, kuongeza usalama wa milki, kuvutia

uwekezaji, kuhifadhi mazingira na kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri, mtoa hoja ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kufika siku ya leo tukiwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuweza kumsaidia katika nafasi ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuwashukuru sana wapiga kura wangu kutoka Jimbo la Ruangwa. Kwa kweli wanazidi kuniamini na kuniunga mkono huku wakijua kuwa kwa dhamana niliyopewa ni ya kitaifa. Mara nyingi ninawa-*miss* kuwa jimboni, lakini wanaelewa kuwa jambo hili ni la Wana-Ruangwa na ni jambo la kitaifa na tunaendelea kuchapa kazi kwa kulinda nchi yetu kupitia shughuli zote zilizopo katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee tena kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Baba huyu amekuwa mwalimu kwangu, amekuwa mlezi kwangu na amenifanya kweli niwe msaidizi wake kwa kunipa majukumu ambayo naendelea kumsaidia. Ana miongozo pale ambapo anaona ninakosea ananiambia fanya hivi. Ninakushukuru sana sana, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumshukuru mke wangu Elizabeth Eston Mbilinyi. Jana alikuwa hapa ametoka Ruangwa akiwa na watoto wake akasema naomba nije kushuhudia tukio hili. Kazi yake kubwa anayoifanya ni kunifanya niwe imara kwa kunipa utulivu, lakini

ananiongoza katika sala ya kumtegemea Mungu katika kazi yangu. Ninamshukuru sana kwa malezi anayoyafanya kwenye familia yangu wakati mimi naendelea kufanya shughuli za siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru sana sana Wabunge wote kwa kuchangia vizuri huku mkiwa na nia njema ya kuleta mabadiliko yenye kuleta matokeo kwenye Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi mmezungumza mengi na mnategemea Wizara hii ifanye mabadiliko na sio mabadiliko tu, tulete majibu ambayo yataleta tabasamu kwa wananchi. Mimi ninawashukuru sana Wabunge. Ninajua tulikotoka ni mbali, lakini tulikotoka huko kuna mengi yamefanyika. Wengi mmeshukuru kwa mambo mengi mazuri ambayo yamefanyika. Ninawaombeni tuwe sehemu ya kuleta matokeo na tuwe sehemu ya kuleta majawabu. Mliyoyaleta sio malalamiko, ni mapendekezo ya maboresho. Tunaendelea kuwa na ninyi, ninawaombeni sana tutakavyokuwa tunatembelea kwenye wilaya au majimbo yenu tuwe sehemu ya kuleta tabasamu kwa wananchi. Ninawashukuru sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaeleza mambo machache tu na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi atafanya ufafanuzi wa hoja katika maeneo mbalimbali ambazo mmeeleza katika michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa eneo la utoaji wa hati. Waheshimiwa Wabunge wengi mmekiri hapa kuna changamoto kubwa sana katika eneo hili la utoaji wa hati. Ni ukweli tulikotoka huko ndiko hali ilivyo, lakini kama jambo hilo umelifuatilia kwa kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan utaungana na Wizara hii kusema kuna mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwaka 2021 tulitoa hati ndani ya mwaka mmoja hazikuzidi hati 67,331. Hivi ninavyoongea mwaka huu tu katika mwaka mmoja tumetoa hati 107,683 na hatujamaliza mwaka. Nilishawaambia Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo alinipa majukumu mahsusi sana katika eneo hili la kutoa hati kuhakikisha tunatoa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliniambia simamia Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi, simamia eneo la utoaji wa hati, simamia mifumo yote ya Wizara ili ilete ufanisi na tija katika kazi zetu. Nilimwambia ahadi yangu kwake ni kutolala na kuhakikisha kuwa kila mmoja atapata hati. Nitakuja kwenye eneo kama hili siku yoyote ile kuja kuwaambia nani hajapata hati ambaye ameomba nitamtafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawahakikishia kila mmoja mwenye kipande cha ardhi, anayemiliki kihalali, aliyeomba mwenyewe akimaliza wajibu wake wa kuambatisha viambatisho vyake vyote huku akijihakikishia eneo hilo ni la halali, halina mgogoro wowote, huna sababu ya kutopata hati, utapata hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ila tu ukija na vikwazo ambavyo kuna mgogoro ukaomba lazima kwenda mbele na kurudi utakuwa umesababisha wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe wito kwa Wabunge na Watanzania wote, kumiliki ardhi ni haki yako tena ni haki ya kikatiba na haki hiyo sisi tunakupa ile hati kama kutimiza wajibu, wewe wajibu wako ni kuhakikisha eneo lako hilo unalilinda kwa kutafuta hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba viwanja vingi tunamiliki Watanzania, lakini hatuombi kumiliki kisheria. Ninawasihi sana maeneo yote ambayo yana mipango pia yana *master plan,* lakini yamepimwa na mchoro wake umekuwa *approved*, tafadhali ombeni hati na utapewa. Ninawahakikishia kwenye mifumo yote ukiomba hiyo hati unaweza kupewa chini ya saa 48 kama viambatisho vyote umefanya usipoweza unapewa baada ya siku 14. Ninaombeni sana tufanye hivyo eneo hilo na ninaomba kwa kuwahakikisheni hayo, Waziri wangu huyu ameeleza na tumewaeleza kwenye hotuba hii tunataka mikoa yote iwe na mfumo huu wa *e-Ardhi.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tufanye hivyo, sasa hivi tuna mikoa mitano, lakini tuna halmashauri 41. Ninaombeni sana twende tukafanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmezungumza huku chini kuna watumishi ambao wana changamoto katika kutoa huduma bora. Katibu Mkuu wetu yuko mahiri sana, Kamishna yuko mahiri sana, Makamishna wote wa Mikoa mmewasifia wako mahiri sana. Hatuna watumishi wengine isipokuwa hawa ndio tuliokuwa nao. Tusiwabeze, tuwatie moyo. Kazi kubwa wanayofanya, matokeo tunayopata ni wao ndio wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kazi yetu tutawasimamia watumishi hawa na kuchukua hatua. Ninyi wenyewe mmeona kuna watu ambao wamefukuzwa, kuna watu ambao wameshushwa mishahara, kuna watu ambao wameshushwa vyeo na kuna wengine wapo kwenye uchunguzi ili shughuli zingine za kisheria ziendelee. Ninawahakikishia tutaenda kuboresha utendaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili mmezungumza sana kuhusu mfumo wa kiutendaji. Mnapendekeza wengine watumishi wetu wa ardhi waende kwenye halmashauri, wengine waende Wizarani. Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yako wazi kabisa. Tunaenda kuanzisha *commission* ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa. Ile *commission*, kwa kifupi tu ona kama *TARURA* ilivyo, ona kama *TANROADS,* ona kama *DUWASA*, ona kama *DAWASA* ndio mfumo huu ambao utakuwa unaenda kusimamia sekta hii ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hakutakuwa na huo mkanganyo na hiyo itakuwa kuanzia juu mpaka chini. Ninawahakikishia kwa mfumo huu, taratibu zote zinaelekea kumalizika. Mheshimiwa Rais ninadhani baraza lake anaweza kupitisha kwa haraka na mambo mengine tukayaleta katika mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja uniruhusu kwa dakika tano. Kuna Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele alisema hapa…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Dakika mbili Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Dodoma ndugu yangu Mheshimiwa Paschal alisema hapa anataka kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kabla sijasema lolote, ninaomba tu ujiandae kuona, mwachie shilingi yake na wewe uunge mkono hoja bajeti hii tupitishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu nimkumbushe kuna mambo mazuri sana yamefanyika Dodoma toka jiji hili mwaka 1973 ilivyotangazwa mkoa huu kuwa makao makuu ya nchi hii kuna mambo mengi yamefanywa pamoja na kuandaa *master plan* ambayo ipo na ambayo tunaitekeleza sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya sisi kama sekta ya ardhi ni kuandaa *detailed plan* ya kila maeneo ya kimkakati. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo, maeneo yote ya kimkakati ni lazima yapangwe. Leo hii utakuwa shuhuda, tumeshirikiana na wewe katika kupanga maeneo ya Kitelela.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Kitelela unayoiona ile pale ni kwa sababu ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaomba tu nikuhakikishie, maeneo yote ambayo umeyasema jana nasema tu machache Matumbulu, Chigongwe, Mpunguzi, Mbabala, Zuzu na maeneo mengine yote ya kimkakati, tayari tumeshakubaliana na Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo hapa tunaenda kuandaa mpango wa kina wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yameendelezwa tutaweka jinsi gani ya kurasimisha, lakini tutashirikiana na sekta zote katika upangaji ili Jiji na wao wahusike, Wizara ya Maji, Ujenzi, barabara na umeme ili tunavyopanga tuwe kitu kimoja. Leo hatutaki maendeleo yakienda mtu mwingine aturudishe nyuma kwa ajili ya kwenda kufanya ubomoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo nikasema nieleze ili ndugu yangu asichukue shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri wa Wizara hii.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kumwita mtoa hoja nina tangazo la wageni.

Tunao wageni 62 wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi na wanachama wa klabu ya *Green Awareness* kutoka Jijini Arusha. Ahsante sana, karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni mtoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote sisi hapa afya njema na pia kuniwezesha mimi kusimama tena hapa kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Mbunge wa Ruangwa ambaye ameongea hivi punde na ni kweli anafanya kazi kubwa sana katika maeneo aliyoyaongea hapo ikiwa ni pamoja na kusimamia mambo ya hati na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee nikupongeze wewe na Mwenyekiti kwa namna ambavyo mmeendelea kuendesha shughuli za Bunge kwa kipindi chote ambacho Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanajadili hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri ambayo imetoa ushauri na maoni ambayo yanalenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Niwahakikishie kwamba Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Kamati kwa ukaribu mkubwa sana ili kufikia malengo ambayo tumeyaainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge waliochangia hotuba yangu ya bajeti ni 29 ambapo wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wabunge wote kwa michango yao ambayo ni mizuri na itatusaidia sana katika kuboresha utendaji wa sekta ya ardhi. Aidha, itatuwezesha kufikia malengo ya Wizara na kutatua changamoto mbalimbali za wananchi kwa lengo pana la kuwapa wananchi wetu furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru Wabunge wote waliotoa pongezi na ushauri kwa Wizara. Aidha, hoja zote zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana na tutazizingatia mpaka kwenye nukta. Hata hivyo kwa sababu ya muda nitatolea ufafanuzi baadhi ya hoja kwa ujumla wake na tutahakikisha kila hoja inajibiwa kwa maandishi na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi vijijini imepata uchangiaji mzuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Korogwe vijijini ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Vilevile, Mheshimiwa Jafari Chege wa Rorya, Mheshimiwa Taska Mbogo wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masanja Kadogosa wa Bariadi Vijijini, Mheshimiwa Ali Khalil Mirza wa Kiembe Samaki na leo Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kutoka Tabora.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri hamna haja ya kutaja majina na yote hayo, endelea tu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tunakubaliana na maoni yao kwamba waandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ni nyenzo

muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji mali, kuzuia migogoro hasa ya wakulima na wafugaji, vilevile kuboresha makazi na hatimaye kufikia malengo tuliyojiwekea kwenye Dira 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye hotuba yangu, azma ya Mheshimiwa Rais ipo wazi kabisa kwenye hili ambapo inalenga kuhakikisha kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi inaongezeka. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni 48.11 na kati ya shilingi hizo bilioni 9.71 ni matumizi ya kawaida, lakini sehemu kubwa ambayo ni shilingi bilioni 38.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hii ni ongezeko kwa 378% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zitawezesha kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 1,492 pamoja na kuandaa hati za hatimiliki za kimila 87,000. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau ili kuongeza uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji zaidi. Ninapenda kutumia fursa hii kuzielekeza halmashauri ambazo zimekasimiwa mamlaka za upangaji kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na masuala ya mipango miji na uendelezaji wa maeneo chakavu nchini ambayo imechangiwa pia na Waheshimiwa kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba usimamizi na uendelezaji wa miji unaongozwa na mipango ya jumla na mipango ya kina. Mipango hiyo inatoa mwongozo wa mgawanyo wa matumizi mbalimbali, kiwango cha uendelezaji, aina ya miundombinu na huduma zinazotarajiwa kutolewa kulingana na idadi ya watu inayotarajiwa kuishi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa mamlaka za upangaji nchini kusimamia kwa ukamilifu mipango iliyopo ili kuleta tija na kuboresha mandhari ya miji na kiwango cha huduma zinazopaswa kutolewa katika miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja iliyotolewa na Kamati ambayo pia imechangiwa na baadhi ya Waheshimiwa kuhusu kurejeshewa 20% ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi ili kuipa nguvu Wizara kutekeleza majukumu ya kukusanya, kupanga, kupima na kusambaza mifumo ambayo hoja hii tumeipokea kwa furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru Serikali kutuwezesha katika ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kwa mwaka huu hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 191 mpaka ilipofika tarehe 15 Mei, 2026 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya shilingi bilioni 50 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo haya hadi tunavyozungumza sasa hivi hapa yamefikia shilingi bilioni 203. Sina budi kuishukuru sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuweza kuona umuhimu wa urejeshaji wa 20% ya fedha za makusanyo ya kodi ya pango la ardhi ili ziweze kusaidia kazi ya ukusanyaji, upangaji, upimaji na usambazaji wa mifumo. Ninatambua kuwa suala hili linafanyiwa kazi na Serikali kupitia kikosi kazi cha maboresho ya sera za kikodi. Bila shaka katika muda mfupi ujao itakamilika na kufanyiwa maamuzi katika ngazi zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa kadhaa walizungumza vilevile kuhusu changamoto zilizopo katika ulipaji wa fidia kwa wakati na kuzingatia bei ya soko. Katika kuhakikisha kuwa wananchi wanalipwa fidia stahiki maeneo yao yanapotwaliwa kwa manufaa ya umma, Wizara imetoa Waraka Na. 2 wa Uthamini na Ulipaji Fidia wa mwaka 2024 ambao umeelekeza kwamba Wizara, mamlaka za mikoa, wilaya, taasisi za umma, taasisi binafsi, mashirika ya umma, mamlaka za halmashauri za miji na wale wote wanaohusika kulipa fidia wanapaswa kwanza kuthibitisha uwepo wa fedha kwa ajili ya malipo ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nitumie fursa hii kuzielekeza hizo mamlaka zote zinazotwaa ardhi kuzingatia taratibu hizi za utoaji wa ardhi na kulipa fidia stahiki na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (KKK) ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Ninapenda kuwataarifu kuwa Wizara imejipanga kuongeza kasi ya kupanga ardhi katika maeneo ya miji na vijiji kwa kushirikiana na sekta binafsi. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuchukua hatua madhubuti kwa halmashauri zote zilizokopeshwa fedha kurejesha fedha hizo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliarifu Bunge lako kuwa kwa sasa Wizara imeboresha utaratibu wa urejeshaji wa fedha za mikopo kwa kuwa na namba ya kumbukumbu ya malipo yaani *control number* inayotolewa wakati wa mauzo ya viwanja; hatua ambayo itawezesha fedha za mikopo kulipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Wizara, tofauti na ilivyokuwa utaratibu hapo awali. Aidha, nitumie fursa hii kuzipongeza zile halmashauri ambazo zimekamilisha marejesho ya fedha walizozikopa na vilevile kuzitaka halmashauri ambazo hazijakamilisha kufanya hivyo mara moja, ni vizuri kutii sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua umuhimu wa matumizi ya mfumo katika kuboresha utoaji wa huduma bora ambayo pia itapunguza gharama na muda wa ufuatiliaji kwa wananchi. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukufahamisha kuwa Wizara inaendelea na zoezi hili, kuhakikisha mfumo wa *e-Ardhi* unasambazwa katika halmashauri zote hapa nchini na tutaongeza kasi kwa mwaka huu 2026/2027. Miongoni mwa kazi tutakazozifanya ni kubadilisha kumbukumbu za ardhi kutoka nakala ngumu kwenda nakala tepe na kuboresha mifumo kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, imechangiwa pia na wachangiaji wengi. Ninapenda kukufahamisha kuwa Wizara imepokea ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na niseme kuwa tutaendelea na kazi ya kuandaa mwongozo wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na tutashirikisha wadau mbalimbali wanaohusika katika mnyororo mzima

wa upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha andiko maalum kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Nyumba. Mfuko huu utakapoanzishwa utawezesha Serikali kuwa na fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo ilitolewa na Mbunge wa Monduli na nimuombe tu Mheshimiwa Isack Copriano aridhie tukutane naye pamoja na wataalamu ili kutafuta ufumbuzi wa malalamiko ambayo aliyaainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimhakikishie kwamba nipo tayari kufanya ziara jimboni kwake ili tusikilize malalamiko ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi kwa pamoja. Nachelea kutoa maamuzi hapa kabla sijapata taarifa za kina, nisije nikaleta mgogoro mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kinondoni pia tuliambiwa kwamba Halmashauri ya Kinondoni ni miongoni mwa halmashauri 169 nchini zinazohusika katika utekelezaji wa programu ya urasimishaji makazi nchini. Aidha, mwenendo wa utekelezaji wa shughuli hizo haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Tarimba Abbas, tutakwenda pamoja katika jimbo lake na Wilaya nzima ya Kinondoni, kwa sababu nimeshangaa kuambiwa kwamba hata Magomeni watu wanakaa kwenye nyumba ambazo hazina hati, ambapo nilikuwa naamini ni mji wa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2026 jumla ya makazi 66,175 yametambuliwa katika eneo lake na kurasimishwa, lakini kama bado mengine, tutaendelea kuyafanyia kazi ili maeneo yote yaweze kurasimishwa. Bila shaka yoyote, kuna haja ya kuongeza kasi, naahadi kwamba tutakuja katika suala hilo tukiwa na kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usimamizi wa watumishi waliopo halmashauri limeongelewa na Waheshimiwa wengi. Ninapenda kusema kwamba Serikali ilifanya uamuzi huo kuhamisha

mamlaka ya nidhamu kule, lakini kutokana na hoja sasa zinazoendelea kutolewa, Wizara itakaa chini na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi ili kuangalia namna bora ambayo watumishi wale watatoa tija kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Kamisheni ya Ardhi kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza ambayo itashughulikia sekta nzima ya ardhi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. Kamisheni hiyo itakuwa na jukumu la kusimamia watumishi wake kama zilivyo taasisi nyingine za Serikali, mfano *RUWASA, TARURA* na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 Toleo la mwaka 2023 hii ilikuwa ni ahadi ambayo iliyotolewa na Mheshimiwa Rais na yeye alitolea maelekezo. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba yote hayo yatazingatiwa na mamlaka hiyo ikianzishwa tutakua hatuna hoja ya kuuliza watumishi wako wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kunti pia aliulizia suala la Chemba, nimhakikishie kwamba tutakwenda kama tulivyomuahidi ili tuweze kutatua matatizo yaliyopo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kiteto, ndugu yangu Mheshimiwa Olelekaita, analifahamu, tulizungumza na nilimuahidi kufika kule na mpaka sasa hivi ile taarifa ya wataalamu imeshakamilika na tutapanga tu ni lini twende naye tukaiseme kwa pamoja kule ili wananchi wa Kiteto wapate furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi kutopewa milki za ardhi katika maeneo ya hifadhi za bahari na madai ya fidia katika Jimbo la Mtwara Vijijini, nimhakikishie Mheshimiwa Premji kwamba wawekezaji wa nje huwa hawapewi hati zile ambazo wanapewa wananchi wa Tanzania, wao wanapewa *derivative,* hawapewi zile zile zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tutaliangalia vilevile kama ambavyo ameliongea ili tukifika kwake na huyu yuko njiani

ninapoenda nyumbani kwetu Masasi napitia kwake. Kwa hiyo, tutakutana pale, tutalizungumza tuone tunalikamilisha namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya maeneo ya wazi imechangiwa sana nayo, tunatoa rai kwa halmashauri zote kulinda maeneo yaliyowazi. Maeneo yaliyowazi siyo kwa ajili ya kazi nyingine yoyote, bali ni kuufanya mji upumue na wananchi wapate sehemu za kupata burudani, waweke bustani kule, wananchi wakaondoe *frustration*. Tunaambiwa kwamba unavyopita kwenye bustani akili zinapumzika kidogo. Kwa hiyo, niwatake wote wa halmashauri, maeneo ya wazi wajenge bustani ili wananchi wetu wapate sehemu za kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kutokana na ufinyu wa muda, Waheshimiwa Wabunge wengi hawakupata nafasi ya kuchangia hotuba zao, naomba niwahakikishie kuwa tutakuwa tayari kwa wakati wowote kupokea ushauri, maoni na changamoto kutoka kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa leo tulipata vilevile michango ya Waheshimiwa Wabunge kadhaa, upimaji wa mashamba hoja iliibuliwa na Mheshimiwa Nawanda, tumeipokea kwa ari kubwa, tutajipanga kwa kushirikiana na halmashauri na vyama vya msingi ili tutekeleze jambo hili ambalo tunaamini kwamba ni muhimu mashamba yetu nayo yawe yamepimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea pia ushauri wa kupima miji, tunatambua umuhimu wa kufanya hivyo. Mheshimiwa Mariam Mungula, pia alizungumzia upungufu wa nyumba nchini tunautambua na sisi tunasema tutakuwa na sera ya nyumba na makazi, itaunganisha mambo ya nyumba na mambo ya makazi, uboreshaji wa nyumba na makazi na hii sera imeshaanza kufanyiwa kazi na zoezi linaendelea. Itakapokamilika tutaiwasilisha katika mamlaka husika ili iweze kurasimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kutoka Tabora alitoa pongezi nyingi kwa watendaji wa Wizara na mimi kwa niaba yao nazipokea; pongezi kwa Kamishna, pongezi kwa *DG*

National Housing, pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi alizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimfamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa mwaka huu tutapanga vijiji 1,492 na tutaendelea na hiyo kasi hadi tumalize vijiji vyote 12,333. Tulipata vilevile hoja ya kupanga matumizi bora ya ardhi nchi nzima, Mheshimiwa Mbunge akirejea kwenye hotuba yangu atagundua kwamba tunao huo mpango na nilitoa taarifa kuwa tunanunua ndege ambayo itatusaidia kwenye zoezi hili na mambo yatakuwa mazuri, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paresso alizungumzia Mabaraza ya Ardhi na nimshukuru sana, kwa sababu alitoa historia ndefu kuhusu kuanzishwa kwa mabaraza haya na sababu zilizosababisha yaanzishwe. Akasema hali ilivyo sasa ni kweli siyo Wilaya zote zina mabaraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi, katika hotuba yangu nimesema kupitia kwa mwaka huu unaokuja, tutaanzisha Mabaraza ya Ardhi kwa wilaya zote zilizobaki na vilevile tutateua Wenyeviti wa Mabaraza ambayo hayana Wenyeviti. Aidha, nimwelekeze Katibu Mkuu sasa aanze mchakato wa kujaza nafasi zilizowazi kwa Wenyeviti wa Mabaraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwita Waitara, huyu ni mkali sana, Mheshimiwa Mwita Waitara tulipanga kwenda Tarime kweli tukatatue tatizo lililopo kule. Ahadi yangu nimhakikishie kwamba ipo palepale na nimwombe Mheshimiwa Waitara, kwa sababu huyu ni mwanafunzi wangu wa kemia na alikuwa mwanafunzi bora kabisa wa kemia pale *University of Dar es Salaam* na alipata *marks* nzuri; sasa asimnyang'anye shilingi mwalimu wake, najua hawezi kushika shilingi. Sasa utashikaje shilingi ya mwalimu wako?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge amekiri mwenyewe kuwa Wizara ina mambo mengi. Kwa hiyo, najua kwamba anajua tutakuwa tunafanya mambo mengine kabla hatujaenda kwake, lakini kwake tutafika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia ilitolewa ya wanawake kupewa nafasi ya kumiliki ardhi. Ninaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba mwezi Machi mwaka huu tulikuwa na Kliniki ya Samia Ardhi. Hii ilikuwa mahususi kwa akina mama, lakini kama mnavyojua, walikuwa akina mama na akina baba tu. Na akina baba pia walikuja na tuliwahudumia akina mama zaidi ya 12,000. Hoja ilikuwa ni kuwapa elimu kuhusu umiliki wa ardhi, lakini vilevile kama kuna matatizo ya umiliki tuyashughulikie na walifurahi sana baada ya ile kliniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nisisitize kwamba kliniki hizi zimekuwa na manufaa sana. Tumepata pongezi nyingi sana kwa kuendesha hizi kliniki, ni leo tu hapa ndiyo nimesikia kwamba kliniki zina matatizo kidogo, lakini mara zote tumekuwa tunaambiwa kwamba kliniki zimesaidia sana. Kama kuna mapungufu tutayaboresha ili kliniki ziwe na manufaa zaidi ya pale ambapo tumefikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo nataka niichangie ni ya Mheshimiwa Rashid Mtima, nafikiri yeye alizungumzia ukuaji wa miji ambapo akasema Tanzania inaongoza kwa asilimia tano. Nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba hoja ya ukuaji wa miji imekuwa ni hoja nzito sana katika mikutano ya Bara la Afrika hata ya kidunia. Nakumbuka tulivyokuwa Nairobi kwenye Mkutano wa *African Urban Forum* lilizungumziwa sana na ilikuwa ni lengo mahsusi la mkutano huo na mapendekezo yalitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulivyokuwa tena kwenye *World Urban Forum* kule Azerbaijan limezugumzwa pia. Siyo Tanzania tu peke yake ni karibu dunia nzima kwa sababu kuna sababu zinazofanya watu waje mijini. Lakini nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Tanzania tumepunguza *push factors* zinazowaondoa wananchi kijijini, zinazowakimbiza ikiwa ni pamoja na mambo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa hivi *REA* imetapakaa karibia nchi nzima, ni vijiji vichache sana ambavyo bado havijapata huduma hii, lakini mambo ya maji, shule, barabara na mitandao ya simu za mkononi ni vitu ambavyo vitapunguza kasi ya wananchi kwenda mijini

kwa sababu tutapunguza hiyo wanaita *push factor*. Lakini *pull factor* bado ipo, miji inakuwa vizuri, inapendezeshwa vilevile, kwa hiyo watu pia wanaitamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kufikia hapo, niseme tu Wizara yangu itafanyia kazi mapendekezo yote ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa siku ya leo na jana, vilevile na niwapongeze sana kwa kwa maoni yenu na tunasema kwamba yale ambayo sijayaongelea hapa tutayaleta rasmi kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, sema unatoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

KITABU CHA PILI

Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*……Sh.12,536,076,172

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hili ndiyo fungu ambalo lina mshahara wa Waziri na hapa ninayo majina matatu. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

MHE. KUNTI Y. MAJALA. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, sina nia wala dhamira ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, lakini ninatamani tu atusaidie Wabunge kwa niaba ya wananchi kwamba suala la migororo limekuwa ni adha kubwa sana kwa Taifa letu. Hata hivyo, wakati anahitimisha hapa amesema kwamba watashuka chini na kati ya Wizara ambayo imekuwa nzito ni Wizara ya Ardhi, pamoja na changamoto zote zilizopo, lakini tumeendelea kumuona Waziri kutoshuka chini na kuweza kuwasikiliza wananchi kwenye suala zima la utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitamani kupata tu kauli ya Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, nini mkakati? Kwa sababu tuna migogoro ya aina mbili; tuna migogoro hii midogo midogo, lakini tuna migogoro mikubwa ambayo iliundiwa Tume ya Mawaziri Nane na ile tume ikaundiwa kamati ndogo za wataalamu, na hizo kamati ndogo zilishafanya tayari tathmini, walishafanya kazi yao na taarifa ziko mezani, na Mheshimiwa Waziri uzuri amekiri hapa kwamba taarifa ziko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kujua na kupewa ufafanuzi wa kina, ni nini kauli ya Serikali juu ya hatma ya migogoro hii ya Tume ya Mawaziri Nane, pamoja na kamati ndogo ama timu ndogo za wataalamu zitakwenda kusomwa kwa wananchi ili wananchi wetu waweze kujua hatma ya migogoro yao ni nini ndani ya Taifa lao?

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yangu niliyoitoa jana nilieleza kwamba Serikali ilifanyia kazi na jumla ya shilingi 95,000,000,000 zimeshalipwa kwa baadhi ya wananchi waliostahili, na vilevile nilisema kwamba maamuzi yameendelea kutekelezwa ikiwemo kurejesha ardhi kwa wananchi ambapo ekari 3,000,000.13 zimerejeshwa na shilingi bilioni 95.27 zimelipwa kwa wananchi waliostahili kulipwa fidia katika maeneo 14. Aidha, mpango kazi kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobaki umeandaliwa na unaendelea kutekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwishaandika barua kwa Mawaziri wale ambao walihusika ili tukutane na tuweze kuangalia namna ya kulikamilisha suala hili na nina uhakika tutafika katika maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyauliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi sina dhamira ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, lakini nilitamani tu nipate ufafanuzi juu ya watumishi wa Wizara na watumishi wa ardhi ambao wapo chini ya Wizara ya Ardhi, lakini wanafanya kazi kwenye Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwamba mpango uliopo ni wa kurudisha Kamisheni ya Ardhi, lakini lazima tujue kwamba mpango huu mpaka kuja kuanzisha Kamisheni ya Ardhi utahitaji mabadiliko ya sera yenyewe ya sasa ilivyo, lakini lazima mtakwenda na mtagusa sheria kwa sababu lile ni dude kubwa ambalo linakwenda ku-*combine* wataalam wa aina mbalimbali. Kwa wakati huu ambao sasa hivi watendaji wale wanaitika chini ya Wizara ya Ardhi, lakini wanafanya kazi TAMISEMI kuna *contradiction* ya kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu utumishi wao unasoma chini ya Wizara ya Ardhi kwa maana ya Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi,

lakini wanafanya kazi TAMISEMI kiutendaji, na kwa kwa kuwa mamlaka ya upangaji yapo TAMISEMI kwa sasa, hii *contradiction* wakati mwingine mtumishi wa ardhi anaweza akawa ni afisa ardhi, anaweza akawa ni mthamini *(surveyor)* au *town planner* anapewa maelekezo na Kamishna wa Ardhi, wakati huo anatumia vitendea kazi na shughuli zote chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *contradiction* wakati mwingine wanashindwa kujua wanaitika wapi na watimize wapi kwa wakati ambapo yanaweza yakatoka maelekezo kwenye pande mbili na Wizara mbili tofauti ambazo mmoja ni msimamizi wa sera, mmoja ni mtendaji ambaye anatakiwa kuhakikisha kwamba ardhi inapangwa na kupimwa, kama msimamizi wa mamlaka ya utendaji kwenye ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani nijue Mheshimiwa Waziri kama haoni hili kwamba pamoja na kwenda kutengeneza Kamisheni ya Ardhi ambayo itahitaji muda kidogo, kwa nini kwa sasa yasifanyike mabadiliko kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi katika Serikali ili watumishi hawa sasa warejee TAMISEMI kwa wakati huu? Wakati kamisheni itakapokuja kuanzishwa sasa tutakwenda kuwahamisha wataalamu wote ili tujue ni wangapi wanakwenda kuitika kwenye kamisheni ili kutokutengeneza mkanganyiko wa sasa ulivyo katika utendaji wa watumishi wa Wizara ya Ardhi. Nilikuwa natamani nipate kauli ya Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Chege tutaifanyia kazi pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa sababu ni suala la Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, sina nia mbaya na Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo.

Kwanza, nimpongeze kwa hotuba yake nzuri. Hata hivyo, eneo ambalo ninaomba nipate ufafanuzi ni eneo ambalo migogoro ya hifadhi nyingi za halmashauri zetu, lakini pia na maeneo ya watu binafsi na hifadhi za Serikali, *TFS, TANAPA*. Kulikuwa na muingiliano mkubwa sana na migogoro hii ndiyo inayosababaisha hata wafugaji wetu wengi wakamatwe kimakosa na kuingizwa kwenye hifadhi zetu, na migogoro hii imechangia kwa kiasi kikubwa sana wafugaji hawa kuipeleka Serikali mahakamani na wafugaji wanashinda hizi kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate ufafanuzi, mfano tu ambao ni wa hali halisi kabisa, ukifika kule kwangu kuna *Usumbwa Forest Reserve,* ni pori ambalo ni la halmashauri lenye *GN number* ya mwaka 1958, lakini wakati Hifadhi ya Msitu wa Kigosi inashushwa hadhi, lilichukuliwa lote likaingizwa kwenye Hifadhi ya Msitu wa Kigosi, pori lote. Kwa hiyo, nataka nipate, maeneo mengi kumekuwa na migogoro hii. Ni nini mkakati mkubwa wa Wizara hii kwenda kuweka mipaka halisi ya wananchi na kuitafsiri vizuri ili kuondokana na kero hii?

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Cherehani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nimeelezea namna ambavyo Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ilivyowezeshwa mwaka huu, na nilisema kwamba katika miaka minne iliyopita, idadi ya vijiji vilivyopimiwa matumizi ya ardhi imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana na mwaka huu, tume imepewa shilingi 48,000,000,000 kama nilivyoongea hivi punde na sehemu kubwa ya hii fedha inakwenda kupanga matumizi bora ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa ni suluhu ya kutosha kuondoa matatizo yote ambayo yamezungumzwa kuhusu mipaka, kuhusu matumizi ya ardhi kama ni ya wafugaji au ya wakulima. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Cherehani kwamba masuala haya yatafanyiwa kazi na mwaka huu tutapitia vijiji 1,492 kwa fedha hii. Hata hivyo, tumeahidiwa kwamba Wizara itaendelea kupokea fedha

kiasi hiki kwa miaka mitano ijayo ili vijiji vyote 12,333 hapa nchini viwe na matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Naona wameridhika wote, kifungu kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*.

Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…….Sh.1,254,184,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*…….Sh.1,233,280,482
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*……..Sh.1,624,916,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……..Sh.554,068,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*……..Sh.755,044,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*……Sh.550,700,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*……Sh.741,084,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*……..Sh.629,284,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*……Sh.16,411,156,200
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*……Sh.14,239,751,400
Kifungu 2003 - *Registration of Titles Unit*……..Sh.1,415,500,000
Kifungu 2004 - *Valuation Department*……Sh.5,756,023,390
Kifungu 2005 - *Dar Es Salaam Land Office*……Sh.900,000,000
Kifungu 2007 - *Dodoma Land Office*……Sh.850,000,000
Kifungu 2008 - *Tabora Land Office*……..Sh.600,000,000
Kifungu 2009 - *Mwanza Land Office*……Sh.834,000,000
Kifungu 2010 - *Kilimanjaro Land Office*……Sh.630,000,000
Kifungu 2011 - *Mtwara Land Office*……Sh.520,000,000
Kifungu 2012 - *Mbeya Land Office*……..Sh.684,828,000
Kifungu 2013 - Simiyu Land Office……Sh.510,362,000
Kifungu 2014 - *Arusha Land Office*……..Sh. 644,716,000
Kifungu 2015 - *Geita Land Office*……Sh.530,000,000

Kifungu 2016 - *Njombe Land Office*……..Sh.530,000,000
Kifungu 2017 - *Katavi Land Office*……..Sh.530,000,000
Kifungu 2018 - *Coastal Land Office*……..Sh.654,023,000
Kifungu 2019 - *Iringa Land Office*……..Sh.500,000,000
Kifungu 2020 - *Kigoma Land Office*……..Sh.548,545,000
Kifungu 2021 - *Lindi Land Office*……..Sh.530,000,000
Kifungu 2022 - *Mara Land Office*……..Sh.645,000,000
Kifungu 2023 - *Morogoro Land Office*……..Sh.730,000,000
Kifungu 2024 - *Ruvuma Land Office*……..Sh.570,000,000
Kifungu 2025 - *Shinyanga Land Office*……..Sh.550,000,000
Kifungu 2026 - *Singida Land Office*……..Sh.524,000,000
Kifungu 2027 - *Tanga Land Office*……..Sh.674,000,000
Kifungu 2028 - *Kagera Land Office*……..Sh.600,000,000
Kifungu 2029 - *Rukwa Land Office*……..Sh.500,000,000
Kifungu 2030 - *Songwe Land Office*……..Sh.500,000,000
Kifungu 2031 - *Manyara Land Office*……..Sh.529,403,000
Kifungu 3001 - *Human Settlement Development Department*……..Sh.9,862,278,356
Kifungu 3002 – *Real Estate Unit*……..Sh.769,584,000
Kifungu 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*……..Sh.6,362,486,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 3 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Kifungu 2010 - *Southern Highlands Regions Zonal Offices*……..Sh.380,925,500
Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*……..Sh.4,036,777,037
Kifungu 1003 - *Procurement and Management Unit*……..Sh.228,545,200
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……..Sh.581,602,000
Kifungu 2001 - *Directorate of Land Use Planning, Management Coordination Division*……..Sh.957,608,500

Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance and Information*……..Sh.1,046,615,000

Kifungu 2003 - *Zonal Offices*……Sh. 0
Kifungu 2004 - *Northern Zonal Offices*……Sh.275,339,016
Kifungu 2005 - *Eastern Zonal Offices*……Sh.572,243,500
Kifungu 2006 - *Southern Zonal Offices*……Sh.183,399,016
Kifungu 2007 - *Western Zonal Offices*……Sh.365,053,216
Kifungu 2008 - *Lake Zonal Offices*……Sh.463,472,000
Kifungu 2009 - *Central Zonal Offices*……Sh.375,103,015

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 3 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Kifungu 1001- *Directorate of Corporate Services*……Sh.1,350,195,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……Sh.191,150,000
Kifungu 2001 - *Directorate of Land Use Planning, Management and Coordination Division*……Sh. 31,922,272,000
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance and Information*……Sh.482,000,000
Kifungu 2004 - *Northern Zonal Offices*……Sh.631,697,500
Kifungu 2005 - *Eastern Zonal Offices*……Sh.631,697,500
Kifungu 2006 - *Southern Zonal Offices*……Sh.631,697,500
Kifungu 2007 - *Western Zonal Offices*……Sh.631,697,500
Kifungu 2008 - *Lake Zonal Offices*……Sh.631,668,500
Kifungu 2009 - *Central Zonal Offices*……Sh.631,697,500
Kifungu 2010 - *Southern Highlands Regions Zonal Offices*……Sh.664,227,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*……..……..Sh.1,316,500,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*…….……Sh.177,000,000
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*…….……Sh. 2,063,700,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……..……Sh.159,902,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*…….……Sh.170,042,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*…….……Sh. 730,429,000
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*……..……..Sh. 66,692,489,000
Kifungu 3001 - *Human Settlement Development Department*…….……Sh. 324,900,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi.

MWENYEKITI: Bunge linarejea

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja. *(Makofi)*

T A A R I F A

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Hivyo, ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa kanuni zetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Naamini walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii na tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii ya mwaka wa fedha 2026/2027.

Hata hivyo, niwapongeze Kamati yetu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mwenyekiti pamoja na Makamu na Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa mnayoifanya kusimamia sekta hii. Pia Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia, tunawapongeza sana na tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya machache, naahirisha Shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.44 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 1 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)